

# **KUONEKANA KWA MWENYEZI MUNGU**

**مسألة الرؤية**

**Kimeandikwa na:**  
Hasan bin Ali Saqqaf

**Kimetarjumiwa na:**  
Amiri Mussa Kea

ترجمة  
مسألة الرؤية

تأليف

الشيخ حسن بن علي السقاف

من اللغة العربية إلى اللغة السواحلية

© Haki ya kunakili imehifadhiwa na:  
Al-Itrah Foundation

**ISBN No:** 978 - 9987 -17 - 049 - 4

**Kimeandikwa na:**  
Hasan bin Ali Saqqaf

**Kimetarjumiwa na:**  
Amiri Mussa Kea

**Kimehaririwa na:**  
Alhaji Hemedi Lubumba

**Kimesomwa Prufu na:**  
Al-Haj Ramadhani S. K. Shemahimbo

**Kimepitiwa na:**  
Al-Haj Mujahid Rashid

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**  
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Agosti, 2016  
**Nakala:** 1000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**  
Alitrah Foundation

S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania.  
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555  
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com  
**Tovuti:** www.ibn-tv.com  
**Katika mtandao:** www.alitrah.info

---

---

# **YALIYOMO**

---

Utagulizi.....	vii
Neno la Mchapishaji .....	1
Dibaji .....	3
Kuonekana kwa Mwenyezi Mungu Dunianina Akhera .....	4
Hadithiya 1:.....	7
Hukumu juu ya Hadithi hii .....	8
Hadithi ya 2:.....	10
Hadithi ya 3:.....	11
Hadithi ya 4:.....	16
Hadithi ya 5:.....	19
Hadithi ya 6:.....	21
Hadithiya 7:.....	23
Hadithi ya 8:.....	27
Hadithi ya 9:.....	28
Hadithi ya 10:.....	30
Hadithi ya 11:.....	33

Hadithi ya 12:	34
Hadithi ya 13:	34
Hadithi ya 14:	35
Hadithi ya 15:	37
Hadithi ya 16:	38
Hadithiya 17:	39
Hadithi ya 18:	41
Hadithi ya 19:	42
Hadithi ya 20:	46
Hadithi ya 21:	48
Hadithi ya 22:	49
Hadithi ya 23:	50
Hadithi ya 24:	51
Hadithi ya 25:	53
Hadithi ya 26:	54
Hadithi ya 27:	55
Hadithi ya 28:	56

Hadithi ya 29:	58
Hadithi ya 30:	58
Hadithi ya 31:	60
Hadithi ya 32:	61
Hadithi ya 33:	62
Hadithi ya 34:	63
Hadithi ya 35:	65
Uchambuziwa Hadithi Isemayo: “Ewe Ambaye Macho Hayamuoni” .....	67
Yaliyopoke wa katika Qur’ani Tukufukuhususalala la kuonekanakwa Mwenyezi Mungu .....	68
Kauliza Wana zuo nimiongonim wa Ahlus-Sunnahnawengineo, ambao hawathibitishisuala la kumuona Mwenyezi Mungu walaha wa semi hivyo .....	77
Kukirik wa Hafidh Ibn Hajar .....	87
Daliliza Kiakili ambazo baadhi ya watu wana dai kuwa zina thibiti shak wamba Mwenyezi Mungu ataonekana .....	94
Kadhiaya Mtume kumuona Mwenyezi Mungu (azzawajaal) usikuwa Israina Miraji .....	99
Faida yenye kustaajabishanakushangaza .....	108

Kutaja yaliyopo kewa kutoka kwa Ibn Abbas kuhusuhilo.....	109
Yale yaliyopo kewa kutoka kwa Bwana wetu Abu Dharrkatikamadahiyo.....	114
Katika Hadithi ya Abu Dharr: “Ni Nuru, Nitamuonaje?” .....	118
Kumuona Mwenyezi Mungu (azzawajaal) usingizini nimuhali.....	120
Manenoya Nawawina Bajouri katika suala la kuonekana kwa Mwenyezi Munguna Ubainifu ambao una oneshaudhaifun akosa .....	125
Kauliya Bajouri katika kitabu Sharhul-Jawharatna Mjadala wake .....	127

---

## UTANGULIZI

---

**K**itabu hiki ni toleo la Kiswahili la taasisi ya Al Itrah Foundation. Chapisho lake limelenga kukidhi mahitaji ya kiroho ya zama hizi pamoja na Ubongo na fikra zinazokuwa za Muislam. Jitihada kubwa zimefanywa na Taasisi kuweka chapisho hili la Kiswahili katika msingi wa haki na wenyewe kukubalika katika Uislam.

Unaombwa kwa Taadhima ukisome kitabu hiki katika malengo yaliyokusudiwa.

Pia Unaombwa kuwasilisha kwetu maoni yako huru juu ya chapisho letu hili, jambo ambalo tutashukuru sana.

Kutangaza ujumbe wa Uislam ni kazi ambayo inahitaji ushirikiano wetu sote. Taasisi inakuomba kuungana na kushirikiana kama ilivyoagizwa katika aya ya Qur'ani: (Surat Saba' 34:46).

Na rehma za Allah ziwe juu yako.

Wako katika Uislam

Al Itrah Foundation

Barua Pepe: [alitrah@yahoo.com](mailto:alitrah@yahoo.com)

SMS: +255 778 300 140

## NENO LA MCHAPISHAJI

*Kuonekena kwa Mwenyezi Mungu* ni utafiti uliofanywa na mwandishi wa kitabu hiki juu ya suala la kuonekana au kutokuoneka kwa Mwenyezi Mungu.

Kuna hitilafu kidogo katika madhehebu zetu za Kiislamu juu ya masuala mbalimbali, lakini nyingi ya hitilafu hizo sio katika misingi ya Uislamu. Hata hivyo kuna nyingine ambazo zinaweza kumtia mtu katika shirki, kama hii ya kuonekana au kutokuonekana kwa Mwenyezi Mungu au kumfananisha kwa umbo na viungo.

Katika kitabu hiki mwandishi amefanya utafiti wa kina juu ya suala hili kwa kutumia ushahidi uliopo kwenye Qur’ani, Hadithi na matukio ya kihistoria, na kufikia hitimisho zuri la kumtakasa Mwenyezi Mungu kutokana na dhana hizi za kishirikina.

Sisi kama wachapishaji, tunakiwasilisha kitabu hiki kama kili-vyo kwa wasomaji wetu na kuwashauri wasome yaliyomo, wayafanyie kazi na kuyazingatia na kufaidika na hazina iliyomo ndani yake.

Hii ni moja kati ya kazi kubwa zinazofanywa na Taasisi ya Al-Itrah katika kuwahudumia kielimu wasomaji wake wazungumzaji wa Kiswahili. Na kwa maana hiyo hiyo imeamua kukichapisha kitabu hiki chenye manufaa makubwa kwa lugha ya Kiswahili kwa lengo lake lilelile la kuwahudumia Waislamu, hususan wanaozungumza Kiswahili.

Hivyo, ni matumaini yetu kwamba wasomaji wetu watanufaika vya kutosha kutokana na kitabu hiki, kwani tumekiona ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi tena katika akili za watu.

Tunamshukuru mwandishi wa kitabu hiki Ustadh Hasan bin Ali Saqqaf kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa ajili ya Ummah huu wa Waislamu, Allah Azza wa Jallah amlipe kila la kheri na amuingize Peponi kwa salama na amani insha'Allah. Halikadhalika tunamshukuru Ndugu yetu Amiri Mussa kwa kukitarjumu kwa Kiswahili kitabu hiki, insha'Allah na ye ye Allah Azza wa Jallah amlipe kila kheri hapa duniani na Akhera pia, bila kuwasahau na wale wote waliochangia kwa namna mmoja au nyingine mpaka kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na Akhera pia.

**Mchapishaji  
Al-Itrah Foundation**

---

## DIBAJI

---

**S**ifa zote njema zinamstahiki Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu, rehema na amani zimfikie bwana wetu Muhammad na ndugu zake watakatifu ﷺ. Ama baada: Makusudio ya msingi ya kuandika kitabu hiki ni kwamba wakati wa kuanza mchakato wa uandaaji; madhumuni yalikuwa ni uwasilishaji wa hadithi mbalimbali zinazohusu suala la kuonekana kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t), kisha kuichunguza hadithi moja baada ya nyingine na kumjibu Ibn Qayyim Jawziyya na Mahanbali kwa imani yao ya kwamba Mwenyezi Mungu ana mwili, na madai yao ya uwepo wa tawaturi ya hadithi za kuonekana kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t). Kisha baada ya kumaliza uwasilishaji huo na kuziweka wazi hadithi hizo, baadhi ya wasomi na ndugu zetu wenye kujali mambo haya, wote waliniomba niandike utafiti huu kwa kutaja Aya ambazo zimepokewa kuhusiana na maudhui hii. Aidha kadhia ya Mtume Muhammad ﷺ kumouna Mola manani usiku wa Miiraji, basi nikawakubalia ili kufanikisha ombi lao hilo. Kwa hivyo nikaamua kuleta utafiti huu kwa mpangilio huu, na kabla ya kuanza mchakato huu nilikuwa nikijiuliza je, niziweke Aya mwanzoni mwa kitabu au hapana. Lakini nilifikia uamuvi wa kuandika utafiti huu na kufuata utaratibu wa kutanguliza hadithi kwanza na mwishowe Aya. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atupe uongofu, taufiki na msaada.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

---

## KUONEKANA KWA MWENYEZI MUNGU DUNIANI NA AKHERA

---

*Kwa jina la Mwenyezi Mungu  
Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.*

**S**ifa zote njema zinamstahiki Mwenyezi Mungu aliyetukuka Mwenye uwezo, kisha rehema na amani ziwe juu ya mbora wa viumbe, mbashiri na muonyaji, na juu ya Aali zake taa za uongofu, kama kuchomoza kwa mchana na kuondoka kwa usiku.

Ama baada ya hayo: Kwa hakika viongozi wa wale wenye imani ya kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) ana mwili wamekusanya hadithi ambazo zimeeleza kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) ataonekana Siku ya Kiyama,<sup>1</sup> na ametaja Hafidh Ibn Hajar katika kitabu chake *Fat'hul-Bari* Juz. 13 Uk. 434, kwamba hakika Ibn Qayyim naye ni mionganini mwa maimamu au viongozi wa imani ya kuwa Mwenyezi Mungu ana mwili na anafanana na viumbe. Amezikusanya hizo katika kitabu chake *Hadiyul-Arwah*, akasema:

“Amekusanya Daru Qutni njia za hadithi zilizopokewa kuhusiana na suala la kuonekana kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) na zika-zidi hadithi ishirini,<sup>2</sup> akazifuatilia Ibn Qayyim katika kitabu chake

<sup>1</sup> Na wenye imani ya kuwa Mwenyezi Mungu ana kiwiliwili, tangu hapo zamani katika historia ya Kiislamu ni wenye kutuhumiwa kwa suala la kuonekana kwa Mwenyezi Mungu, na wanaihesabu itikadi hiyo kuwa ni mionganini mwa misingi ya itikadi na wanatunga vitabu vingi na risala lukuki, na itikadi hiyo ndio kitenganishi baina yao na Jahmiyyah na wengineo.

<sup>2</sup> Na nyingi kati ya hizo ni zenyenye kukanushwa na zilizobuniwa, bali zote, na kitabu cha kuonekana kwa Mwenyezi Mungu kimehusishwa na Daru Qutni, naye kwetu sisi ni mtu mwenye kuweka imani ya kuwa Mwenyezi Mungu ana umbile na utengenezaji wao wa

*Hadiyul-Arwaah* basi zikafikia thelathini, na nyingi kati ya hizo ni nzuri.<sup>3</sup> Na akaegemeza Daru Qutni kutoka kwa Yahya bin Muiin, amesema: Ninazo hadithi 17 sahihi kuhusu kuonekana kwa Mwenyezi Mungu.”

Na zote hizo hazikubaliki kwetu kama utakavyoona katika utafiti na upembuzi huu yakinifu, na hakika amedai Ibn Qayyim kwamba zipo hadithi zinazojulisha juu ya kuonekana kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) na kwamba kwa hakika zimekuwa ni mutawatiri! Na sio hivyo! Bali ni hadithi zilizopokewa na mtu mmoja na zenyekupondwa, nazo kwetu sisi ni zile zilizotengenezwa na kubuniwa na hata kama zipo katika vitabu sahihi, nazo zimezagaa katika umma huu, kwa mfano zipo za kutoka kwa Kaab bin Akhbar, na zipo katika vitabu sahihi, na zipo za kutoka kwa Abdullah bin Salama na mfano wa hao wawili. Na yule aliyesoma utangulizi wetu na mstari wetu wa pambizo katika kitabu *al-Uluwu* cha Dhahabi amelijua hilo na amekuwa na yakini kutoka kwake kwa kukithiri ushahidi na uwepo wa dalili mbalimbali.

Na suala la kuonekana kwa Mwenyezi Mungu au itikadi ya kuonekana kwake limetia dosari kanuni ya Tawhid na kumpweke-sha Mwenyezi Mungu na kumtakasa na yale yasiyomhusu, aidha limemfanya yeye ni kama vile mtu au viumbe wengine, ana sura na umbo, bali mawazo ya makundi mengi ya wale wenye kushikamana na imani ya kuonekana kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t), ambao wanalingatia hilo kuwa ni msingi ambao haiwezekani kuepukana nao, yamejikita katika kuona kwamba Mola Muumba ana sura, mguu, uso, macho mawili, mdomo, kidaka tongue, magego, ugoko, dhiraa, kifua, unyayo na vidole na yeye anashuka, anapanda, anaweka unyayo wake motoni, na yasiyokuwa hayo mionganoni mwa mielekeo

---

kiubunfu kama lilivyobainika hilo katika Risala mahsusii.

<sup>3</sup> Maneno haya sio sahihi kama utakavyoona katika utafiti na uhakiki huu.

inayopatikana kutokana na mawazo ya Wagiriki, Wayunani, itikadi za Mayahudi na wenge imani ya kuwa Mwenyezi Mungu ana mwili, na mfano wa hao.

Kwa nadharia hii kuwa yeye ana mwili anakuja mara nyingine kwa sura isiyo halisi kama wanavyowaza, na wakati mwingine kwa sura yake halisi, na anawafunulia wao ugoko wake kisha anaenda zake na wanamfuata yeye<sup>4</sup> na wao wanamuona, wanazungumza naye na wanatembea nyuma yake... hadi mwisho!!

Je, baada ya hayo umebakia ufananisho mwengine?! Na asili ya suala hilo ni itikadi ya kuonekana kwa Mwenyezi Mungu, hakuna shaka zikibainika dalili za kisheria juu ya ubatili wake, yataadharaaulika na kutupiliwa mbali mambo yote hayo au aghlabu yake.

Na suala la kuonekana kwa Mola Manani ni mada au maudhui muhimu mno kwa wale wenge imani ya kuwa Mwenyezi Mungu ana mwili na kumfananisha Yeye na kitu kingine, wameandika nyaraka na vipeperushi mbalimbali! Na huo ndio mpaka tenganifu kwao kati ya Majahmiyya na Masunni, hakika wamehadaika baadhi ya wale wenge kujishughulisha na elimu kwa ushawishi wao na upitukaji mipaka wao na yale wanayoyataja kutokana na hadithi kuhusiana na maudhui hii na kuwapeleka kwenye yale wayatakayo! Na wakakumbwa na ufuataji wa ububusa wale ambao hawana uwezo wa usahihishaji wa athari na utambuzi juu ya udhaifu wake, na kujua sababu zake na yale yasiyohusika kwa kumfanya mtu fulani kuwa ni sahihi. Na kurudisha athari hizo katika *Sahihi* ya fulani si chohchote isipokuwa ni uunganishaji wa mawazo na ufuataji mbaya katika mlango huu ambao unahitaji uhakiki, jitihada na uchunguzi

<sup>4</sup> Hayo yote yapo katika hadithi ya sura iliyopingwa na kukataliwa katika *Sahih* mbili, na sisi tunamuepusha mbora wa viumbe ﷺ kuwa ameyatamka hayo, na lahudhi “Basi anaondoka zake (yaani Mola Manani) na wanamfuata yeye” katika haki ya Mola Manani aliyetukuka mtazikuta hizo katika *Sahih Muslim*, Uk. 190.

yakinifu!! Kwa hakika imenistaajabisha kauli ya Jallahu Dawwani rafiki yangu katika utangulizi alioueleza katika kitabu *Al-Aqaidul-Adhadiyyat*, anasema:

“Na wala sikuungana pamoja na watu wa ‘imesemwa na inasemwa,’ kama ilivyozoleka kwa watu wa mijadala, wazembeaji wasiweza kufuata njia za utoaji wa dalili, bali nimefuata haki iliyo wazi hata kama watakwenda kinyume nayo watu mashuhuri, na nimechukua kwa muktadha wa dalili hata ikiwa makala za jamhuri hazikusaidia hilo.”

Maneno haya mazuri yanayotoka kwa mtu mfano wake ni mazuri yapaswa kufikiriwa na kuzingatiwa, hakika mfuasi wa leo na wa hapo kabla tunawaona wanatetea na wanazingira na wanakoroga ili kuhalalisha neno au makala au fikra mbaya iliyosemwa na baadhi ya wale waliotangulia. Mfuasi huyo anamuona kiongozi wake kuwa ni Qur’ani iliyoteremshwa bila dosari wala kosa, hivyo yeye hugeuza na kubadilisha ili kuthibitisha kinga na umaasumu juu ya anayemfuata au mheshimiwa wake!! Hata kama taawili yake katika njia ya utengezaji wa neno batili ni ufisadi na uovu wa dhahiri!! Basi ni upi wajibu wetu kuhusiana na mfano wa watu hawa!! Na Mwenyezi Mungu (s.w.t) ndiye Mwenye kuombwa msaada, na Yeye ndiye Mwenye kutegemewa.

Na tuzipitie na kuziperuzi zile hadithi ambazo amezitaja Ibn Qayyim katika kitabu chake *Haadiyul-Arwaah Ila Bilaadil-Afraah* uk. 269, tuzitaje hizo kulingana na malezi yake na tuziperuzi moja baada ya nytingine na Mwenyezi Mungu ndiye mwafikishaji na mwezeshaji:

**Hadithi ya 1:** Amesema huko baada ya kutaja majina 25 ya Masahaba na pia mmoja hakutaja jina lake, na akaanza katika kubainisha hadithi moja baada ya nytingine na hili ndilo andiko lake:

“Ama hadithi ya Abu Bakr Swiddiq ﷺ, amesema Imam Ahmad bin Hanbali: Ametuhadithia Ibrahim bin Is-haaq Twaliqani amesema: Amenisimulia Nadhr bin Shumail Maazini amesema: Amenihadithia Abu Naamat amesema: Amenisimulia Abu Haniida Barrau bin Nuufal kutoka kwa Waalan Aduwiyy kutoka kwa Hudhai-fat kutoka kwa Abu Bakri Swiddiq ﷺ, amesema: Mtume ﷺ صلی اللہ علیہ وسّع نعمتہ ameemah aliha wasala ya asubuhi akakaa....”

Na akataja hadithi ndefu ya uombezi ambayo ndani yake ni kwamba watu watatokwa na majasho Siku ya Kiyama na uendaji wao kwa Manabii, nayo ni hadithi ya kubuni iliyoingizwa na kusimuliwa katika umma huu kutoka katika vitabu potofu vya kale na Abdullah bin Salam Myahudi, basi baada ya kupita muda akaigeuza na kudai ni hadithi iliyopokewa kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, na huenda ameihadithia Kaab bin Akhbar pia, na hakika nimeitaja katika yale niliyoyaandika katika kitabu *al-Uluwu* na ukusho wake kutoka kwa Ibn Salam, basi arejee mwenye kupenda kujuua zaidi, kuchunguza zaidi, kupata mwamko na kuondokana na vinara wa watoaji matusi na kuelekeea na kuukumbatia ufuataji wa kibubusa na ushabiki!!

Na mahala pa ushahidi katika hadithi na dalili kutoka kwake juu ya kuonekana kwa Mwenyezi Mungu ni kauli yake kuhusu hilo wakati wa kutaja uombezi wa bwana wetu Mtume Muhammad ﷺ na sajda yake chini ya kiti cha enzi cha Mwenyezi Mungu, kama vile wanavyodhani: “Akasema: Basi anainua kichwa chake, akiangalia uso wa Mola Wake Mlezi anaporomoka chini hali akisujudu kwa kadiri ya Ijumaa nytingine, ndipo Mwenyezi Mungu anamwambia: “Inua kichwa chako na sema unasikilizwa...”!!

### **Hukumu juu ya hadithi hii:**

Ni kwamba: Sanad yake ni dhaifu sana na matini yake ni batili. Ama kuhusu sanad ya hadithi hii ambayo ameichukua Ibn Qayyim kutoka

kitabu *Musnad Ahmad* Juz. 2, uk. 4, kwa hakika sanad ya hadithi husika ni dhaifu mno!! Na zingatieni ubainifu ufuatao:

Hafidh Ibn Hajar amesema katika kitabu *Lisanul-Miizan*, Juz. 6 uk. 263, na katika kitabu *Taaqilul-Manfaat*, Juz. 1, uk. 436, katika Wasifu wa Walaan baada ya kunukuu ukweli wa Ibn Muiin na usahihishaji wa Ibn Haban: “Daaru Qutni katika kitabu *Ilal* amesema: ‘Sio mashuhuri, na hadithi sio thabiti.’”

Na Ibn Naama ambaye jina lake kamili ni Amru bin Isa bin Swedi bin Hubairat Aduwiyy Baswriy, Ibn Saad amemzungumzia katika kitabu *Twabaqaat*, amesema: “Ni kweli isipokuwa yeye alichanganikiwa kabla ya kifo chake.” Angalia kitabu *Tahdhiibul-Tahdhiib*, Juz. 8, uk. 76.

Na Waalan Aduwiyy hakupokea kutoka kwake ila Abu Huraira, naye kuna ikhtilafu katika jina la baba yake, pia hajulikani katika uhakiki wa hili, Daru Qutni amesema: “Sio mtu mashuhuri na hadithi yake sio thabiti.” Kama ilivyokwisha kutangulia. Na hana yeye hadithi katika vitabu tisa – pamoja na kwamba yeye hatokani na vikundi vilivyo kinyume na kinywaji cha watu wa hadithi kama ilivyodhiihiri – isipokuwa hadithi hii ipo katika *Musnad*, na kitabu hiki Musnad kimechezewa na kutiwa mikono ya wenyewe dhambi, hususan ukizingatia kwamba Dhahabi anasema katika kitabu *Siyaru Aalaam Nubalaalaa*, Juz. 13, uk. 522 kwamba Musnad sio katika vitabu vili-vyoandikwa na Ahmad bin Hanbali!!

Na Abi Hunaydat ambaye jina lake ni Baraai bin Nuufal na imesemwa ni Harith bin Malik, hakupokea kwake yejote kutoka mionganoni mwa waandishi wa vitabu tisa, kama vile alivyokuwa wa kabla yake kikamilifu, naye ni mionganoni mwa wale wenye kukubalika mbele ya Hafidh katika kitabu *Taqriib*, yaani ikiwa atafuatiliwa, waila basi yeye ni mlaini wa hadithi kama vile alivyosema katika utangulizi wa kitabu chake *Taqriibu*.

Na katika utangulizi wa maelezo ya hadithi isiyofaa, nayo ni kauli yake huko: Kwamba Mtume ﷺ baada ya kuswali Swala ya asubuhi “Alikaa hadi ulipofika wakati wa dhuha, akacheka kisha akakaa mahala pake hadi aliposwali Swala ya adhuhuri, Alasiri na Magharibi, alifanya yote hayo bila ya kuzungumza hadi aliposwali Swala ya Isha hapo akasimama na kuelekea kwa familia yake...”

Na matini pia ina kasoro kwa upande mmoja kwa kuhitilafiana kwake na hadithi ambazo zipo katika sahihi mbili, japo sisi hatuse-mi kuwa inatofautiana na zote, na hakika tumebainisha ikhtilafu inayopatikana kati yake katika yale tuliyoyaeleza katika mstari wa pambizo katika kitabu *al-Uluwu* wakati wa kuitolea maelezo hadithi nambari 49 na nyinginezo, na kutokana na maelezo hayo unajua kwamba si sahihi uzingatiaji wa kwamba hadithi hii ni nzuri, ulio-fanywa na Sheikh Shuaib Arnautwi au wale waliohakiki kitabu Musnad kilichochapishwa hivi karibuni na Taasisi ya *ar-Risalah*, vivyo hivyo maneno ya Sheikh Shuaib katika msitari wake wa pambizo katika kitabu *Al-Awaswim Wal-Qawaswim*, Juz. 5, Uk. 129 cha Waziri, aliposema: “Na sanad yake ni nzuri.” Na hadithi ni batili kama ilivyokwisha tangulia!!

**Hadithi ya 2:** Ibn Qayyim<sup>5</sup> baada ya hadithi ya kwanza katika kitabu chake *Haadiyul-Arwaah* amesema: “Na ama hadithi ya Abu Huraira na Abu Said imo katika sahihi mbili.....” Ametaja hadithi ndefu ya kuonekana kwa Mwenyezi Mungu - ametukuka na kutakasika kutokana na yale wayasemayo – kwamba atawajia watu kwa sura wasiyoijua ..... nayo hadithi ya sura ni yenye kuleta kinyaa na kichefuchefu!! Na kwayo imetaja suala la Mwenyezi Mungu kujifunua na kuuonesha ugoko wake!! Ametukuka Mola Manani na kuepukana na yote kwa utukukaji mkubwa! Nayo ni hadithi batili

<sup>5</sup> Ni kutoka katika kitabu *Al-Awaswim Minal-Qawaaswim*, Juz. 5, uk. 132 akinukuu kutoka katika kitabu *Haadiyul-Ar-waah*.

isiyokubalika, nayo ni riwaya ya Abu Huraira kutoka kwa Kaab bin Akhbar bila shaka kama vile hadithi ya udongo, na ndani yake kuna maovu ya kiyahudi ambayo Mwenyezi Mungu kwayo ni Mjuzi zaidi!! Na yule mwenye ushabiki na king'ang'anizi kwa kuzitetea *Sahih Mbili* kuwa hazina makosa, ye ye hakuchukua dhahiri ya hadithi na hivyo amekimbilia kwenye taawili kwa rangi mbalimbali za kupendeza za taawili zisizo na manufaa kwa *Sahih Mbili*!!

Na kufanya hivyo ni kwenda kinyume na maneno ya Mwenyezi Mungu ndani ya Kitabu Chake kitukufu aliposema: "Hakijiwi na batili mbele yake na nyuma yake." Wakati Mungu anasema hivyo juu ya Kitabu Chake Kitukufu watu hawa wanasema kwa lugha ya hali zao na usemajji wao kana kwamba wanamzindua Mwenyezi Mungu aliyetukuka kwamba: "Na *Sahihi Mbili* nazozhazijiwi na batili mbele wala nyuma."!!

Na amezungumza mja fukara juu ya hadithi hii katika vitabu vyake vingi na mistari ya pambizo, kwa mfano *Sahihu Sharhul-Aqidatil-Twahawiyat*.

### **Hadithi ya 3: Ibn Qayyim baada ya hayo amesema:**

"Na ama hadithi ya Jabir bin Abdillah Answari katika *Sahihi Mbili* kuhusiana na hadithi ya Ismail Ibn Abi Khalid kutoka kwa Qays bin Abi Hazim, amesema: Tulikuwa tumekaa pamoja na Mtume ﷺ basi akauangalia mwezi usiku wa mwezi kumi na nne, akasema: Hakika nyinyi mtamuona Mola Wenu Mlezi wazi wazi kama vile mnavyouona huu....."

**Nasema:** Hadithi hii ni batili ameiponda Juhabadha kutoka kwa wanahadithi wa zamani, na hakika Dhahabi amesema katika kitabu chake *Siyarul Aalaam Nubalaat*, Juz. 11, uk. 53, katika kisa kilichoko huko kwamba hakika Ali bin Madini alisema: "Hakika katika sanadi

kuna yule asiyefanyiwa kazi yeye wala yale anayoyapokea, naye ni Qays bin Hazim, hakika hakuwa ila ni bedui mwenye kutoa haja ndogo kisogoni.”

Na aliyojaribu Khatiib na Dhahabi<sup>6</sup> na mwenye kuwafuata hao wawili katika kulazimisha kwa hili au kulikana na kulibatilisha, yanakataliwa na kupingwa kwa sababu zipo kauli za kundi la Maimamu zenye kumponda Qays bin Abi Hazim katika kitabu *Tadhhibul-Kamaal*, Juz. 24, uk. 15, na kwamba hakika Yahya bin Abi Said Al-Qatwan alisema kuhusu Qays bin Abi Hazim: “Hadithi yake haikubaliki.” Na huko pia imepokewa kutoka kwa Ismail bin Abi Khalid, amesema: “Qays bin Abi Hazim aliihi hadi akavuka miaka 160 mpaka akachanganikiwa na kutokwa na akili.”

Na Yakub bin Shayba Saduusi amesema: “Na wamezungumza watu wetu kuhusiana na hilo, basi mionganoni mwao yupo yule aliyyenyanya uwezo au kadari yake na akamtukuza yeye na akafanya hadithi kutoka kwake ni yenyе sanadi sahihi zaidi. Na mionganoni mwao yupo mwenye kumbebesha tuhuma, amesema: ‘Anazo hadithi nyingi zinazokataliwa.’ Na wapo wale waliozibeba hadithi hizi kutoka kwake kwa wao kuzingatia kwamba si zenye kuchukiza kwao, wakasema hizo ni ngeni,<sup>7</sup> na mionganoni mwao yupo ambaye hawajambebesha tuhuma yoyote kuhusu hadithi bali katuhumu madhehebu yake, na wakasema alikuwa akimtuhumu Ali ﷺ na Masahaba wote, na lililo mashuhuri kutoka kwake ni kwamba ali-kuwa akimtanguliza Uthman, na kwa ajili hiyo wengi mionganoni

<sup>6</sup> Khatiib alikuwa ni Mhanbali kisha akawa Mshaafi! Na historia yake alitengeneza ali-pokuwa Mhanbali kama inavyodhihirika kutokana na yaliyopo ndani yake! Na Hanbali ni madhehebu yenyе chuki binafsi dhidi ya Ahlulbayti, na ni madhehebu yenyе kumzingatia Mwenyezi Mungu kuwa ana umbo, na ni yenyе kutetea hayo mawili! Na Dhahabi anatosha katika ubainifu wa uhakiki wa hali yake katika utangulizi wa kitabu chake *Al-Uluwu tulichokiandika!* Na Mwenyezi Mungu ni mwenye kuwajua!

<sup>7</sup> Na mageni yanatokana na shari ya elimu, kama vile ilivyonukuliwa kutoka kwa asiyekuwa mmoja mionganoni mwa wanahadithi wa kale.

mwa watu wa Kufa wa zamani walijiepusha kupokea riwaya kutoka kwake.”

Basi imebainika kutokana na hili kwamba hakika mtu huyu ni Naswibii, yaani ni mwenye kumchukia bwana wetu Ali ﷺ, na mwenye kumchukia bwana wetu Ali ﷺ ni mnafiki kwa andiko la mtaoji sharia, kwa mujibu wa hadithi sahihi ya Mtume ﷺ: “Ewe Ali! Hakupendi wewe ila mumini na hakuchukii ila mnafiki.”<sup>8</sup> Na mnafiki amepoteza uadilifu<sup>9</sup> kwa mujibu wa maneno ya Mwenyezi Mungu: “Hakika wanafiki watakuwa katika tabaka la chini kabisa motoni.” (Quran 4:145).

Na kutokana na nukuu hizi tulizonukuu inabainika kwa mtu mwenye insafu kwamba hakika maneno ya Khatwib:<sup>10</sup> “Hakika watu wa athari akiwemo Ali, wamekusanyika juu ya kuitolea hoja riwaya ya Qays na kuizingatia kuwa ni sahihi,” ni batili na hayakubaliki na yanatupiliwa mbali.

Na vivyo hivyo inabainika kwetu uhakika wa maneno ya Dhahbi katika kitabu *Mizan*: “Na yule ambaye amemzungumzia vibaya hakika ameiudhi nafsi yake”, nayo hayo ni katika maneno batili pia!!

Na ama yule ambaye ameiudhi nafsi yake ewe Dhahbi ni Qays bin Abi Hazim mwenye chuki na bwana wetu Ali, hakika huyu ndiye aliyeiudhi nafsi yake!! Maajabu yaliyoje haya!!!

<sup>8</sup> Ameipokea Muslim katika *Sahih* yake, uk. 78 na *Tirmidhi* hadithi 3736 na vitabu vinginevyo visivyokuwa hivyo viwili.

<sup>9</sup> Lakini hawa wenye chuki binafisi Manawasibu wenye kujidhihirisha kwa ufuutiliaji wa hadithi hawako tayari kufanya kazi hukmu ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake juu ya Masahaba wao na wapendwa wao, lakini sisi tunawakuta wamuonapo mtu wa haki anamkosoa bwana wao Muawiya wanawaambia watu kumhusu yeye na wanamlauimu yeye na wanajitenga naye, utawasikia: “Huyu anawaponda Masahaba ﷺ” pamoja na kuwa mtu hajawaponda Masahaba bali anamponda Muawiya!! Basi fikirieni na zingatieni katika vitendo yya wenye taasubi! Na vipi matamanio yanawachezea hao na kuwapotosha mbali na haki!!

<sup>10</sup> Mara ngapi Khatibu amekuwa na maneno mfano wa haya yasiyokubalika kwa kujitenga kwake mbali na ukweli!! Angalia kitabu *Taanibul-Khatib* cha Imam Kawthari رحمه الله.

Na hili linajulisha chuki aliyokuwanayo Dhahbi dhidi ya Ali, nalo ni jambo mashuhuri!! Vipi mwenye kumponda Qaysi huyu mwenye chuki dhidi ya Ali, ambaye anamtu humu bwana wetu Ali ﷺ na kumtukana na kumsema vibaya,<sup>11</sup> awe ni mwenye kuiudhi nafsi yake!!! Na wala halisemi hilo juu ya wale wenye chuki binafsi dhidi ya Ali akiwemo huyu Qays na Hariz ambaye alikuwa akimtusi Bwana wetu Ali, hasemi kuwa ameiudhi nafsi yake na kwamba riwaya yake haikubaliki!!! Bali anatamka wazi kuwa ni mwaminifu, ilihali ni mwongo mzushi hata kama Bukhari kaandika Hadithi yake katika *Sahih* yake.

Zaidi ya hapo hata tukiachana na suala la chuki binafsi bado kauli ya Dhahbi ni batili baada ya Mahufadhi wengine wengi kusema hali ya Qaysi katika maneno tuliyoyanukuu. Na Qaysi huyu alikuwa akiishi kwa kivuli cha Bani Umayyah, Serikali ambayo ili-kuwa ikimmiminia laana na matusi Bwana wetu Ali ﷺ, na ndio maana tunamuona Dhahbi akimtukuza aliyeitukuza!!

Kisha akanukuu Ibn Qayyim baada ya hatidhi ya Jarir bin Abdillah, majina ya watu wengi amedhani kwamba wao wameipokea hadidhi hii au wamekiri ukweli wake! Na hili ni mionganini mwa yale ambayo hayanenepesi wala hayaondoi njaa!! Na zipo hadithi ngapi dhaifu ambazo lau tutaziperuzi na kuchunguza wapokezi wake na majina ya watu waliopo katika mlolongo wa wapokezi wake (sanad zake) tutakuta ni wengi zaidi kuliko idadi hiyo aliyoitaja Ibn Qayyim Jawziyya! Nazo ni kati ya zile hadithi ngeni na za mtu mmoja! Na misingi ya dini haijengwi juu ya hadithi ngeni na ya mtu mmoja!

Na majina haya ameyanukuu Ibn Qayyim kutoka katika kitabu *Faaruq* cha Sheikh wa imani ya kwamba Mola Manani ana mwili,

<sup>11</sup> Baadhi ya wajinga wenye taasubi hulikuza na kulikanusha hilo licha ya kuthibiti kwake kutoka kwa Muawiya katika *Sahih Muslim*, kitabu ambacho ni moja kati ya vitabu viwili ambavyo haviingiwi na batili mbele wala nyuma!!

na ambaye ni mmoja kati ya maimamu wao wakubwa, Abu Ismail Answari Harawiy kama alivyoitaja hiyo Hafidh Ibn Hajar katika kitabu *Alfat'hu*, Juz. 13, uk. 427.

Kisha Ibn Qayyim Jawziyya baada ya orodha hiyo amesema:

“Watu wote hawa wameshudia juu ya Ismail ibn Abi Khalid, na akashuhudia Ismail bin Khalid juu ya Qays ibn Abi Hazim, na akashuhudia Qays ibn Abi Hazim juu ya Jarir bin Abdillah, na akashuhudia Jarir bin Abdillah juu ya Mtume ﷺ kama kwamba wewe unamsikia Mtume ﷺ naye akisema hilo na akilifikisha kwa umma wake, wala hakuna kitu chenye kutuliza macho yao kushinda hilo.

Ama Jahmiyyah, Mafirauni, Marafidhu, Qaramitwa, Batwin-  
iyya, Maswabiat, Majusi na Wagiriki wao wameshudia ukafiri wa  
yule mwenye kuitakidi hivyo, na kwamba ye ye ni mionganini mwa  
watu wenye kumfananisha Mwenyezi Mungu (s.w.t) na viumbe na  
ni wenye kumfanya ana mwili, na akawafuata katika hilo kila adui  
wa Sunna na watu wake, na Mwenyezi Mungu aliyetukuka ni Mnus-  
uru wa Kitabu chake na Sunna ya Mjumbe Wake hata wakichukia  
makafiri.”

Na ninasema baada ya maneno yake hayo: Hili litokalo kwake  
ni maneno ya kipuuzi! Hayana thamani yoyote ile katika vipimo vya  
kielimu! Kwani Ibn Qayyim ameugeuza ukweli na akasahau kwam-  
ba Sheikh wake, Al-Harrani, ni msemaji mwenye kuamini uazali wa  
ulimwengu na masuala mengine yaliyo mashuhuri! Na mwenye ku-  
amini hivyo ndiye anayefaa zaidi kunasibishwa na vikundi vidogo  
vidogo vya Swabiat Al-Harraniyyat au Wayunani! pamoja na kuwa  
maneno yake haya ni kutoka katika mlango wa khutuba zisizo na  
elimu! Na anaweza mtu yeyote kulisema hilo wakati wa kuwasilisha  
hadithi yoyote atakayo kuitetea! Na kila mwenye akili timamu ana-

jua kuwa maneno haya yamekorogwa, hata wanaoona kuwa hadithi ya Jarir ni sahihi wanalijua hilo!

Na sijui je, utafiti juu ya Wagiriki, Mafirauni na wengineo ni mionganoni mwa yale yalijotajwa hapa au hilo ni kwa ajili ya kuog-opesha na upotoshaji wa maneno?! Na lau tungeliambatanisha maelezo na ufanuzi juu ya kila neno analolisema, basi tungechafua kurasa katika kumjibu, kwani katika maneno yake kuna mapungufu mengi! Kwa sababu katika utangulizi wetu juu ya kitabu *al-Uluwu* katika kurasa zake za mwanzo nimefanya kazi ya kufafanua ni nani mwenye kuamini itikadi za Wagiriki, Wayunani na Mayahudi wenyewe kuona kwamba Mwenyezi Mungu ana kiwiliwili: Ni Ibn Qayyim Jawziyya na wafuasi wake wenyewe imani ya kwamba Mungu ana mwili, au ni watu wa haki wenyewe kumtakasa Mungu na hilo!!

Na Ibn Abi Hatam amesema katika kitabu *Al-Ilal*, Juz. 2, uk. 96: Nilimuuliza baba yangu kutokana na hadithi ambayo alitusimulia Umar bin Nadhru Nahrawaani kutoka katika kumbukumbu yake, kutoka kwa Zayd bin Harun, kutoka kwa Ismail bin Abi Khalid, kutoka kwa Qayyim ibn Abi Hazim, kutoka kwa Abu Bakri Swiddiq رضي الله عنه، katika maneno ya Mola Manani ‘Wale walifanya wema watapata wema na zaidi’ akasema: “Mema ni pepo na zaidi ni kuangalia uso wa Mwenyezi Mungu (s.w.t)”, basi nikamsikia baba yangu akisema: “Hadithi hii haina asili, ni yenye kuchukiza, na hili pia ni mionganoni mwa uzushi wa Qays bin Abi Hazim!!”

**Hadithi ya 4:** Kisha akasema Ibn Qayyim Jawziyya baada ya hayo: “Na ama hadithi ya Suhaib, ameipokea Muslim katika *Sahih* yake kutoka kwenye hadithi za Hamad bin Salama kutoka kwa Thabit bin Abdil-Rahman ibn Abi Layla kutoka kwa Suhail, kwamba Mtume صلی اللہ علیہ وسّع نعمتہ amesema: “Watu wa peponi watakapoingia peponi, Mwenye-

zi Mungu (s.w.t) atasema: ‘Je, mnataka kitu kingine nikuzidishieni?’ Watasema: ‘Haukuzifanya nyuso zetu kuwa nyeupe, je, haukutuingiza peponi na kutuokoa na moto?’ Akasema: Basi ataondoa pazia, hawatapewa chochote wakipendacho zaidi wao kuliko kumuangalia Mola Wao Mlezi. Kisha akasoma Aya hii ‘**Wale waliofanya wema watapata wema na zaidi.**’’ Na hadithi hii imepokewa na maimamu kutoka kwa Hamad na waliipokea kutoka kwa Nabii wao kwa kui-kubali na kuisadikisha.’’

**Nasema:** Hadithi hii imekataliwa pia, nayo inakwenda kinyume na hadithi zilizotangulia walizozisimulia! Katika hadithi hiyo ni kwamba uonaji utakuwa kwa waumini peponi, na hadithi zilizotangulia na hususani hadithi ya Abu Huraira na Abu Said ambayo ipo katika Sahih Mbili ni kwamba uonaji utakuwa baada ya ufufuo na utatokea kwa wanafiki.

Na hadithi nayo ni kauli ya Ibn Abi Layla, ameinukuu kutoka kwa baadhi ya watu wasiojulikana, na sio hadithi ambayo haina mlolongo wa wapokezi, na wala hakuipokea kutoka kwa bwana wetu Suhaibu kama alivyolibainisha hilo Daru Qutni, Tirmidhi na wengineo kama itakavyokuja Mungu akipenda.

Na kauli ya Ibn Qayyim “Hadithi hii imepokewa na maimamu kutoka kwa Hamad . . .” ni maneno yasiyo na thamani yoyote na in-awezekana kwa mtu ye yoyote kudai hayo kwa hadithi yoyote ile kama iliviyotangulia.

Na ama kuhusu hadithi husika, katika sanad yake yupo Hamad bin Salama, na hakika tumerudufu kwamba yeye hategemewi katika hadithi za sifa na yale yanayofungamana na Mwenyezi Mungu aliyetukuka na yasiyokuwa hayo, kama utakavyoyakuta hayo katika mstari wetu wa pambizo juu ya kitabu *Daf'u Shubhi Tashbihi Bi Akaffi Tanzih*, uk. 190 cha Hafidh Ibn Jawziyya, na katika uhakiki

wetu juu ya kitabu *al-Uluwu* mstari wa pambizo nambari 255 na sehemu nyinginezo.

Na hakika ametaja Tirmidhi katika kitabu *Sunan* 3030 kasoro, ila na dosari ya hadithi hii akasema: “Hadithi ni ya Hamad bin Salama, ni hivyo ameipokea asiyekuwa mmoja kutoka kwa Hamad bin Salama bila mlolongo wa wapokezi, na ameipokea Sulaiman bin Mughira hadithi hii kutoka kwa Thabit kutoka kwa Abdul-Rahman bin Abi Layla, na hakutaja humo ‘kutoka kwa Suhaib kutoka kwa Mtume’.” صلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ

Na ametaja Hafidh Dar Qutni hadithi hii katika kitabu chake *Al-Ilzaamat wa Tataabuu*, uk. 210, na akasema kwamba ni hadithi isiyo na sanadi kamili: “Na ameeleza Muslim hadithi ya Hamad kutoka kwa Thabit kutoka kwa Ibn Thabit kutoka kwa Ibn Abi Layla kutoka kwa Suhaib: ‘Wale waliofanya wema watapata wema na ziada’ haina mlolongo wa wapokezi. Na ameipokea Hamad bin Zaid kutoka kwa Thabit kutoka kwa Abi Layla.”

Na sanadi yake ni ngeni katika matabaka manne ya kwanza.

Na amesema Imam Nawawi katika kitabu *Sharh Sahih Muslim*, Juz. 3, uk. 17:

“Vivyo hivyo hadithi hii ameipokea Tirmidhi, Nasaai, Ibn Maaja na wengineo kutokana na riwaya ya Hamad bin Salama kutoka kwa Thabit, kutoka kwa Ibn Abi Layla, kutoka kwa Suhaib, kutoka kwa Mtume صلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ, Abu Isa Tirmidhi, Abu Masuod Damishi na wasio-kuwa hao wawili wamesema: ‘Hakuipokea yejote hivyo bila kutaja sanadi kutoka kwa Thabit ilia Hamad bin Salama. Na ameipokea Suleiman ibn Mughira na Hamad bin Zaid na Hamad bin Waqid kutoka kwa Thabit kutoka kwa Ibn Abi Layla kutokana na kauli yake, humo hakutajwa Mtume صلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ wala Suhaib.’”

Kisha akataja Nawawi huko kwamba, kutotajwa huko matabaka ya wapokezi na uungaji ni nyongeza ya ukweli, nalo ni jambo yeye kukubaliwa!! Na hili ni kosa linalotokana na Nawawi, hafuatwi katika hilo, kwani huu ni mlango ulio kinyume, wenyе kukataliwa hususani na Hamad, ana maneno mengi katika mlango huo.

Na Dhahbi amepokea hadithi katika kitabu *Miizan*, Juz. 1, uk. 593, katika wasifu wa Hamad bin Salama kwa anwani kwamba ni katika Hadithi zake zisizokubalika, na hakika Dhahbi amemfuata katika hilo Ibn Uday katika kitabu Kaamil, Juz. 2, uk. 676, ambapo amesema Ibn Uday huko: “Na Abu Abdillah bin Thalji ni muongo na alikuwa akibuni hadithi na kuziingiza ndani ya vitabu vya watu wa hadithi; hadithi za ukafiri, basi hadithi hizi ni mionganoni mwa zile alizozichomeka...” Kisha akataja hadithi ya kwanza kati ya hizo ni hadithi ya Hamad ambayo ipo katika *Sahih Muslim*! Na hakika katika hilo kuna mazingatio kwa yule mwenye kutega masikio na yeye ni shahidi.

Na amesema Ibn Uday kabla ya hayo: “Abdul-Rahman bin Mahdi amesema: Alikuwa Hamad bin Salama hajulikani kwa hadithi hizi mpaka alipotoka kwenda Abadan, aliporudi akaja akiwa anamezipokea....” Na baada ya yote hayo tunasema kwamba hadithi ni yenyе kukataliwa na ni batili yenyе dosari na ila! Na kauli ya Ibn Qayyim: “Wamepokea maimamu kutoka kwa Hamad na wakaipokea hiyo kutoka kwa Nabii wao kwa kuikubali na kuisadikisha” ni insha isiyo na maana, nayo ni mazigazi ambayo mwenye kiu hudhani ni maji!

### **Hadithi ya 5: Kisha Ibn Qayyim Jawziyya amesema:**

“Na ama hadithi ya Abdillah bin Masuud, Twabarani amesema.... Kutoka kwa Mtume ﷺ amesema: Mwenyezi Mungu atawaku-

sanya watu wa mwanzo na wa mwisho kwa ahadi ya kisimamo cha Siku maalum, ni kisimamo cha miaka 40, macho yao yatakuwa yakikodolea mbinguni wakiangalia usafi wa anga .....” Kisha akata 4 na kwayo zipo sentensi zenye kutia kinyaa mno: “Na anateremka Mwenyezi Mungu katika kivuli cha mawingu kutoka kwenye Arshi mpaka kwenye kiti cha enzi...”

Na ndani yake: “Na itakapozimika – nuru – atasimama na Mola Mlezi yupo mbele yao mpaka apite kwenye moto, na itabakia athari yake kama vile wembamba wa makali ya upanga.....” Haya yanashabihiana na maneno ya Talmudi! Na wao hawaoni haya na aibu kueleza mfano wa maneno haya, hivyo wanayaita kuwa ni hadithi na wanayanasibisha na kuyahusisha na Mtume ﷺ na wanayatumia kuthhibitisha itikadi zao!! Na mwisho wake kuna: “Kaab bin Akhbar akasema: Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko mikononi mwake, hakika Jahannam siku hiyo itatoa sauti ya mvumo.....”

Bila shaka hapa unajua kwamba maneno haya wanayodai kuwa ni Hadithi za Mtume, ni fikara za Kaab bin Akhbar ambazo msingi wake ni Talmudi, ni fikra alizokuwa akizisambaza baina ya Waislamu na akiwasimulia. Bwana wetu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ni mwenye kuepukana na upotofu huu!!

Kisha Ibn Qayyim Jawziyya baada ya hayo akasema:

“Hadithi hii kubwa ni hasan wameipokea waandishi katika sunna kama vile Abdullah bin Ahmad, Twabarani na Daru Qutni katika kitabu cha kuonekana kwa Mwenyezi Mungu. Ameipokea kutoka kwa Swaid: Ametuhadithia Muhammad bin Abi Abdul-Rahman Mughaari mfurutu ada, amesema: Ametuhadithia baba yangu: Ametuhadithia Warqau bin Umar: Ametusimulia Abu Twibat kutoka kwa Karz bin Wabrat, kutoka kwa Nuaym: Ametuhadithia Daalaani: Ameisimulia Minhal ibn Amru kutoka kwa Abi Ubaida, na

ameipokea kutoka katika njia ya Zaid bin Abi Anisat kutoka kwa Minhal ibn Amru, kutoka kwa Abi Ubayda, na ameipokea kutoka katika njia ya Ahmad bin Abi Twaybat, kutoka kwa Karz bin Wabrat, kutoka kwa Nuaym bin Abi Hind, kutoka kwa Abi Ubayda.”

**Nasema:** Hadithi hii ni ya kubuniwa, ya kuchukiza na ni bati, na ndani yake ina fikra nyingi potofu. Hulidiriki hilo kila mwenye kuisoma na akazingatia na kuchunguza kwa undani. Je, inafaa kuchukua kauli zilizopachikwa na zichukizazo ili kuthibitisha suala la upinzani lenye kukinzana na fikra iliyokuja ndani ya Qur’ani?

Hakika nimeandika hadithi hii na nimezungumzia katika mstari wa pambizo wa kitabu *al-Uluwu cha Dhahbi*,<sup>12</sup> na tumbainisha hilo kwamba hakika Abu Ubayda ibn Abdillah bin Masuud, riwaya yake kutoka kwa baba yake ni yenye kukatika, na hakika kitabu *Minhal mwandishi* wake ni mtu wa mabalaa makubwa:

Alikuwa Yahya bin Muin akichomeka katika hadithi zake. Na amesema Mughiira bin Maqsam: “Hakika ushahidi wa *Minhal* juu ya dirhamu mbili haufai. Na Aamash alikuwa akikataza kupokea riwaya kutoka kwa *Minhal*, na hakika Yahya Qatwan alimpuuza na Shuuba alimwacha, na Uqayli amemtaja katika orodha ya wapokezi dhaifu, katika kitabu *ad-Dhuafai*, Juz. 4, uk. 236/1830. Na mengi zaidi ya hayo, basi haturefushi hapa marudio yake.

Na hadithi hii ameipokea Twabarani katika *Mujamul-Kabir*, Juz. 9, uk. 417/9763, na Hakim, Juz. 4, uk. 592, na ameikataa hiyo Dhahabi katika mstari wa pambizo wa kitabu *Mustadrak*. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amani.

**Hadithi ya 6:** Ibn Qayyim Jawziyya baada ya hayo amesema:

<sup>12</sup> Mstari wa pambizo nambari 347 katika kuitolea maelezo hadithi nambari 108, na katika kuitolea maelezo hadithi 149, na katika kuitolea maelezo hadithi 188 na 189.

“Na ama hadithi ya Ali bin Abu Talib, Yaaqub bin Sufiyan amesema: Ametuhadithia Muhammad bin Muswaffa: Ametusimulia Swaid bin Abdul-Aziz: Ametuhadithia Amru bin Khalid, kutoka kwa Zaid bin Ali, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa babu yake Ali bin Abu Talib, kwamba Mtume ﷺ amesema: ‘Watu wa peponi humzuru Mola Mlezi aliyetukuka kila siku ya Ijumaa, na akataja watakayopewa, akasema: Kisha Mwenyezi Mungu atasema: ‘Ondoeni hijabu (sita-ra)’ itaondoka sitara kisha atajitokeza kwao kutohana na uso wake kana kwamba wao hawajawahi kuona neema kabla ya hapo, nayo ndio maneno ya Mwenyezi Mungu: ‘Na kwetu sisi ziada.’”

**Nasema:** Hadithi hiyo ni batili iliyopachikwa, na ufuatao ni ubainifu wake:

- i. Ama kuhusu Suwaydu bin Abdil-Aziz, Ahmad bin Hanbali amesema: “Hadithi yake imeachwa.” Ibn Muiin amesema: “Sio chochote.” Ibn Saad amesema: “Alikuwa anapokea hadithi zisizofaa.” Bukhari amesema: “Hadithi yake ni ya kuchunguzwa, wala haitegemewi, na hakika wamemsifu kwamba yeze ni mwenye hadithi zisizofaa na zinazochukiza na kwamba yeze ni mwangi wa kukosea.” Angalia *Tahdhiibul-Kamaal*, Juz. 12, uk. 258, na *Tahdhiibul-Tahdhiib*, Juz. 4, uk. 242. Na imepatikana katika wasifu wa mtu huyu kwamba alihamia Homsi (Emesa) basi akaishi huko na hadithi ya Homsi (Emesa) ina maneno mengi ndani yake, na Homsi (Emesa) ni mji mkuu wa Kaab bin Akhbar.
- ii. Na Sheikh wake Amru bin Khalid, yeze ni muongo mno na mtungaji wa hadithi, kama linavyolikuta hilo katika wasifu wake katika *Tahdhiibul-Kamaal*, Juz. 21, uk. 603, na vitabu vinginevyo vya kujua kasoro na mapungufu ya wapokezi, na maneno yao kwake ni yenye kukataliwa sio sahihi, yale

ya kwamba yeze ni mpokezi wa vitabu vya Imam Zayd au *Musnad* yake.

- iii. Na mpokezi kutoka kwa Suwaydu bin Abdil-Aziz, naye ni Muhammad bin Muswaffa naye ni mtu wa Homsi (Emesa) pia alikuwa akichakachua hadithi na kuzisawazisha atakavyo, Swaleh bin Muhammad Baghdadi amesema: “Alikuwa mchakachuaji, na ninataraji atakuwa mkweli, na hakika amehadithia hadithi zisizokubalika.” Na Abu Hatam amemwelezea kwamba yeze ni mkweli mno, na Nasaa'i akasema: “Ni mtu mwema.” Hafidh katika kitabu chake *Taqriib* amesema: “Ni mkweli ana mawazo na mchakachuaji.” Na Aqili amemtaja katika kitabu chake *Dhuafau*, angalia katika kitabu *Tahdhiibul-Kamaal*, Juz. 26, uk. 469, na kitabu *Tahdhiibul-Tahdhiib*, Juz. 9, uk. 406.

Basi kiwango hiki chatosha katika kubainisha uzushi wa hadithi, na kinatosha pia katika kubainisha uwongo mwangi wa Ibn Qayyim Jawziyya na jeshi lake lenye kukimbia lenye kushindwa, na yule anayefanana naye katika uthibitishaji wa tawaturi wa hadithi za kumuona Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kuombwa msaada!

### **Hadithi ya 7: Kisha Ibn Qayyim Jawziyya akasema:**

“Na ama hadithi ya Musa iliyopo katika *Sahih* mbili iliyopokewa kutoka kwake, imepokewa kutoka kwa Mtume ﷺ kwamba amesema: “Pepo mbili zinazotokana na fedha nimewapatia wao na vilivyomo ndani yake, na pepo mbili kutoptaka na dhahabu nimepatia wao na vilivyomo ndani yake, na hakuna baina ya watu na kumwangalia Mola Wao Mlezi ila vazi la kiburi lililopo juu ya Uso Wake katika pepo ya kudumu.”

**Nasema:** Hadithi hii ameipokea Twayalisi katika *Musnad* yake uk. 72, Hadithi namba 529, kwa lafudhi “Wamtembelee Mola Wao Mlezi katika pepo ya kudumu” na sio kwa lafudhi: “Kumwangalia Mola Wao Mlezi” nayo ni njia ya Abu Qudaama Harith Ibn Abiid, nao ni uchegemezaji uliyotajwa katika *Sahih Muslim*, na hili linatia ukakasi kutolea kauli hiyo dalili, kwani katika hadithi hiyo hakuna dalili inayothibitisha kuonekana bali inazuia kuonekana, nayo ni hadithi yenyewe kukataliwa kwetu na ufuataao ni ubainifu wake:

- i. Abu Bakri bin Abu Musa Ash'ari ni Naswibii khabithi, naye sio mkweli kwetu! Ibn Saad katika kitabu chake *Twa-baqaat*, Juz. 6, uk. 269, amesema: Alikuwa mchache wa hadithi na mtu mdhaifu.” Na imekuja katika Wasifu wake katika kitabu *Tahdhibul-Kamaal*, Juz. 33, uk. 145: “Ajuuri amesema: Nilimwambia baba wa Daud: Abu Bakri bin Abi Musa alisikia kutoka kwa baba yake? Akasema: Naona alisikia, na Abu Bakri anaridhiwa zaidi kwao kuliko Abu Burda bin Abi Musa, yeye alikuwa akienda na madhehebu ya watu wa Sham, alimjia Abu Dhaadiya muuaji wa Ammar basi akamkalisha pembezoni mwake na akasema: Karibu ewe ndugu yangu.”

Na mwingine akaamrisha, naye ni Abdullah bin Ahmad amesema katika kitabu *Ilal*: Nikasema kumwambia baba yangu je, Abu Bakri bin Abi Musa amemsikia baba yake? Akasema: Hapana.

Na kaka wa Abu Bakri huyu ye ye ni Abu Burda ibn Abi Musa Al-Ash'ari ameipokea kutoka kwa Abdullah bin Amru bin Aswi na Abdullah bin Salama Myahudi, na hawa ni wanukuu wa hadithi za Kiyahudi basi huenda ye ye amesikia hadithi hii kutoka kwa watu hawa, na ameipokea kutoka kwake kaka yake, kisha jambo likageuz-

wa na hatimaye kuwa hadithi ambayo haina mlolongo wa wapokezi, na mfano wa hilo umepatikana na kutokea kama ilivyobainika katika utangulizi wa kitabu *al-Uluwu*.

**Nasema:** Aliishi baada ya baba yake miaka 56 na inamuia viguu yeye kuwa alimsikia baba yake, hata kama hadithi yake kutoka kwake ipo katika *Sahih Mbili*, na Ibn Jawzi ameieleza hadithi hii katika kitabu *Daf'u Shubha Tashbihih*, uk. 253, Hadithi nambari 44.

- ii. Na zipo hadithi zinazoipinga hiyo: Hafidh katika kitabu *Fat'ul-Baari*, Juz. 13, uk. 434, amesema: Na inapingana na hadithi ya Abu Huraira: Tulisema ewe Mtume tusimulie pepo na majengo yake yalivyo? Akasema: “Ni matofali ya dhahabu na matofali ya fedha...” hadithi ameieleza Ahmad na Tirmidhi na akakubali usahihi wake Ibn Haban, na ina ushahidi kutoka kwa Ibn Umar ameueleza Twabarani na sanad yake ni nzuri, na nydingine kutoka kwa Abu Said ameieleza Bazar..., na ukusanyaji kati ya hizo mbili ni wenyne kukalifisha.
- iii. Kisha hadithi hii haina uthibitisho wowote unaothibitisha hakika wao watamwangalia Mwenyezi Mungu, bali yaonesha kwamba wao hawatamwangalia Yeye! Kwa sababu juu ya Uso Wake kuna shuka la kiburi!! Na shuka la kiburi haliondoki mbele ya waja Wake!!

Kisha ufikiriaji huu kwa Mwenyezi Mungu (a.j) kwamba Yeye ana sura ya kiumbe, juu ya Uso Wake kuna shuka na Yeye yuko ndani ya pepo ya kudumu. Na hakika imekuja katika andiko la hadithi hii “na hakuna baina ya watu na kumwangalia Mola Wao Mlezi ila vazi la kiburi lililopo juu ya Uso Wake katika pepo ya kudumu”!!

Sifa hizi zimewafanya watu wa elimu waitilie shaka hadithi hii kama ilivyo katika kitabu *Fat'hul-Baari*, Juz. 13, uk. 433. Hafidh

amesema huko: “Akasema: - Khatwani:- ‘Hakika umekuja utajo wa pazia (hijabu) katika hadithi chungu nzima sahihi na Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameepukana na yote yanayomstiri, kwani sitara huzingira kiwango cha hisia, lakini makusudio ya sitara yake ni kwamba ameyazuia macho ya viumbe wake...’”

Hafidh amesema: “Na Nawawi amesema: ‘Asili ya hijabu ni kuzuia kuona, na hijabu kilugha ni sitara, na hakika inahusiana na mili, na Mwenyezi Mungu ametakasika hana mwili, basi akajulikana kwamba makusudio ni kizuizi chenye kuzuia kumuona yeye...’” Na Hafidh amesema: “Ayyadh amesema: ‘Waarabu walikuwa wakitumia istiara sana...na yule asiyefahamu hilo huhangaika, basi yule ambaye ameyapitisha maneno juu ya dhahiri yake hali hiyo imempeleka katika kumfanya Mwenyezi Mungu ana mwili, na yule ambaye haijakuwa wazi kwake na akajua hakika Mwenyezi Mungu ameepukana na lile ambalo ni muktadha wa dhahiri ya Hadithi hiyo, ima aikanushe nukuu yake na ima aitolee maana nyingine...’”

Na Hafidh amesema: “Karumani amesema: ‘Hadithi hii ni miongoni mwa zile za mafumbo, ima itelekezwe au itafutiwe maana na maelezo kwamba mradi wake ni uso wa dhati, na shuka ni sifa kati ya sifa za dhati zinazolazimu kuepukana na yale yote yanayofanana na viumbe. Kisha akatilia shaka dhahiri yake kwamba muktadha wake unazuia kuonekana kwa Mwenyezi Mungu, kisha akajibu kuwa kinachofahamika ni kwamba inaonesha ukaribu wa kuangalia...’”

Kisha Hafidh akasema: “Na matokeo ni kwamba shuka ya kiburi ndiyo kizuizi cha kuonekana kama kwamba katika maneno kuna kitu kilichofutwa...”

**Nasema:** Hafidh hathibitishi suala la watu kumuona Mola Wao Mlezi, na Mwenyezi Mungu ameepukana na sifa au hali ya kuingia kwenye pepo ya kudumu, na hadithi hii ni ngeni kwa upande wa

sanad, ni batili kwa upande wa matini na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kuombwa msaada.

**Hadithi ya 8:** Ibn Qayyim Jawziyya amesema:

“Imam Ahmad amesema: Ametuhadithia Hasan bin Musa na Uthman wamesema: Amesimulia Hamad bin Salama, kutoka kwa Ali bin Zayd, kutoka kwa Ammara, kutoka kwa Abi Burda, kutoka kwa Abi Musa, amesema: Mtume ﷺ alisema: “Mwenyezi Mungu atakusanya nyumati katika muinuko mmoja Siku ya Kiyama na pindi atakapoanza Mwenyezi Mungu kutenganisha kati ya viumbe Wake, kila kaumu ataitolea mfano wa kile walichokuwa wakikiabudu basi watakifuata hao mpaka kiwaingize motoni. Kisha atatujia Mola Wetu Mlezi (s.w.t) na sisi tukiwa sehemu ya juu, basi atatuuliza: Nyinyi ni nani? Tutamjibu sisi ni Waislamu, atasema: Mnangojea kitu gani? Tutasema: Tunamngojea Mola Wetu Mlezi; atasema: Je, mtamjua ikiwa mtamuona? Tutasema: Ndiyo, hakuna kikwazo kwake, basi atajitokeza kwetu hali akicheka.....”

**Nasema:** Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameepukana na ametakasika na upotofu huu wa Kiyahudi!! Hadithi hii haina mashiko kuhusiana na sanad yake, na matini yake ni batili kama utakavyoona!!

Na ubainifu wa hilo ni kwamba katika sanad yake yupo Hamad bin Salama na yametangulia maelezo kumhusu yeye, na kwamba habari yake haikubaliwi katika hadithi za sifa, na Sheikh wake ni Ali bin Zayd, watafiti wa wapokezi wanamuona ni dhaifu (na sisi tunakwenda kinyume nao). Na Sheikh wake ni Ammara ni dhaifu mno kama ilivyokuja katika kitabu *Lisaanul-Miizan*, Juz. 4, uk. 279. Na Hafidh Abu Zar’aa Muiraq amekufa mwaka 826, katika kitabu *Dhairul-Kaashif* hakumtaja.

Na hakika tumetaja katika maneno ya hadithi ambayo kabla yetu kwamba Abu Burda alipata elimu kutoka kwa Abdullah bin Salam

Myahudi!!! Na matini ya hadithi ni yenyé kuchukiza mno, nayo ni batili kwetu. Ibn Qayyim baada ya hadithi hii amesema:

“Ametaja Daar Qutni kuhusiana na hadithi ya Abaan bin Abi Ayyash kutoka kwa Abu Tamiima Hujaymi kutoka kwa Abi Musa kutoka kwa Mtume ﷺ amesema: “Mwenyezi Mungu atamtuma mnadi (muitaji) Siku ya Kiyama kwa sauti, wataisikia wa mwanzo wao na wa mwisho wao. Hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) amekuahidi wema na ziada, wema ni pepo na ziada ni kuangalia uso wa Mwenyezi Mungu (s.w.t)].

**Nasema:** Huu ni uongo wa dhahiri kabisa!! Abaan ibn Abi Ayyash ni mwenye kuachwa na kupuuzwa, hadithi anayoipokea inarudishwa na kukataliwa kama unavyokuta katika kitabu *Tahdhiibul-Kamaal*, Juz. 2, uk. 22. Na kauli yake “Basi wema...” imechakachuliwa kama ilivyo wazi kwa mwenye kuzingatia fuo la maneno.

### **Hadithi ya 9: Ibn Qayyim Jawziyya amesema:**

“Na ama hadithi ya Uday bin Hatam iliyopo ndani ya *Sahih Bukhari* amesema: “Pindi mimi nilipokuwa kwa Mtume ﷺ punde akajiwaa na mwanaume mmoja akamshitakia ugumu wa maisha....” Ameitaja hadithi hii, na sehemu anayoikusidia katika hadithi hii inasema:

“Na Mwenyezi Mungu atakutana na mmoja wenu siku atakayokutana naye, ilihali kukiwa hakuna kizuizi kati yake na yeye, wala mkalimani atakayemtarjumia, basi atasema: Je, sijakutumia wewe mjumbe na akufikishia?”

**Nasema:** Hakuna dalili katika hadithi hii juu ya kuonekena kwa Mwenyezi Mungu wala lafudhi ya kumuona Mwenyezi Mungu! Na hakika Muslim ameipokea hadithi hii na mwingineo kwa lafudhi: “Hakuna ye yeyote miiongoni mwenu ila Mwenyezi Mungu atazung-

umza naye ilihali hakuna kati Yake na yeye mkalimani...” hakuna utajo wa kumuona Mwenyezi Mungu wala linaloashiria juu ya hilo, na lingine kwamba hadithi hizi kwa maana hutokana na tabia na nyendo za wapokezi, hivyo hazina hoja yoyote.

Na yawapasa watu kujua kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) sio mtu hadi akutane na watu Siku ya Kiyama na wazungumze Naye na kukaa Naye, Mwenyezi Mungu ameepukana na hilo mbali zaidi. Na hadithi hii ni batili kwetu haisihi kwani inapingana na Qur’ani kuhusiana na andiko la Mwenyezi Mungu kuwa hasemi nao makafiri na wanafiki. Na hadithi iliyomo katika *Bukhari* ni yenyе kutaja kwamba hakika mja ambaye Mwenyezi Mungu atamsemesha hataona ila moto, na katika lafudhi lingine ni hataona ila Jahannam, na nimebainisha hilo katika mstari wa pambizo wa kitabu *al-Ibanah*, nimesema huko: Lafudhi hii imepokewa na Bukhari, 7443 na 7512.

Nayo ni hadithi yenyе kurudishwa na kukataliwa, na hadithi zake katika Sahihi Mbili zinajulisha kwamba maneno haya yatatokea kwa watu wa Jahannam kabla hawajaingia! Na watu hawa ndiyo wale ambao Mwenyezi Mungu amewazungumzia kwa kusema: “Wala Mwenyezi Mungu hatasema nao siku ya Kiyama” (2:174), na lafudhi ya hadithi katika *Bukhari* 1413 inasema: “Kisha mmoja wenu atasimama mbele ya Mwenyezi Mungu hakuna pazia kati yake wala mkalimani anayewatarjumia kisha atamwambia je, sijakupa mali? Basi atasema: Hakuna shaka umenipa, kisha atasema: Je, sijakutumia mjumbe basi atasema: Bila shaka ndivyo hivyo, hapo ataangalia kuliani kwake haoni ila moto kisha ataangalia kushotoni mwake haoni ila moto, basi auogope mmoja wenu moto lau kwa kutoa kokwa ya tende.” Na katika lafudhi nyingine katika *Bukhari* 3595: “Na atakutana na Mwenyezi Mungu mmoja wenu siku atakayokutana naye na hakuna kati yenu na Yeye mkalimani anayemtarjumia, na hapo atamwambia yeye je, sijakutumia wewe mjumbe na kukufikishia?

Atasema: Hakuna shaka ndivyo hivyo, atasema: Sijakupa mali na lililo bora zaidi juu yako, atasema: Bila shala ndivyo hivyo, basi atangalia kushotoni kwake wala haoni ila Jahannam.” Na kwa hivyo imebatilika dalili ya hadithi hii, pamoja na kuwa hadithi ni yenye kugongana katika lafudhi yake.

### **Hadithi ya 10: Ibn Qayyim Jawziyya amesema:**

“Na ama hadithi ya Anas bin Malik iliyopo katika *Sahih Mbili* kuto-kana na hadithi ya Saad bin Abi Uruwat kutoka kwa Qitada kutoka kwa Anas bin Malik, ni kwamba Mtume ﷺ amesema: “Mwenyezi Mungu atawakusanya watu Siku ya Kiyama basi watalijali hilo...watasema: Lau tungeliomba uombezi kwa Mola Mlezi hata atupe raha....” na akataja hadithi ndefu ya uombezi.

Na mahala pa ushahidi ni kauli yake: “Basi nitamuomba idhini Mola Wangu Mlezi na atanipa idhini, basi pindi mimi nitakapomuona nitaporomoka chini kumsujudia.”

Na akataja Ibn Qayyim hadithi nyingine mbele ya Ibn Khuzaima na ndani yake kuna: “Basi nitasema mimi ni mwenye kustahiki, basi nitakwenda zangu mpaka nitakapotaka kufungua mlango wa peponi na atanifungulia na nitaingia ilihali Mola Wangu Mlezi yuko juu ya kiti Chake cha enzi, basi hapo nitaporomoka chini na nitamsujudia.”

Hadithi hii inathibitisha kwamba Mwenyezi Mungu atakuwa peponi juu ya Arshi Yake! Na Mwenyezi Mungu ameepukana na hilo mbali kabisa! Na lenye kuchukiza zaidi ni lile lililopo katika *Sahih Bukhari* mstari wa pambizo, Juz. 13, uk. 422/ 7440, na akaunga Ahmad katika Juz. 3, uk. 244: Basi nitamuomba idhini ya kuingia kwake, atanipa idhini ya kuingia kwake, basi nitakapomuona nitaporomoka chini na kusujudu.”

Na Dhahabi amehukumu juu ya hadithi hii katika kitabu *al-Ulu-wu*, uk. 176 mstari wa pambizo 254 kwamba: “Hadithi si ya kawaida, ni yenye kuchukiza, potofu na batili!”

Na hakika nimemtaja huko yule ambaye ameipokea hadithi hii katika *Sahih Mbili* na vitabu vingine mionganoni mwa watu wakweli, na haikuja ibara ya kuonekana kwa Mwenyezi Mungu na nyumba, jambo ambalo linaonesha kuwa hadithi hii ni yenye mgongano na ni yenye kukataliwa! Na baya zaidi ya hilo ni yale aliyoyaeleza Dhahabi uk. 179 kuhusiana na hadithi ya Assal, ambayo kwa rai ya Dhahbi ina sanad yenye nguvu, kaipokea kwa tamko: “Basi nita-kwenda kwenye mlango wa pepo, atanifungulia na nitaingia kwa Mola Wangu Mlezi (s.w.t) Naye akiwa ameketi juu ya kiti Chake au kitandani Kwake, basi nitaporomoka chini kumsujudia.”

Na huu ni upotoshaji uliopindukia! Fikira hizi zinatoka wapi? Na katika matini ya hadithi ya bwana wetu Anas kuna mambo ambayo wanazuoni wanaona ni mushkeli kama alivyotaja hilo Hafidh katika kitabu *al-Fat’hu* katika ufanuzi wake wa kitabu *Riqaq*. Hakika ndani yake yameelezwa wazi wazi makosa ya Mitume ﷺ, na kwamba hatoingia motoni ila yule aliyefungwa na Qur’ani, yaani yule ambaye Qur’ani imetaja kuwa atadumu milele motoni kama vile muuaji wa nafsi, nayo inakwenda kinyume na hadithi nyingine ambazo zinataja kuwa hata wasiokuwa hao wataingia motoni. Na ndani yake kuna hadithi ya kwanza ya bwana wetu Anas kuhusu uombezi wa kuomba kupata raha kutokana na matatizo ya kisimamo, na mwishowe ndipo anataja uombezi kuhusiana na kutolewa motoni, na Hafidh katika kitabu *al-Fat’hu*, Juz. 11, uk. 438, ameelia-za kwamba hakika huu ni mushkeli wenye nguvu.

Na amenukuu kabla ya hivyo kwa mistari kadhaa kutoka kwa Daud amesema: “Kama kwamba mpokeaji wa hadithi hii amebe-basha kitu ambacho si katika asili yake” na mengineyo mionganoni

mwa mambo ambayo huenda sisi tukayazungumzia katika Risala maalumu. Na ufupisho wa maneno ni kwamba hakika maudhui ya uombezi yamethibiti katika Qur'an na katika hadithi nyingine, lakin i hadithi hii ndefu ya Anas kuhusiana na uombezi iko kinyume na haikubaliki.

Ibn Qayyim Jawziyya amesema:

“Na suala la Mtume ﷺ kumuona Mola Wake Mlezi katika sehemu hii limethibiti uthibiti wa yakini kwa watu wa elimu ya hadithi na sunna.” Hakika Hafidh Ibn Arabi Muafari Malik katika kitabu *Aaridhatul-Ahwadhi Sharhul-Tirmidhi*, Juz. 10, uk. 23, amesema: Maana yake ni kwamba watu hawamuoni Mwenyezi Mungu katika ardhi ya ufufuo kwa mujibu wa maneno ya wanazuoni, na hakika sehenu ya kumuona ni peponi..... kwa mujibu wa kongamano la wanazuoni.....!!

Na huko Ibn Qayyim Jawziyya amesema: “Na katika hadithi ya Abu Huraira: Mimi ni wa kwanza ambaye ardhi itapasuka kwa ajili yake (kufufuliwa) Siku ya Kiyama wala sio kujifaharisha. Na mimi ni mtoto wa Adam... Nitachukua komeo na kugonga mlango wa peponi basi ataniruhusu na atanipokea kwa uso wa Jabbar (utukufu ni wake) basi nitaporomoka chini na nitamsujudia.”

Jibu: Sijaipata hadithi ya Abu Huraira! Na hakika nimeipata hadithi ya Anas ibn Malik katika kitabu *Taadhiim Qadrul-Swalaat*, ni hadithi ya 269 na sanad imeoza na ina hitilafu. Nayo ni batili kwa kila mwenye akili timamu kwani Mwenyezi Mungu ametukuka na kuepukana na kuwapokea watu na kuingia peponi, hizo ni katika sifa za baadhi ya viumbe Wake na sifa zenyenye kuzuka za viumbe.

Kisha Ibn Qayyim ametaja hadithi katika kitabu *Al-Ruuyat* chenye kunasibishwa na Daar Qutni katika njia hii: “Umar Abaha kutoka kwa Said bin Abi Urwat kutoka kwa Qatadah kutoka kwa

Anas kutoka kwa Mtume ﷺ katika maneno ya Mwenyezi Mungu (s.w.t): ‘Wale waliofanya wema watapata wema na ziada’ akasema: Uangaliaji wa uso wa Mwenyezi Mungu.”

**Nasema:** Huo ni upotofu batili! umetajwa katika kitabu *Al-Ruyat* chenye kunasibiswaa na Daar Qutni, katika kutaja hadithi kuto ka kwa Anas bin Malik katika tafsiri ya Aya hii, na katika sanad yake yumo Abaha ambaye ni mwenye kuachwa kwa Hafidh Ibn Habban, na *Bukhari* amesema: Ni hadithi chukizo<sup>13</sup> na hakuna yeoyote aliyemzingatia kuwa ni mkweli.

**Hadithi ya 11:** Kisha akataja Ibn Qayyim baada ya hayo hadithi ya Anas bin Malik ambayo haikutajwa wapokezi wake, na mwanzo wake ni:

“Alinijia Jibrail na kiganjani kwake kipo kitu kama vile kioo cheupe alichokibeba, na ndani yake kama vile nukta nyeusi, nikasema: Ewe Jibrail ni kitu gani kipo mkononi kwako? Akasema: Hii ni Ijumaa.....” Nayo ni hadithi ndefu na mahala pa ushahidi ambapo panaonesha kuonekana kwa Mola Muumba kwa mujibu wa Ibn Qayyim Jawziyya na wafuasi wake wenye imani ya kuwa Mwenyezi Mungu ana mwili ni:

“Hakika Mola Wako Mlezi amefanya makazi yake peponi kwenye bonde ambalo pananukia mahala hapo zaidi ya miski nyeupe, na itakapofika Siku ya Kiyama atateremka (s.w.t) kutoka juu ya kiti Chake cha enzi..... basi atajitokeza kwao Mola wao Mlezi hadi waangalie Uso Wake... kisha anapanda juu ya kiti Chake cha enzi na watapanda wakweli na mashahidi pamoja naye.....” Mwenyezi Mungu ametukuka na hilo na hayuko hivyo kabisa!!

<sup>13</sup> Angalia *Tafsirul-Kabiir*, Juz. 6 uk. 143, *Lisaanul-Miizan*, Juz. 4 uk. 301, Al-Majruuhiina cha Ibn Habaan, *Al-Jarhu wa Taadiil* Juz.6 uk. 111, *Dhuafaal-Aqil*, Juz.3 uk. 166 na *Al-Kaamil*.

Na jibu la hilo: Hakika hadithi hii imepachikwa na ni batili! Na ina harufu ya Kiyahudi! Na nimezungumza juu ya ncha zake zote na riwaya zake katika utoaji na ukosoaji wa kitabu *al-Uluwu*, uk. 159-171 cha Dhahabi, hivyo sintarudia hapa.

**Hadithi ya 12:** Kisha Ibn Qayyim Jawziyya baada ya kutaja hadithi ya “Kioo cheupe na kidoti cheusi” akasema:

“Na ama hadithi ya Buraydah bin Haswiib: Amesema imam wa maimamu Muhammad bin Is’haaq ibn Khuzayma: Ametuhadithia Abu Khalid Abdul-Aziz bin Abaan Quraishi: Ametusimulia Bashir bin Muhajir, kutoka kwa Abdullah bin Burayda kutoka kwa baba yake kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amesema: Hakuna ye yeyote mionganoni mwenu ila atakuwa na Mwenyezi Mungu Kwake Siku ya Kiyama na baina yake na Yeye hakutakuwa na sitara wala mkalimani.”

Na jibu juu ya hilo ni kwamba hakika hadithi hii imewekwa na ni ya uongo kwa ubainifu ufuatao:

Ama Abu Khalid Abdul-Aziz bin Abaan Quraishi, Yahya bin Muin amesema kuhusu yeye: “Ni mtu muongo khabiithi anazusha hadithi.” Na Ahmad bin Hanbali na wengineo wamemwacha. Angalia *Tahdhiibul-Tahdhiib*, Juz. 1, uk. 294. Na Sheikh wake ni Bashir bin Muhajir, Ahmad amesema: “Hadithi zake hazikubaliki.” Abu Hatam amesema: “Huandikwa hadithi yake wala haitumiwi kama hoja.” Angalia wasifu wake katika kitabu *Tahdhiibul-Tahdhiib*, Juz. 1, uk. 411.

Na unatosha ubainifu huu juu ya uzushi wa hadithi hii.

**Hadithi ya 13:** Ibn Zafil ambaye ni maarufu kwa jina la Ibn Qayyim Jawziyya amesema baada ya hayo:

“Na ama hadithi ya Abu Raziin Uqayliy ameipokea Imam Ahmad katika hadithi ya Shuubat na Hamad bin Salama kutoka kwa Antwai bin Yaali kutoka kwa Wakii bin Udsu, kutoka kwa Abi Raziin amesema: Tulisema: Ewe Mtume! je, sisi sote kila mmoja wetu atamuona Mola Wake Mlezi Siku ya Kiyama? Akasema: Ndio. Nicasema: Ni ipi alama hiyo katika viumbe Wake? Akasema: je, sio kila mmoja wenu anauangalia mwezi usiku wa katikati ya mwezi? Tukasema: Ndio. Akasema: Mwenyezi Mungu ni Mkuu na Mtukufu zaidi.”

Na jibu juu ya hilo ni kwamba hakika sanad ya hadithi hii ni dhaifu, na hadithi imetungwa hakuna shaka, na katika sanad yupo Wakii bin Udu na wala hakukiri ukweli wake ila Ibn Habaan, na hakupokea kutoka kwake ila Yaali bin Atwai, naye hajulikani kama ilivyo katika kitabu *Tahdhibul-Tahdhib*, Juz. 11, uk. 115.

Naye ni mhusika na mwenye hadithi inayosema: “Wapi alikuwa Mola wetu Mlezi? Akasema: Katika *Amaau*, juu yake wala chini yake hakuna hewa.” Na hadithi hii ameipokea Abu Daud 4731 na Ahmad bin Hanbali katika *Musnad*, Juz. 4, uk. 11, na Ibn Abi Aswaim katika kitabu *Sunan*, uk. 200, hadithi nambari 459-460 na wengineo.

Na ni kichekesho kweli kwamba hakika Alban mpizani, ameizingatia hadithi hiyo kuwa ni hasan, licha ya kukiri kwake kwamba Wakii bin Udu ni mwenye kuzua Hadithi, na licha ya kauli ya Dhababi kwamba “hajulikani,” na akailetea nguzo kutoka katika kitabu *Tawhiid* cha Ibn Khuzaima, na katika sanad ya nguzo hiyo wapo wawili ambao hawajulikani!! – Hivyo hadithi ni batili yenyewe kuktaliwa na kurudishwa, wasalam.

### **Hadithi ya 14: Ibn Zafil ambaye ni Ibn Qayyim Jawziyya amesema:**

“Na ama hadithi ya Jabir bin Abdillah amesema Imam Ahmad: Ametuhadithia Ruuhu bin Ubaada kutoka kwa Ibn Juraih, amesema: Amenipa habari Abu Zubair kwamba amemsikia Jabir akiulizwa na Waruud, akasema: Sisi Siku ya Kiyama juu ya kadhaa wa kadhaa... utaitwa umma kwa masanamu yake na vile walivyokuwa wakivivabudu wa kwanza wataanza. Kisha atatujia Mola Wetu Mlezi baada ya hapo basi atauliza: Mnamngojea nani? Watajibu: Tunamngojea Mola Wetu Mlezi. Atasema: Mimi ndiye Mola Wenu Mlezi. Watasema: Mpaka tukuangalie Wewe. Basi atajidhihirisha kwao (s.w.t) atacheke. Akasema: Ataondoka zake na wao watamfuata Yeye.....”

Na ametaja Ibn Qayyim huko kwamba hakika Muslimu ameipokea katika *Sahih* yake. Na ndio vivyo imo katika *Sahihi Muslim*, imeegemezwa juu ya Jabir, na kilichoegemezwa sio hoja, nayo ni hadithi batili yenye kuchukiza yenye kumfananisha bayana Mola Manani na viumbi na kumfanya kuwa ni mwenye mwili! Ni batili yenye kuchukiza kinaga ubaga katika ufananishaji na ufanyaji mwili huo! Amenukuu Jabir kutoka kwa Kaab bin Akhbar, amenukuu kwamba yeze ni mionganini mwa waliopokea kutoka kwake, Dhahbi katika kitabu *Siyaru Aalaamul-Nubala*, Juz. 3, uk. 489, amesema: Hakika Kaab bin Akhbar “Alikuwa anakaa na Masahaba wa Mtume صلی اللہ علیہ وسالہ na akiwahadithia kuhusiana na vitabu vya Kiyahudi.”

Ila Muslim amefuta matini ya tamko alilolitaja Abu Awana katika kitabu *Musnad*, Juz. 1, uk. 139, licha ya kuwa hadithi hiyo imepokewa kwa njia hiyohiyo, nalo ni: “Basi atajidhihirisha kwao ilihali anacheke mpaka kitadhihirika kilimi chake na magego yake.” Tunamuomba msamaha Mwenyezi Mungu! Na tunamuomba Mwenyezi Mungu amani na afya! Na wala sidhani kuwa mtu mwenye akili timamu anaweza kutamka athari hii batili hususan ukizingatia kwamba hadithi yenye ni hadithi ndefu ya Abu Huraira ipo katika *Sahih Mbili* ambayo ukosoaji wake umetangulia hapa na katika vi-

tabu vingine, wala hatuna shaka kwamba haya ni kutokana na yale aliyoypokea kutoka katika hadithi za Kiyahudi, ametukuka Mwenyezi Mungu (s.w.t) mbali na hilo.

Wala hatushughuliki katika kubainisha sanad yake na yale yaliyomo ndani yake, hakika kujishughulisha na hadithi kama hiyo yenyne matini mbaya zilizo wazi kwa ufananisho au kumfanya Mola Muumba ana mwili ni aina ya kuchanganikiwa na uwendawazimu, na hakika nimetaja katika utangulizi wa uhakiki wa kitabu *al-Uluwu* cha Dhahabi, njia za zilizotumika kuingiza hadithi za Kiyahudi katika hadithi za Kiislamu, na yule aliyepokea mionganoni mwa Masahaba kutoka kwa Kaab bin Akhbar na kutoka kwa Abdullah bin Salam, basi na arejee hayo huko kwani ni muhimu mno.

### **Hadithi ya 15: Kisha Ibn Qayyim akasema:**

“Na amesema Ibn Majah katika *Sunan* yake: Ametuhadithia Muhammad bin Abdul-Malik bin Abi Shawaarib: Ametuhadithia Abu Aswim Abadani, kutoka Fadhl bin Isa Raqaashiy, kutoka kwa Muhammad bin Munkadar, kutoka kwa Jabir ibn Abdillah amesema: Mtume ﷺ amesema: “Watu wa peponi watakapokuwa katika neema zao ghafla nuru itajitokeza basi watainua vichwa vyao, punde Mola Mlezi (s.w.t.) atawakaribia juu yao atasema: Amani iwe juu yenu enyi watu wa peponi, nayo ni kauli ya Mwenyezi Mungu (a.j.) ‘Kauli ya amani kutoka kwa Mola Mlezi Mwenye huruma’ hapo hawatakigeukia chochote mionganoni mwa vile vilivromo humo mionganoni mwa neema, maadamu macho yao yanamtazama Yeye, mpaka atakapotoweka na itabakia kwao baraka Yake na nuru Yake.””

Na ametaja njia nyingine ya Harb katika kitabu chake *al-Mas'alah*, na Bayhaqi katika kitabu chake *Al-Ba'ath Wan-Nushuur*,

na kitabu *Ruuyat* na zote hizo zinazunguka kwa Abu Aswim Abadani na Sheikh wake Fadhl Riqaashiy!!

**Nasema:** Hadithi hii ya uzushi na uwongo imepokewa na Ibn Majah Juz. 1, uk. 66 na 184, na hakika nimeitoa hiyo katika mstari wa pambizo katika ukosoaji wa kitabu *al-Uluwu* cha Dhahbi, na katika sanad yake yumo Abu Aswim Abadani, amesema Dhahbi yeye mwenyewe katika kitabu *Al-Miizan*, Juz. 4, uk. 543: “Sio hoja, huja na maajabu mbalimbali.” Na Aqiliy amesema: “Ni mwenye Hadithi zisizokubalika.”

Na ama sheikh wake Fadhl bin Isa Riqaashiy ametajwa katika kitabu *Tahdhiibul-Kamaal*, Juz. 23, uk. 243 – 247, huu ndio ufupisho wake: “Amesema Ibn Muiin: ‘Alikuwa....., na alikuwa ni mtu muovu.’” Nasema: Basi ni vipi kuhusu hadithi yake? Anasema: “Usulizie kuhusu Qadiria huyu khabithi.” Na amesema Abu Zar’at na Abu Hatam: “Ni mwenye Hadithi zisizokubalika.” Ayub Sakhtiyani amesema: “Lau yeye angezaa mtoto kiziwi ingelikuwa ni kheri zaidi kwake.” Na Abu Daud amesema: “Alikuwa mwenye kuangamia.” Na Hamad bin Zayd akasema: “Alikuwa ni mtu khabiithi zaidi katika watu kikauli.”

Na kutokana na hayo utajua jinsi wanavyochukua hadithi za uwongo na uzushi batili na fedheha ili kuthibitisha itikadi zao za Usalafi (Uwahabi) na wakidai hadithi hizi ambazo ziko katika aina hii kuwa ni mutawatiri!!

### **Hadithi ya 16: Kisha Ibn Zafil amesema:**

“Na katika kitabu cha kumuona Mola Manani kuna yale yenyе kuunga mkono habari hii, Daaru Qutni amesema: ‘Ametupa habari Hasan bin Ismail: Ametuhadithia Abul-Hasan Ali bin Abdat: Ametusimulia Yahya bin Said Qatwani, kutoka kwa Abi Dhi’ib kutoka kwa Mu-

hammad bin Al-Munkadar, kutoka kwa Jabir kwamba Mtume ﷺ amesema: "Hakika Mwenyezi Mungu (a.j.) atajidhihirisha kwa watu wote na atajitokeza kwa Abu Bakri pekee."

**Nasema:** Hadithi hii ni ya kubuniwa, Dhahbi katika kitabu chake *al-Miizan*, Juz. 3, uk. 120, katika wasifu wa mmoja wa wapokezi wake naye ni Ali bin Abdat; amesema: "Na hili lathibitisha kwa yakini kwamba yeze ndiye aliyebuni upuuizi huu kwa jina la Qatwani." Na Daaru Qutni amesema huko kumhusu yeze: "Alikuwa ni mwe-nye kuzua hadithi za uwongo." Na ameipokea hadithi hii Khatwiib katika kitabu chake cha historia Juz. 12, uk. 19, na akatoa andiko huko juu ya ubatili wake na amelieleza hilo Jawzi katika kitabu *Maudhuuat*, Juz. 1, uk. 306, na Hafidh Suyutwi katika kitabu *Aal-aaa Mas-nuuat Fii Ahadiith Maudhuuat*, Juz. 1, uk. 288, na Ibn Haban katika kitabu *Al-Majruhiin*, Juz. 2, uk. 115, na Ibn Arraq katika kitabu *Tanzihul-Shariiat Marfuat Alaa Ahadiithil-Mawdhuuat*, Juz. 2, uk. 372, na wengineo.

### **Hadithi ya 17: Kisha Ibn Qayyim Jawziyya akasema:**

"Na ama hadithi ya Abu Amamat: Ibn Wahb amesema: Amenipa habari Yunus bin Yazid, kutoka kwa Atwai Khurasani, kutoka kwa Yahya bin Abi Amru Siybaani, kutoka kwa Amru bin Abdullah Khadhrami, kutoka kwa Abi Amamat, amesema: 'Mtume ﷺ al-ituhutubia siku moja na hotuba yake ilihu zaidi utajo wa Dajjal, ambapo alikuwa akitutahadharisha naye..... basi atasema mimi ni Mola Wenu Mlezi, na hamtamuna Mola Wenu Mlezi mpaka mfe na kwamba yeze ameandikwa kati ya macho yake mawili: Kafiri.....'"

**Nasema:** Ameipokea Ibn Majah, Uk. 4077, na Ibn Abi Aswim katika Sunan, uk. 429, na Ajuriy katika *Shariiat*, uk. 376, na amean-guka kutoka katika sanad ya Ibn Majah Amru bin Abdullah Saybaani

Abu Ajmaai Hadhrami Hamswi, naye ni mtu dhaifu, hakupokea kutoka kwake ila Yahya bin Abi Amru, naye yumo katika kitabu *Diwan Dhuafaa* nambari 3188 cha Dhahbi. Na amesema katika kitabu *al-Mizaan*: “Ni tabiihana ambaye hajulikani.”

Na hadithi ya Dajjali kwetu sisi ina maneno mengi kutoka katika njia zake na riwaya zake mpaka katika *Sahih Mbili*! Na ama lafudhi “Na hamtamuna Mola Wenu kamwe hadi mfe,” hakika imekuja katika *Sahih Muslim*, na mtoaji habari hakutoa habari juu ya hilo. Imekuja katika *Sahih Muslim*, Juz. 4, uk. 2935 baada ya hadithi ya Ibn Umar kuhusiana na Dajjali:

Amesema Ibn Shuaib – yaani Zahri –: Amenipa habari Umar bin Thabit Answaari kwamba baadhi ya Masahaba wa Mtume ﷺ walimweleza kwamba hakika Mtume alisema siku moja wakati akitoa tahadhari kuhusu Dajjali: “Hakika yeye ameandikwa kati ya macho yake mawili: Kafiri. Atasoma hayo yule mwenye kuchukia matendo yake au atayasoma hayo kila muumini.” Na akasema: “Na jueni kwamba hakuna mmoja wetu atakayemuona Mola Wake Mlezi (a.j) mpaka afe.”

**Nasema:** Hatujui ni kwa nini Zahri au Umar bin Thabit alipitiwa na kutomjua huyo Sahaba ambaye amepokea kutoka kwake kwa lafudhi hii, na kwa sababu hii ni dhahiri kuwa hayo ni mionganii mwa yale yaliyochomekwa na Zahri, na hasa ukizingatia kwamba Bukhari amepokea hadithi katika mahala pengi na akaipa kisogo na kukikataa kipande hiki na kukata shauri kwamba ni hadithi iliyo kinyume na hakukitaja kipengele hicho huko!!

Hivyo kauli yenyewe nguvu kwangu ambayo haina mpinzani ni kwamba Hadithi hiyo ni kati ya zile ambazo zimechomekwa na Zahri, kwani yeye ni upenyo wa kuingiza katika hadithi maneno menge yasiyokuwemo katika asili ya Hadithi, kama nilivyolibainisha

hilo mwishoni mwa Juzuu ya tatu ya kitabu *Al-Tanaaqudhaat!* Na huenda ameichukua hiyo kutoka katika hadithi ya Abu Amamat! Na amepokea Ahmad bin Hanbali katika *Musnad* yake hadithi kuhusiana na Dajjali kwa sanadi yenyeye mlolongo wa watu wa Sham! Kutoka kwa Ubdat bin Swamit! Na akaongeza mmoja wa wapokezi wake mwishoni mwake naye sio mwingine bali ni Yazid bin Abdu Rabbah, nyongeza itokayo kwake mwenyewe, Ahmad akasema huko: “Yazid amesema: Jueni hakika Mola Wenu Mlezi (a.j.) sio chongo, na hakika nyinyi hamtamuna Mola Wenu Mlezi mpaka mfe, Zaydi akasema: Mtamuona Mola Wenu Mlezi baada ya kufa.” Na hadithi iliyomo katika *Sunan Abi Daud*, uk. 4320 bila ya nyongeza hii imetoka nje ya kawaida.

**Nasema:** Na Abu Amamat Bahiliy, ni sahaba aliyeishi Emesa (Homsi), napo ni sehemu ya Kaab bin Akhbar, na ikiwa itathibiti lafudhi kutoka kwake basi hakika habari hiyo itakuwa ni kati ya zile zilizopokewa kutoka kwa Kaab bin Akhbar.

### **Hadithi ya 18: Kisha Ibn Qayyim baada ya hayo akasema:**

“Na ama hadithi ya Zaydi bin Thabit, Imam Ahmad amesema: Ametuhadithia Abu Mughiirat amesema: Amesimulia Abu Bakri, amesema: Amehadithia Dhamrat bin Habiib, kutoka kwa Zayd bin Thabit kwamba hakika Mtume ﷺ alifundisha yeze dua na akamwamrisha awazoeze dua hiyo ndugu zake kila siku.”

**Nasema:** Ndani yake kuna ibara: “Ewe Mwenyezi Mungu ninakuomba... ladha ya kuangalia uso wako na shauku ya kukutana nawe.....”<sup>14</sup>

<sup>14</sup> Yatapita pamoja nasi Mungu akipenda hakika sisi tumefanya utafifi katika njia za hadithi hii na tukaikuta hiyo imepokewa kutoka kwa Abdillah bin Mas’ud na Ammar bin Yasir na haiko ndani yake lafudhi hii, na lafudhi hii ni kutokana na ziada ya watu wa Shamu na wa kale ambao pia wao wanaungana na Kaab Akhbar! Basi zinduka kwa hili!

Sanad yake ni dhaifu mno! Na lafudhi: “Ladha ya kuangalia uso wako” inachukiza na haipendezi, na sanad ya hadithi hii hapa yumo Abu Bakri bin Abdullah ibn Abi Maryam, kuhusu yeye Ahmad bin Hanbali amesema: “Si chochote,” na Daaru Qutni amesema: “Ni mwenye kuachwa,” tazama kitabu *Tahdhiibul-Tahdhiib*, Juz. 12, uk. 33.

Na hadithi ameipokea Ahmad bin Hanbali katika *Musnad*, Juz. 5, uk. 191, na Ibn Abi Aswim katika Sunan, uk. 185 nambari 426, na amekiri Albani huko kwamba hakika sanad yake ni dhaifu. Na ameipokea Hakim katika *Mustadrak*, Juz. 1, uk. 516, na amekubali usahihi wake! Dhahbi akamfuatia akisema: “Abu Bakri ni mtu dhaifu na wapi alikuwa katika usahihi?”

### **Hadithi ya 19: Kisha Ibn Qayyim akasema:**

“Na ama hadithi ya Ammar bin Yasir: Imam Ahmad amesema: Ametu hadithia Is’haaq Azraq, kutoka kwa Sharik, kutoka kwa Hashim, kutoka kwa Abi Mijlaz, amesema: Ammar alituswalisha Swala akafupisha basi wakachukizwa na hilo....” Na ndani yake kuna ibara: [Basi akaomba dua ambayo ndani yake kuna: Na ninakuomba ... na ladha ya kuangalia uso wako ....]

**Nasema:** Haijathibiti humo lafudhi “Na ladha ya kuangalia uso wako” hakika ameipokea Ibn Abi Shaybat, Juz. 6 uk. 45 /29348 kwa sanadi sahihi na hakuna ndani yake lafudhi hiyo!! Abu Hashim na Yahya bin Dinar Rummani, na Abu Mijlaz na Lahiq bin Humaid Sadusi, na hakika amechakachua hapa Abu Mijlaz hivyo akamwondoa Sheikh wake katika mlolongo wa wapokezi, naye ni Qays bin Ubaada!

Ameipokea hadithi hii Ahmad, Juz. 4, uk. 264, na Nasai, Juz. 3, uk. 55, na wengineo kutokana na njia ya Sharik kutoka kwa Abu

Hashim Yahya bin Dinar Rummani kutoka kwa Abi Mijlaz, kutoka kwa Qays bin Ubaad kutoka kwa bwana wetu Ammar. Ila hakika Ahmad hakumtaja katika *Musnad* yake Qays bin Ubaada! Na Bazazz amesema katika *Musnad* yake Juz. 4, uk. 229: “Wala hatujui alichopokea Qays bin Ubaada kutoka kwa Ammar ila hadithi hii.”

Abu Mijlaz ni mkorogaji wa hadithi mbele ya Yahya bin Muiin, na katika kitabu *Twabaqaatul-Mudallisiina*, uk. 27 amesema: “Ibn Abi Khaythamat ameashiria kutoka kwa Ibn Muiin kwamba hakika yeeye alikuwa ni mchakachuaaji, na amelikubali hilo Daaru Qutni.” Na ninaongeza katika hilo hakika ndani ya sanad yupo Sharik naye ni mtu dhaifu kwao!!

Na imebakia sanadi nyingine nayo ni ile ilioandikwa na Ibn Abi Aswim, uk. 425, na Nasai, Juz. 3, uk. 45. Na Ibn Haban katika *Sahih* yake, uk. 1971, na Hakim Juz. 1, uk. 524, na Ibn Khuzamat katika *Tawhiid* kutokana na njia za Hamad bin Zayd kutoka kwa Atwai bin Saaib, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa bwana wetu Ammar .

**Nasema:** Na sanadi hii ni dhaifu kwa ajili ya Atwai bin Saaib na alikuwa msahaulifu na alichanganikiwa! Na Yahya Qatwan ametaja kwamba hadithi ya Shuubat na Sufyan kutoka kwake ni sahihi ila hadithi mbili. Na pamoja na hivyo hakika alikuwa Shuubat akisema: “Ametuhadithia Atwai bin Saaib na alikuwa msahaulifu.” Na Yahya bin Muiin amesema: “Wote waliopokea kutoka kwa Atwai wamepokea wakati alipokuwa amechangan-yikiwa ila Shuubat na Sufyan, na pia Shuuba amesema – naye ni kama vile walivyosema amepokea kutoka kwake kabla ya kuchanganikiwa:- Watatu wamo katika moyo, mionganoni mwao ni Hajis: Atwai bin Saaib...”

Na amenukuu Aqiliy katika kitabu *Dhuufaa* kutoka kwa Nasai, Qatwan na Bukhari kwamba hakika hadithi ya Hamad bin Zayd ku-

toka kwake ni sawa na ya Shuubat na Sufyan, na wala sioni chochote katika hilo, kwa sababu zifuatazo:

1. Hakika wao hapo kabla wamepokea kutoka kwao kauli hizi pasi na kumtaja Hamad bin Zaydi.
2. Hakika Yahya bin Muin na wengineo hawakumwengua Hamad bin Zaydi.
3. Hakika Yakub bin Sufyan amesema katika kitabu *Al-Maarifatu wa Taariikh* Juz. 3, uk. 84: “Atwai ni mtu mkweli, hadithi zake ni hoja, waliopokea kutoka kwake ni Sufyan na Hamad bin Salama hapo zamani....”

Na hapa zimevurugana na kukorogana hadithi kutoka kwao! Na lililo dhahiri ni kwamba mmoja wa wanahadithi wa kale amemungeza Hamad kwa Shuubat na Sufyan, watu hawa hawakumjua ni nani Hamad basi wakamwekea shaka yeye, kwamba je, yeye ni Hamad ibn Salama au Hamad bin Zayd! Na kwa hivyo tunarejea katika asili, nayo ni kwamba hadithi ya Ibn Zayd si hoja kwani alikuwa katika zama za kuchanganikiwa.

1. Hakika Bukhari hakupokea kwa Atwai bin Saaib ila hadithi moja ya ufuataji!
2. Hakika hadithi ya Hamad bin Zaydi kutoka kwa Atwai bin Saaib hakuieleza ye yeyote miiongoni mwa watanzi wa vitabu tisa ila Tirmidhi, uk. 959, na Nasai katika sehemu nne katika kitabu chake *Sunan Sughra*, uk. 1305, 1348, 2919, 4163 na Ahmad bin Hanbali katika kitabu chake *Musnad* katika sehemu moja tu. – Na kwa hivyo inasihi kwetu kusema kwamba njia za hadithi hii zote ni dhaifu sio thabiti.

Hakika nimelifuatilia hili na nikakuta kwamba Ibn Abi Shaybat ameipokea katika kitabu *Muswanafu* Juz. 6, uk. 45, kwa sanad sahihi

kutokana na hadithi ya bwana Ammar bin Yasir na hakuna lafudhi “Na ladha ya kuangalia uso wako.”

Vivyo hivyo ameipokea kwa njia nyingine ambayo kuna udhaifu wa Abu Yaali katika *Musnad* yake Juz. 3, uk. 195/1624, na Mua’mmar ibn Rashid ameipokea katika *Jaamiat*, Juz. 10, uk. 442, kutoka kwa mwanaume kutoka kwa Mtume ﷺ. Na Twabarani ameipokea katika kitabu *Al-Kabiir*, 10/68/9942 kutokana na hadithi ya Ibn Mus’ud bila ya kipengele hicho katika dua ya mwisho wa swala. Hakuna ndani yake kuangalia uso wake pamoja na kuwa ndani yake kuna lafudhi “Pasi na madhara yenyewe kudhuru wala fitna ipotoshayo.”

Na linanithibitikia mimi kwamba kuna uchakachua ji katika hadithi husika, kwa upande wa watu wa kale wa Sham ambao wana muunganiko wa kifakra na Kaab bin Akhbar, tunakuta hayo kutokana na ufuatiliaji wa sanad na kuchunguza wapokezi wake na matini zake.

Ibn Qayyim baada ya hadithi ya bwana wetu Zayd bin Thabit amesema: “Abu Daud ameipokea katika *Sahih* yake” na hadithi hajaipokea Abu Daud! Na Abu Daud hana *Sahih*! Lakini imepatikana katika *Awaaswim Minal-Qawaasim* Juz. 5, uk. 173 kwa lafudhi: “Hakim ameipokea katika *Sahih* yake,” na akatoa maelezo juu yake mtoaji maelezo huko – na ninadhani yeye ni Sheikh Shuaiba Arnaut – kwa kauli yake: “Katika kuiita *Mustadrak* ya al-Hakim kuwa ni *Sahih* ni kutojali kusikokubalika, na hakika limetokea hili kwa Ibn Qayyim Mungu amhurumie, katika sehemu zaidi ya moja katika utunzi wake, na wala sidhani kuwa yafichikana kwake kuwa katika kitabu *Mustadrak* kuna hadithi nyingi zilizo dhaifu na kati ya hizo ni zile zilizowekwa na kupachikwa!!”

**Nasema:** Na sababu ya kauli ya Ibn Qayyim “Amepokea Hakim katika *Sahih* yake” ni upotoshaji na kuwazuga watu kwa kuwaziba macho!!

### **Hadithi ya 20:** Kisha Ibn Qayyim akasema:

“Na ama hadithi ya Bi. Aisha ﷺ katika Sahihi ya Hakim kutoka kwa Zahri kutoka kwa Urwat, amesema: Mtume ﷺ alisema kumwambia Jabir: “Je, nikubashirie?” Akasema: Ndio, Mwenyezi Mungu akubashirie kwa kheri, akasema: “Nimehisi hakika Mwenyezi Mungu amemweka hai baba yako na amemkalisha mbele Yake. Amemwambia: ‘Mja wangu tamani chochote utakacho nitakupa hicho.’ Yeye amesema: ‘Ewe Mola Wangu Mlezi...’” Nayo imo katika *Musnad* kutokana na hadithi ya Jabir, na kwa Tirmidhi kuna fuo la maneno lililotimia zaidi kuliko hili, kutoka kwa Jabir, amesema: “Pindi alipouawa Abdullah bin Amru bin Haram siku ya vita vya Uhud, Mtume ﷺ alisema: ‘Ewe Jabir! Je, nikupe habari aliyosema Mola Manani kumwambia baba yako?’ Akasema: Ndio. Akasema: ‘Mwenyezi Mungu hakumsemesha yejote isipokuwa nyuma ya pazia, na amemsemesha baba yako ana kwa ana moja kwa moja (bila pazia) amemwambia: Ewe mja wangu tamaani neema Yangu nitakupa...’” Tirmidhi akasema: Hadithi hii ni hasan (nzuri) ngeni. Nasema: Na isnad yake ni sahihi ameipokea Hakim katika *Sahih* yake.””

**Nasema:** Bali hiyo ni Hadithi ya kubuniwa ya uwongo, ipo nje ya kawaida na utaratibu, na ni yenye kuchukiza kwa matamshi hayo!! Katika sanadi ya Hakim kuna muongo sana naye si mwiningine bali ni Faidh bin Wathiq, na Ibn Qayyim hakumtaja kwa sababu yeye amevunja utoaji wake wa dalili kwa hadithi hii iliyooza!!

Na hakika Dhahabi amemwelezea baada ya Hakim katika kitabu *Al-Mustadrak*, Juz. 3, uk. 203, akasema: “Faidh ni mtu muongo sana.” na Yahya bin Muin amesema: “Ni mtu muongo na khabithi” angalia kitabu *Lisaanul-Miizan*, Juz. 4, uk. 532, Chapa ya Darul-Fikr.

Na ama katika sanadi ya Tirmidhi, Hadithi ya 3010, ndani yake yumo: Musa bin Kathiir Answari: “Hakuna aliyemzingatia kuwa ni mwaminifu na mkweli ila Ibn Abaan katika kitabu chake *Athuqaat*, Juz. 7, uk. 449, na akasema: “Alikuwa kati ya wale wanaokosea.” Angalia kitabu *Tahdhiibul-Kamaal*, Juz. 29, uk. 20 - 21.

Na Sheikh Answariy amesema: “Twalha bin Khirash amesema: Hafidh bin Hajar amesema katika wasifu wake katika *Tahdhiibul-Tahdhiib*, Juz. 5, uk. 14-15: [Azdi amesema: Twalha amepokea kutoka kwa Jabir yale yachukizayo. Na Abu Musa amemtaja katika kitabu *Dhaylu Maarifatul-Swahabat*, na akabainisha kuwa hadithi yake ni Mursal] na amepokea kwa lafudhi na sanad pia Ibn Majah 190 na 2800.

Na vipi itakuwa hadithi hii ni sahihi kama anavyosema Ibn Zafir?! Hasa ikizingatiwa kuwa amepokea hadithi hii kutoka katika njia nyingine ikiwa ndani yake haijataja yale ayatakayo Ibn Qayyim ili kuthibitisha kuonekana kwa Mwenyezi Mungu? Na hili ni mionganoni mwa yale yanayoharibu utoaji wa dalili!

Miongoni mwa njia hizo ni yale aliyoyapokea Ahmad bin Hanbali katika *Musnad* wake Juz. 3, uk. 361, amesema: Ametuhadithia Ali Madani: Ametusimulia Sufyan, kutoka kwa Muhammad bin Ali bin Rabiat Salami, kutoka kwa Abdullah bin Muhammad bin Aqil kutoka kwa Jabir, Mtume ﷺ alimwambia: “Ewe Jabir! Je, unajua hakika Mwenyezi Mungu (a.j.) amemweka hai baba yako aka-mwambia omba neema yoyote Kwangu, akasema: ‘Nirudishe duniani niuwawe mara nyingine,’ akasema: Hakika Mimi nimepitisha hukumu hakika wao hawarejei humo”

Wala sijui ni kwa nini hakubainisha mtoaji maelezo wa kitabu *Awaaswim* cha Ibn Wazir kwamba hakika hadithi hii ambayo amehukumu sanad yake kuwa ni nzuri katika mstari wa pambizo, kwamba haitaji suala la kuonekana kwa Mwenyezi Mungu?!

Na Bibi Aisha رضي الله عنها, mama wa Waumini, ni mwenye kuchukizwa na suala la kuonekana kwa Mwenyezi Mungu, na hadithi yake kuhusu hilo ipo katika *Sahih Mbili*, naye anatoa hoja kwa ujumla wa kauli ya Mola Manani: “Na haikuwa kwa Mwenyezi Mungu aseme na kiumbe ila kwa ufunuo au nyuma ya pazia au amtume mjumbe.....,” na kwa ujumla wa kauli ya Mwenyezi Mungu (s.w.t): “Macho hay-amfikii, bali ye ye anayafikia macho.”

Na atakayedhibiti na kuzingira hilo kwa kusema: Makusudio yake ni duniani na sio akhera! Tutamwambi: Ubainishaji na uwekaji mipaka huu ni kulazimisha bila dalili! Hivyo hauna thamani yoyote! Na ujumla unabaki kama ulivyo!

**Hadithi ya 21:** Ibn Qayyim baada ya hayo amesema:

“Na ama hadithi ya Abdullah bin Umar; Tirmidhi amesema: Ametu-hadithia Abdu bin Humayd, kutoka kwa Shubabat kutoka kwa Ismail, kutoka kwa Thaur bin Abi Fakhitat, amesema Twabarani: Ametu-hadithia Asad bin Musa: Ametusimulia Abu Muawiya Muhammad bin Khazim, kutoka kwa Abdul-Malik bin Abkhar, kutoka kwa Thaur bin Abi Fakhitat, kutoka kwa Ibn Umar kwamba Mtume ﷺ amesema: “Hakika daraja ya chini zaidi ya watu wa peponi ni kuangalia ufalme wake miaka elfu moja, wa mbali atauona kama atakavyouona wa karibu, kama vile mtu anavyowaona wake zake, kitanda chake, viti vyake na watumishi wake. Na hakika mbora wao mwenye daraja ya juu zaidi atamwangalia Mwenyezi Mungu mara mbili kila siku.””

Na amekiri Ibn Qayyim baada hayo kwa mistari miwili akasema: Ashjaii Ubaidullah amepokea kutoka kwa Thauri kutoka kwa Mujahid kutoka kwa Ibn Umar mfano wa hayo na wala hakuacha kutaja mlolongo wa wapokezi wake.....

**Nasema:** Ni yenyе kupachikwa na kubuniwa! Mzunguko wa hadithi katika njia hizi uko juu ya Thaur bin Abi Fakhitat. Sufyan

Thaur amesema: "Yeye ni mionganini mwa nguzo za uongo." Na Ibn Muin amesema: "Sio chochote." Daru Qutni amesema: "Ni mwenye kuachwa na kupuuzwa." Angalia kitabu *Tahdhiibul-Kamaal*, Juz. 4, uk. 430.

Na hadithi hii imepokewa na Abu Yaali, 5712 na 5729, na Hakkim Juz. 2, uk. 553, na Abu Nuaim katika kitabu *Hilyatu*, Juz. 5, uk. 87, na Ahmad bin Hanbali Juz. 2, uk. 13 na 64, na Ibn Mubarak katika kitabu *Zuhd*, Juz. 1, uk. 127, na wale wenyewe fikra na imani kuwa Mwenyezi Mungu ana mwili katika vitabu vya Sunna kama vile Laalkaai na Aajury na wengineo. Nayo ipo katika *Musanaf*, Juz. 7, uk. 34, ikiegemezwa kwa Ibn Umar, na vivyo hivyo ametoa habari yake Tirmidhi katika Sunan 2553 na 3330! Na kama ikiwa ni hivyo hakuna shaka kwamba hiyo ni kati ya zile walizopokea watu kutoka kwa mfano wa Kaab bin Akhbar na mfano wake mionganini mwa wale wanaonukuu kutoka katika vitabu potofu vya kale!! Na kwa mfano wa hadithi hizi na athari wanahukumu juu ya suala la kuonekana kwa Mwenyezi Mungu kwa tawaturi na ukataji shauri!!

### **Hadithi ya 22: Kisha Ibn Qayyim baada ya hayo akasema:**

"Na Said bin Hashim bin Bashir amesema: Kutoka kwa baba yake, kutoka kwa Kauthar bin Hakim, kutoka kwa Nafi kutoka kwa Ibn Umar: Mtume ﷺ amesema: "Siku ya kwanza ya Kiyama jicho litamwangalia Mwenyezi Mungu." Ameipokea Daru Qutni kutoka katika kundi....."

**Nasema:** Huu ni uongo na imebuniwa na ni yenye kuwekwa! Kauthar bin Hakim ambaye yumo katika sanadi ya hadithi hii amesema Ahmad bin Hanbali kumhusu yeye: "Hadithi zake ni batili na sio chochote," na Barqani na Daru Qutni wamesema: "Hadithi zake ni zenye kuachwa" na Dhahabi ametaja katika kitabu *Miizan*

na Hafidh Ibn Hajar katika kitabu *Lisaanul-Miizan*, Juz. 4, uk. 490, Chapa ya India, kwamba hakika miongoni mwa batili zake ni hadithi hii batili! Mwenyezi Mungu awatosha kuwakinga waumini na shari ya mapigano! – Na hadithi ameieleza Khatwiib Baghdadi katika *Tarikh* yake Juz. 10, uk. 351-352, na Daylami katika kitabu chake *Musnadul-Firdaus*, Juz. 5, uk. 530.

Kisha iweje anukuu Ibn Qayyim hadithi ya Jabir ya kwamba hakika baba yake alimuona Mwenyezi Mungu baada ya kifo chake?! Na hakika Ibn Abbas K kama wanavyodai amesema kwamba Mtume ﷺ alimuona Mola Wake Mlezi usiku wa Israa, hadithi inasema: “Hakika nyinyi hamtamuna Mola Wenu Mlezi mpaka mfe,” na isiyokuwa hiyo! Yote hayo yanapingana na hadithi ambayo ndani yake kuna ibara inayosema: “Jicho la kwanza kumuona yeye Siku ya Ki-yama!!” Na kutokana na haya inabainika msigano wa watu hawa katika ufkiri wao na utoaji wao wa dalili!!

### **Hadithi ya 23:** Kisha Ibn Qayyim akasema:

“Daru Qutni amesema: Ametuhadithia Ahmad bin Suleiman: Ametusimulia Muhammad bin Yunus: Ametuhadithia Abdul-Hamiid bin Saleh: Ametusimulia Abu Shihaab Al-Hanaat, kutoka kwa Khalid bin Dinar kutoka kwa Hamad bin Ja’far, kutoka kwa Abdullah bin Umar, amesema: Nimemsikia Mtume ﷺ akisema: ‘Je, nikuhabariheni watu wenye daraja la chini peponi?’” Wakasema: Ndio, ewe Mtume, basi akataja hadithi hadi aliposema: “Hadi itakapofikia neema ya kiwango cha juu na wakadhani miongoni mwenu hakuna neema bora zaidi kuliko hiyo, mara atajitokeza Mola Mlezi juu yao basi watakapoangalia uso Wake, Rahman atasema: Enyi watu wa peponi nifanyieni tahlili na kunitukuza na kunifanya mkubwa na kunitakasa kama mlivyokuwa mkinifanya tahlil na kunitukuza na kunitakasa duniani, basi wataitikiana kwa tahlili ya Rahman.....””

**Nasema:** Lafudhi hii ya hadithi imo katika kitabu cha *Ru'uyat* ambayo inanasibishwa kwa Daru Qutni. Ni hadithi nambari 176, na amepokea mfano wake Abdu bin Hamiid katika *Musnad* wake Juz. 1, uk. 268 na 851, na akasema Mundhiri katika kitabu *Targhiib Wa Tarhiib*, Juz. 4, uk. 278: Na amepokea Ibn Abi Dunia na katika sana-di yumo yule ambaye simjui hadi sasa.

Katika sanadi yake yumo Muhammad bin Yunus na yeze ni wa kale na mwekaji hadithi mashuhuri. Ana wasifu mrefu katika kitabu *Tahdhibul-Kamal*, Juz. 27, uk. 66-81, na kuhusu yeze amesema Daru Qutni: "Alikuwa mtu wa Kadimi akituhumiwa kwa uwekaji wa hadithi" na amekadhibishwa na Abu Daud na Ahmad bin Hanbali na Suleiman Shadhikuni.

Na inatosha uangushaji huu wa hadithi!! Ninaongeza katika hilo kwamba Hamad bin Ja'far hana hadithi kutoka kwa Masahaba, naye ni dhaifu, na huu ni upungufu wa sanadi!! Na mbunifu na mzushi wa hadithi hii hakuweka mlolongo wa sanadi. Hivyo basi hadithi ni ya kubuniwa na ni ngano za kale. - Kisha Ibn Qayyim wakati wa kumjibu kwake Bashar Mariisi ameirudia hadithi hii kutoka katika njia ya Uthman bin Said Daarimi kwa sanadi hiyo hiyo iliyobuniwa.

**Hadithi ya 24:** Ibn Qayyim baada ya hayo akasema:

"Na ama hadithi ya Ammara Ruwaiba: Ibn Batwa katika kitabu *Al-Ibaanat* amesema: Ametuhadithia Abdul-Ghafir bin Salaam Himswi: Ametusimulia Muhammad bin Awf bin Sufyan Twaai: Ametuhadithia Abu Al-Yamaan: Ametusimulia Ismail bin Ayaash, kutoka kwa Abdul-Rahman bin Abdullah kutoka kwa Ismail bin Abi Khalid, kutoka kwa Abi Bakri bin Ammara bin Ruwaiba kutoka kwa baba yake amesema: Mtume ﷺ aliuangalia mwezi usiku wa badri akasema: Hakika nyinyi mtamuona Mola Wenu Mlezi kama vile mnavyouona

huu mwezi. Hamtapata madhara katika kumuona kwake, na kama mkiweza kutoshinda na swala kabla ya kuchomoza jua na kabla ya kuzama kwake basi fanyeni.”

**Nasema:** Ibn Batwa ni muongo, na ni mhanbali na ni mwenye imani ya kwamba Mwenyezi Mungu ana mwili, na inatosha kuikataa hadithi hii kwa sababu ya kuwepo yeye katika sanad yake. Na hakika Hafidh ibn Hajar ametaja wasifu wake katika kitabu *Lisanul-Miizan*, Juz. 4, uk. 131, na akasema katika wasifu wake huo, akifuatilizia maneno ya Dhahabi: “Nilipata kwa Ibn Batwa jambo lililonishangaza na ngozi yangu kujikunja kwalo.”

Kisha Hafidh akathibitisha kwamba yeye ni mwekaji na mbunifu wa hadithi, na hakika yeye alikuwa akiyaponda majina ya maimamu kutoka katika vitabu vya hadithi na akiweka jina mahali palipofutwa, na ameandika Khatib Baghdadi katika *Tariikh* yake Juz. 10, uk. 375, hadithi kwa sanad batili kisha akasema: Nayyo imewekwa kwa sanad hii, na mzigo wake ni juu ya Ibn Batwa.” Yaani hakika yeye ni mpandikizaji wa hadithi! Na angalia kitabu chetu *Ilamul-Hajar* uk. 4 - 6.

Na katika wasifu wa Abi Bakri bin Ammara bin Ruwaiba katika *Tahdhibul-Kamal*, Juz. 33, uk. 125 imetaja hadithi hii na kwamba ipo katika *Sahih Muslim*, akifupisha kwa kutaja swala pasi na kutaja uonaji! Hivyo basi hadithi hii imechezewa na mikono ya viongozi ambao ni wahudumu na vibaraka wa fikra za Kiyahudi!!

Na Abu Bakri huyu hata akiwa ni mionganini mwa wapokezi wa Muslim, na yeye ni mionganini mwa wale wenye kukubalika kwa Hafidh katika kitabu *Taqrib*!! Na hao hazikubaliwi hadithi zao ila kwa mfuataji!! Na Ismail bin Ayash Al-Himswi ni dhaifu kwa wasiokuwa watu wa Sham, na Abdul-Rahman bin Abdullah naye ni Mas’ud walimuona dhaifu.

Na aliirudia Ibn Batwa kwa sanad ambazo ndani yake kuna baadhi ya ikhtilafu na wala hakuna faida kwayo, nayo ni katika batili zake!

### **Hadithi ya 25: Kisha Ibn Qayyim Al-Jawziyya akasema:**

“Na ama hadithi ya Sulaiman Farsi: Baba wa Muawiya amesema: Ametuhadithia Aswim Ahwal, kutoka kwa Abi Uthman, kutoka kwa Sulaiman Farsi amesema: Watamjia Mtume ﷺ na watasema: Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu amefungua kwako na amehitimisha kwako, na amekusamehe, simama utuombee kwa Mola Wako Mlezi, atasema: “Ndio, mimi ni sahiba wenu,” basi akatoka hali watu wakimzunguka hadi watafika kwenye mlango wa peponi basi atachukua komeo la mlango atagonga, hapo pataulizwa: Ni nani wewe? Atajibu: Muhammad, basi atamfungulia mlango, atakuja mpaka atasimama mbele ya Mwenyezi Mungu, ataomba idhini ya kusujudu na atamuidhinisha....”

**Nasema:** Hii ni athari batili, hakuna utajo wa kumuona Mwenyezi Mungu, lakini ndani yake kuna maneno yanayoashiria kwamba hakika Mwenyezi Mungu (a.j.) anachukua nafasi Yake peponi, Mwenyezi Mungu ametukuka na ameepukana nalo, hayuko hivyo kabisa.

Amepokea athari hii Twabarani katika kitabu *Al-Kabiir*, Juz. 6, uk. 247, na Muhamili katika kitabu *Aamal*, Juz. 1, uk. 115, na amepokea Ibn Abi Aswim katika *Sunnan* nambari 813 na Ibn Shuaiba katika *Muswanafu wake*, Juz. 11, uk. 447, na Dhahabi katika *Siyaru Aalaam Nubalaat*, Juz. 1, uk. 554. Nayo ni yenyenye kunasibishwa na bwana wetu Salman Farsi, nayo ni katika hadithi za Kiyahudi bila shaka, na ikisihi kutoka kwa bwana wetu Salman Farsi basi itakuwa ni kati ya zile alizonukuu kutoka katika vitabu vya kale alivyokuwa amevisoma.

Na kati ya dalili za kuonesha kwamba alikuwa akinukuu kutoka katika vitabu hivyo alivyosoma kabla ya Uislamu, ni yale yaliyot-hibiti katika maelezo ya andiko nambari 99 katika kitabu *al-Uluwu* cha Dhahabi, ambayo nimeyataja huko.

Amepokea Bayhaqi katika kitabu *Asmaau wa Sifaat*, uk. 90, kutoka hadithi ya Abu Uthman Nahdi kutoka kwa Salman Farsi amesema: “Ninakuta katika Taurat: hakika Mwenyezi Mungu yu hai mkarimu anaona haya kurudisha mikono miwili tupu iliyomuomba kheri.” Hili amelieleza Tirmidhi, na unabainika ukweli kwamba ni katika yale aliyoyanukuu kutoka katika Taurati.

Na hii ni katika hadithi za Abu Uthman Nahdi, nayo pia ni miongoni mwa hadithi za Kiyahudi!! Hivyo kauli ya Albani katika utoaji wa maelezo juu ya kitabu *Sunnan* cha Abu Aswim kwamba hakika hiyo sio mionganini mwa zile hadithi za Kiyahudi, ni mionganini mwa mapotofu yake yenye kujulisha kwamba hakudiriki kadhia ya Hadithi za Kiyahudi na hakuzielewa wala kuzifahamu! Hasa ukizingatia kwamba hadithi hii imepokewa na wengine pia mionganini mwa Masahaba kama vile Anas bin Malik na wengineo, na wao ni mionganini mwa wadogo ambao wamepokea kutoka kwa Kaab bin Akhbar na kutoka kwa asiyekuwa yeye hadithi za Kiyahudi kama ilivyohakikawa na kuthibitishwa katika utangulizi wetu katika kitabu *al-Uluwu* na katika maelezo tuliyoweka!!

**Hadithi ya 26:** Kisha baada ya hayo Ibn Qayyim Jawziyya akataja hadithi ya kioo cha siku ya Ijumaa, ambayo ndani yake kuna maelezo kwamba bwana wetu Jibrail عليه السلام alimjia Mtume ﷺ akiwa na kioo kikiwa na kidoti cheusi, kama inavyoeleza hadithi ya Hudhaifa bin Al-Yamaan. Na hadithi hii imebuniwa nayo ipo katika kitabu *al-Uluwu* cha Dhahabi andiko namba 40 – 43, na hakika nimetoa maelezo juu yake huko na kubainisha kwamba hadithi imebuniwa na kuzushwa.

Lakini hapa ameitaja katika hadithi za kutoka kwa bwana wetu Hudhaifa, nayo imebuniwa na kupachikwa pia! Na yatupasa kuzungumza hapa juu ya sanad yake kwani mazumbukuku hawajui ubatili wa hadithi ila tukisema na kuwaambia wao: ‘Amesema Abu Zur’at na akasema Abu Mur’at!!’

**Tunasema:** Amepokea hadithi hii Bazzaz katika *Musnad* yake Juz. 7, uk. 289 na 3518, na Hafidh Haythami ameitaja hiyo katika kitabu *Majmaul-Zawaaid*, Juz.10, uk. 422, na akasema: “Ndani yake yuko Qasim bin Matwiib, naye ni mwenye kuachwa na kupuuzwa.” Na baada ya hayo Bazzaz akasema: “Na hadithi hii hatujui wapi imepokewa kutoka kwa Hudhaifa ila kutohana na upande huu, wala hatumjui aliyeipokea kutoka kwa Aamash ila Qasim bin Matwib, wala hakumhadithia yeye ila Yahya bin Kathir. Kutoka kwa Ibrahim bin Mubarak, amesema: Nimemsikia Ahmad bin Amru bin Ubaida akisema: Nilimkumbusha Ali bin Madani akaniambia: Hadithi hii ni ngeni na wala sijaisikia.....” hivyo hadithi hii ni ya uzushi na ya uwongo.

### **Hadithi ya 27: Kisha Ibn Qayyim Jawziyya akasema:**

“Abdul-Rahman bin Mahdi amesema: Ametuhadithia Israil, kutoka kwa Abu Is’haq kutoka kwa Muslim bin Yazid Sa’adi, kutoka kwa Hudhaifa katika kauli yake (s.w.t) “Wale waliofanya wema wata-pata wema na ziada” akasema: Kuangalia uso wa Mwenyezi Mungu (s.w.t).”

**Nasema:** Haisihi hii, nayo imeachwa, na iliyooachwa haina hoja!! Na niliona maelezo juu ya kitabu *Awaswim Minal-Qawaswim* cha Ibn Wazir Juz. 5, uk. 182 – wala sijui je, huyo ni Sheikh Shuaib au mwingine, kwa sababu hizo tafiti na uhakiki na utoaji wa maelezo havina mwelekeo na iko wazi kuwa vimenukuliwa kutoka kwa Al-

bani – huko anasema: Wapokezi wake ni wakweli, Muslim bin Yazid: “Ni Muslim bin Nadhir, hakuna tatizo lolote kwake” na neno “hakuna tatizo lolote kwake” amelinukuu mtoaji maelezo na akat-egemea maelezo ya mwenye kujipinga (Albani) aliyoyatoa juu ya kitabu *Sunnah Ibn Abi Aswim!!*

Na kwa hali yoyote itakayokuwa hakika Hafidh amesema katika kitabu *Lisaanul-Miizan*, Juz. 7, uk. 469 kuhusu Muslim huyu kuwa “Alivusha hadithi kutoka kwa Ali,” na akasema katika kitabu *Taqrib*: “Anakubalika katika tabaka la tatu.” Na hakika nimezungumza katika kitabu *Risaalat Taqswiir Thawb* juu ya Muslim bin Nadhir huyu, na nimebainisha kuwa hajulikani kwa usahihi zaidi, basi rejea huko ukipenda upanuzi na ufanuzi zaidi, nayo ni maneno muhimu mno.

Na hadithi hii ameipokea Ibn Abi Shaybat, Juz. 7, uk. 140 katika kumjibu kwake Marisi, na Ajuriy katika kitabu chake *Shariat*, na Ibn Ahmad katika *Sunnan*, na Laalkaai katika kitabu chake *Sharhu Usuul Itiqaadihi*, na Ibn Khuzaima katika kitabu chake *Tawhiidi* ambacho ametubu kutokana nacho! Na hii ni miuongoni mwa dalili za uzushi wake na kwamba yeche ni mpotoshaji wa maelezo kutoka kwa bwana wetu Hudhaifa bin Yamaan!!

### **Haadithi ya 28: Kisha Ibn Qayyim baada ya hayo akasema:**

“Na ama hadithi ya Ibn Abbas ﷺ; amepokea Ibn Khuzaima kutokana na hadithi ya Hamad bin Salama kutoka kwa Ibn Juduan, kutoka kwa Abi Nadhra amesema: Alituhutubia Ibn Abbas ﷺ akasema: Mtume ﷺ alisema: ‘Hakuna Nabii ila ana maombi anaharakishiwa kujibiwa duniani, na mimi nimeficha maombi yan-  
gu katika uombezi kwa umma wangu Siku ya Kiyama. Nitakwenda kwenye mlango wa pepo na nitagonga mlango. Na itaulizwa: Ni

nani wewe? Nitasema: Mimi ni Muhammad. Basi nitamwendea Mola Wangu Mlezi naye akiwa ameketi juu ya kiti chake au kitanda chake, basi atajidhihirisha kwangu Mola Wangu Mlezi, hapo nitaporomoka chini na kumsujudia.' Na ameipokea Ibn Uyyayna kutoka kwa Ibn Jaduan akasema: Kutoka kwa Abu Said badala ya Ibn Abbas ﷺ."

**Nasema:** Ewe mpotokaji!! Hamuoni haya kutaja hayo!! Hivi mnakokoteza na kumsifu Mwenyezi Mungu kwamba yuko juu ya kiti chake au juu ya kitanda chake?!! Na lau mngelidiriki zama hizi basi mngepokea kwa maana ya zama hizi, mngesema: "Juu ya meza yake..." Mwenyezi Mungu ametukuka kwa upotofu wa fikra zao na wayasemayo, ameepukana nayo kabisa!!

Ama kuhusu sanad ya Hamad bin Salama, yeye ana mapungu-fu mengi, habari zake hazikubaliwi wala hazichukuliwi, na hakuna dalili bora juu ya hilo kushinda kukiri kwa Ibn Qayyim kuwa Ibn Uyyayna ameipokea kutoka katika hadithi za Abu Said, na Abu Said ameipokea mfano wa hadithi hizi za Kiyahudi kutoka kwa Kaab Akhbar na mfanowe mionganii mwa wale wanaowaita kuwa ni Waislamu wa watu wa kitabu!!

Na hakika ameipokea Hamad bin Salama kama ilivyo katika kitabu *Taadhiim Qadr Swalaat*, Juz. 1, uk. 274 na 265, kutoka kwa Thabit kutoka kwa Anas, na hili linajulisha juu ya uchakachuaji wake wa hadithi hii, au hakika mtoto wake wa kulea ameingiza mikono katika hadithi na kutia maneno "naye akiwa juu ya kiti chake au kitanda chake"!! Na hadithi ameieleza Ahmad Juz. 1, uk. 281 na 295. Na Daarimi mwenye imani kuwa Mwenyezi Mungu ana mwili ameiandika katika kitabu chake, vivyo hivyo kaka yake Laalkaa 1843. Na Ali bin Zayd bin Jaduan wameutambua udhaifu wake huyu na alikuwa akibadilisha hadithi.

### **Hadithi ya 29: Kisha Ibn Qayyim akasema:**

“Na Abu Bakri bin Abi Daud amesema: Ametuhadithia Ammi Muhammad bin Ash’ath: Ametusimulia Ibn Jubair amesema: Amenihadithia Abi Jubair, kutoka kwa Hasan, kutoka kwa Ibn Abbas ﷺ, kutoka kwa Nabii ﷺ amesema: ‘Hakika watu wa peponi wata-muona Mola wao Mlezi (s.w.t) kila siku ya Ijumaa katika changarawe za karafuu maiti, na atakayekuwa karibu naye zaidi katika kikao chake ni yule mwenye kuharakisha zaidi kwenda kwake (kwenye swala ya Ijumaa) siku ya Ijumaa na yule mwenye kuwahi mapema zaidi.’”

Hadithi hii tumeielezea katika maelezo ya kitabu *Daf'u Shibhu Tashbihih*, ni hadithi ya ishirini na tatu, pale tuliposema:

“Hadithi hii imebuniwa, ni potofu. Ameipokea Ajuriy katika kitabu chake *Shariat*, uk. 265, na sanadi ya hadithi hii ni uozo mtupu, amesema ndani yake: Ametuhadithia Abu Bakri bin Abi Daud - naye ni muongo mno kama alivyomsifu baba yake mwandishi wa kitabu cha *Sunan*, angalia *Lisaanul-Miizan* Juz. 3, uk. 364:- Ametuhadithia Ammi Muhammad bin Ash’ath – Huyu ni mtu asiyejulikana kama ilivyo katika kitabu *Thuqaat*, Juz. 9, uk. 149 cha Ibn Haban: Ametusimulia Hasan bin Hasan – Huyu naye hajulikani; Amesema: Amenihadithia Abi Hasan – Huyu naye hajulikani: kutoka kwa Hasan kutoka kwa Ibn Abbas ﷺ.” – Na sanad iliyotajwa hapa ni potofu kama ilivyo dhihirika!!

### **Hadithi ya 30: Kisha Ibn Qayyim akasema:**

“Na ama hadithi ya Abdullah bin Amru bin Aswi: Amesema Swagha-ni: Ametuhadithia Swadaqat Abu Amru Maq’ad, amesema: Nimesoma kuhusu Muhammad bin Is’haq: Amenisimulia Umayya bin Abdullah bin Amru bin Uthman kutoka kwa baba yake.... Amesema

nilimsikia Abdullah bin Amru bin Aswi akimhadithia Marwan bin Hakam naye alikuwa kiongozi wa Madina, akasema:

Mwenyezi Mungu ameumba makundi mbalimbali ya malaika kwa kumuabudu Yeye, mionganoni mwao wamo malaika waliosimama kwenye mistari tangu siku waliyoumbwa mpaka siku ya Kiyama, na wengine ni malaika wenye kurukuu wanyenyekemu tangu siku waliyoumbwa mpaka siku ya Kiyama, na malaika wengine wamesujudu tangu siku waliyoumbwa mpaka siku ya Kiyama, na itakapofika siku ya Kiyama Mwenyezi Mungu atajidhihirisha kwao, hapo watauan-galia Uso Wake Mtukufu watasema: Utakasifu ni Wako tumekuabu-du Wewe haki ya kukuabudu.”

**Nasema:** Hii imeegemezwa kwa Abdullah bin Umar, nayo ni mionganoni mwa zile za Kiyahudi ambazo zimenukuliwa kwa ajili ya umma huu!! Na hakutaja ni wapi amepokea hadithi hii hadi tuangalie katika sanad zilizobakia!!<sup>15</sup> Nayo ni athari yenyenye kurudishwa na kukataliwa haitupiwi jicho hiyo na ile inayofanana nayo!!

Na hakika ametaja mtoaji maelezo juu ya kitabu *Al-Awaasim Minal-Qawaasim* Juz. 5, uk. 185 cha Ibn Wazir kwamba hakika Suyuut ametaja katika Risala yake *Al-Habaik* 551, na akainasibisha kwa Bayhaqi katika kitabu *ar-Ruuyah*, na kwa Ibn Asakir, na hili ni mionganoni mwa yale ambayo hayanenepeshi wala hayaondoi njaa. Kama alivyotaja mtoaji maelezo juu ya kitabu *Al-Udhmat* cha Ibn Sheikh Isfahani na akasema huko katika mstari wa pambizo Juz. 3, uk. 995: “Nasema: Sanad yake ni sahihi hadi kwa Abdullah bin Amru bin Aswi lakini yeche alikuwa akiangalia katika vitabu vya mwanzo.”

**Nasema:** Huu ni usemaji wa wazi kutoka kwake hadi katika hadithi hizi za Kiyahudi ambazo zimenukuliwa katika umma huu kwa

<sup>15</sup> Ametaja Suyutwi katika kitabu *Al-Haawiyu lil-Fataawa* uk. 199-200 hakika Bayhaqi ametoa athari hii katika kitabu cha kuonekana kwa Mola Manani, na sijasimama kwa uchunguzi juu ya isnad yake kwa ukamilifu.

kuhusisha Mwenyezi Mungu (a.j.), kuhusiana na hadithi hizo za Ki-yahudi Mola Manani anasema: “Na wanasema hili linatoka kwako na hili halitoki kwa Mwenyezi Mungu na wanasema kwa Mwenyezi Mungu uongo na hali ya kuwa wao wanajua.”

Na kutokana na hayo inabainika kwamba maneno haya ni batili na hayafai kuyafanya dalili juu ya masuala ya tohara sembuse kadhia na mambo ya kiitikadi!!

### **Hadithi ya 31: Kisha Ibn Qayyim akasema:**

“Na ama hadithi ya Ubaiy bin Kaab: Daru Qutni amesema: Ametus-hadithia Abdul-Aziz bin Ali: Ametusimulia Muhammad bin Zakaria bin Ziyad, akasema: Amenihadithia Qahtwaba bin Ghudana: Ametusimulia Abu Khalda kutoka kwa Abu Aliya kutoka kwa Ubay bin Kaab kutoka kwa Mtume ﷺ kuhusiana na kauli ya Mola Manani isemayo: “Wale waliofanya wema watapata wema na ziada” akasema: “Ziada” ni Kuangalia uso wa Mwenyezi Mungu (s.w.t).”

**Nasema:** Daru Qutni na Laalkaai wamekuwa wa pekee katika hilo, na hilo linajulisha kwamba hayo ni mionganini mwa hadithi zilizobuniwa na za uongo!! Hata hivyo mimi sijaiona katika kitabu *ar-Ruuyah* chenye kunasibishwa na Daru Qutni!! Bali ipo katika kitabu *ar-Ruuyah* cha Laalkaai, ni hadithi nambari 849.

Na Abdul-Aziz bin Ali, na Sheikh wake Muhammad bin Zakaria ni mionganini mwa wale wasiojulikana!! Wala sijui ni ipi siri ya kunyamaza mhakiki wa kitabu *al-Awaswim Minal-Qawaswim* kwa kuacha kubainisha udhaifu wa hadithi hii – na ninadhani yeye ni Shuaiba na huenda akawa mtu mwengine –?! Na ama sanad ya Laalkaai ndani yake yupo Abbas bin Fadhl Hashim, na sijapata wasifu wake, na amesema mhakiki huko: “Katika sanad yake wamo ambao sijawapata, nao ni: Qahtwaba, Abbas, Waiim na Shekh wa mwandishi!!”

**Nasema:** Hakika nimewapata hao ila Abbas. Wao wasifu wao umetajwa katika kitabu cha historia cha Jurujan, na Qahtwaba wasifu wake umetajwa katika kitabu *Al-Jarh wa Taadiil*. Na kwa ujumla hadithi hii ni mionganoni mwa hadithi zitokazo kwa mmoja wa waongo wenye imani ya kwamba Mwenyezi Mungu ana mwili. Ameizua na kudai kuwa imetoka kwa bwana wetu Mtume ﷺ !! Nayo kwangu mimi ni mionganoni mwa ngano za Kiyahudi ambazo zimesemwa na kuenea mpaka zikawa ni kati ya hadithi za Kiislamu!! Basi tanabahi!

### **Hadithi ya 32. Kisha Ibn Qayyim akasema:**

“Na ama hadithi ya Kaab bin Ajzat: Amesema Muhammad bin Hamid: Ametuhadithia Ibrahim bin Mukhtar, kutoka kwa Ibn Jurayh, kutoka kwa Atwai Khurasani, kutoka kwa Kaab bin Ajzat, kutoka kwa Mtume ﷺ katika kauli yake (s.w.t): ‘Wale waliofanya wema watapata wema na ziada’ akasema: Ziada ni kuangalia uso wa Mola Wao Mlezi aliyetukuka.”

**Nasema:** Hili halisihi kabisa!! Ameipokea hadithi hii Ibn Jarir Twabari katika *Tafsiri* yake Juz. 2, uk. 68 na Laalkaai Juz. 3, uk. 457, na Muhammad bin Hamid Raazi amemtuhumu yeye Abu Zur’at na wengineo kwa uongo, na Bukhari amesema: “Katika hadithi yake yahitaji uangalifu, wasifu wake umo katika kitabu *Tahdhib-Kamaal*, Juz. 9, uk. 111-115.” Na sheikh wake Ibrahim bin Mukhtar amesema Bukhari kumhusu yeye: “Katika hadithi yake yahitaji uangalifu, kama ilivyokuja katika *Tahdhibul-Kamaal* Juz. 2, uk. 196.”

Na ama Atwai bin Abi Muslim Khurasani katika *Jaamiul-Tahswiil fi Ahkamil-Maraasiil* uk. 238, kutoka kwa Yahya bin Muiin amesema: “Simjui kama yeye alikutana na yeote mionganoni mwa Masahaba wa Mtume 8, zaidi ya hilo ni kwamba yeye ni mwingi wa

mawazo hewa!” hivyo sanadi hii ni mbovu na imeoza nayo kwetu sisi ni ya kuunda ya kutengenezwa!!

### **Hadithi ya 33. Kisha Ibn Qayyim akasema:**

“Na ama hadithi ya Fadhal bin Ubaid: Amesema Uthman bin Said Darimi: Amesimulia Muhammad bin Muhajir, kutoka kwa Ibn Abbas K, kutoka kwa Ibn Halbis, kutoka kwa Abi Dardai: Hakika Fadhl bin Ubaid alikuwa akisema: Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba radhi baada ya majaaliwa na maisha mazuri baada ya kufa, na ladha ya kuangalia uso wako, na shauku ya kukutana nawe pasi na madhara yenyе kudhuru wala fitina ipotoshayo.”

**Nasema:** Kwanza hadithi hii hajamtaja Mtume, na si kati ya maneno ya Mtume, wala si hoja hadithi ambayo si kati ya maneno ya Mtume kama inavyojulikana!! Na hakika imebainika kutokana na utoaji wa andiko nambari 19, hakika lafudhi “Na ladha ya kuangalia uso wako” ni upotoshaji katika hadithi au athari!! Na watu wote wa sanad ni watu wa Sham, wa kwanza na baba yake wote ni watu wa Emas, nayo ni sehemu aliyojikita na kitovu cha Kaab Akhbar, hadithi na habari zao hazikubaliki kabisa katika mfano wa jambo hii!!

Na hadithi ameipokea Ibn Abi Aswim katika kitabu chake *Sunnat* 427, Twabarani katika kitabu chake *Al-Kabir* Juz. 18, uk. 319 na 825, na vivyo hivyo katika kitabu *Al-Awsat* na *Majmaul-Bahrayni* 455, na akasema Haytami katika kitabu *Al-Majmau*, Juz. 10, uk. 177 wapokezi wake wawili ni wakweli, na Laalkaai 847. Na dhahiri ni kuwa sanadi yake ni sahihi, nayo ni yenyе mushkeli kwetu sisi kwa kutofautiana na kundi la Masahaba katika lafudhi, kwani hakuna ndani yake utajo wa neno “ladha ya kuangalia uso wake.”

### **Hadithi ya 34. Kisha Ibn Qayyim akasema:**

“Na ama hadithi ya Ubada bin Swamit: Katika *Musnad Ahmad* kutoka kwa Baqiyat: Ametuhadithia Buhair bin Saad, kutoka kwa Khalid bin Maadan, kutoka kwa Amru bin As’wad, kutoka kwa Junadat bin Abi Umayyat, kutoka kwa Ubadat bin Swamit, kutoka kwa Mtume ﷺ amesema: Hakika nimekuhadithieni kuhusu Dajjal mpaka ninachelea kwamba hamtaelewa. Hakika Masihi Dajjal ni mtu mfupi, mwenye umbo baya, mwenye nywele za kusokota, chongo, jicho makengeza, hapendezi wala hana mvuto. Ikiwa mtapatwa na mkanganyiko jueni kuwa hakika Mola Wenu Mlezi sio chongo na nyinyi hamtamuona Mola Wenu mpaka mfe.”

Ameipokea Abu Daud 4320 na hakuna ndani yake neno ziada; na neno ziada ni la Zayd bin Abdu Rabbih kama ilivyokuja katika *Musnad* Juz. 5, uk. 324, na huko kuna mushkeli kuhusu hadithi hii na mgongano kati yake umetajwa katika kitabu *Alfat’hu*, Juz. 13, uk. 97, rejea huko.

Na ameipokea Dhahabi katika kitabu *Mukhtaraat*, Juz. 8, uk. 264 na wengineo. Na Baqiyya ni mtu dhaifu, Sufyan bin Uyayna amesema: “Msisikie kutoka kwa Baqiyya yale ambayo yapo katika sunna,<sup>16</sup> na sikieni kutoka kwake yale yaliyokuwa ya thawabu na mengineyo.” Kitabu *Jarh wa Taadiil*, Juz. 2, uk. 435 cha Ibn Abi Hatam na Dhahabi katika kitabu *Mughni Fil-Dhuafaai*, Juz. 1, uk. 109.

Baqiyya bin Walid ni mmoja wa maimamu wa kuhifadhi hadithi. Amepokea kutoka kwa yule ambaye ameingiza na kuchomeka hadithi za uongo, na yeye anazo hadithi ngeni na za kushangaza, na suala la kuonekana kwa Mola Manani ni uovu uchukizao kutoka kwa wakweli kwa wingi wa hadithi. Ibn Khuzaima amesema: “Simtolei hoja Baqiyya,” na akasema Ahmad bin Hanbali: “Yeye ana

<sup>16</sup> Yaani haikuwa katika itikadi.

machukizo kutoka kwa wakweli waaminifu,” amesema Ibn Haban: “Alisikia kutoka kwa Shuuba na Malik na wengineo hadithi iliyonyooka kisha akasikia kutoka kwa watu waovu kutoka kwa Shuuba na Malik, akapokea kutoka kwa wakweli waaminifu kwa uchakachuaji, yaani akawaangusha hawa waongo kati yake na wao (wakweli), basi haitolewi hoja hadithi yake.”

Na kwa hivyo inabainika kutokukubalika kwa maneno ya Abi Zur’at na wengineo hata kama yeye alipokea kutoka kwa mtu mweweli, bali yatosha kuwa yeye ni mtu wa Emas, na hadithi ya mtu wa Emas haichukuliwi hivi hivi.

Na anayetaka kujua maneno ya mahafidhi wa hadithi kuhusu hadithi ya mtu wa Emas basi aangalie kwa mfano vitabu vifuatavyo:- *Mustadrak*, Juz. 1, uk. 601, *Sunan Bayhaqi*, Juz. 4, uk. 302, *Sunan Abi Daud*, Juz. 2, uk. 321 /2423, *Sunan Nasaai Kubra*, Juz. 1, uk. 312, *Sharhu Maanil-Athaar*, Juz. 2, uk. 81, *Hashiyat Ibn Qayyim ala Abi Daud Maa Aunul-Ma’abuud*, Juz. 2, uk. 332 na Juz. 7, uk. 50, *Aunul-Ma’abuud*, Juz. 7, uk. 53, *Talkhiiswul-Habiir*, Juz. 2, uk. 216 na vinginevyo.

Kisha hakika matini haithibitishi kuonekana kwa Mwenyezi Mungu bali ndani yake kuna ukusho wa hilo!! Na kauli yake “mpaka mfe” haithibitishi hilo bali ndani yake inathibitisha zio mfano wa maneno ya Mola Manani “mpaka apite ngamia kwenye tundu la sindano”!! Nayo ni mionganoni mwa nyongeza za Zahri na ni mionganoni mwa kauli zake na juhudzi zake kama tulivyobainisha katika uwasilishaji wa nambari 17 wa Risala hii! Na sio maneno ya Mtume 8!! Na dhahiri hapa ni kwamba Baqiyya ndiye aliyeibuni na kuichomeka sentensi hii katika hadithi au Ziyad bin Abdu Rabbih kama tulivyobainisha hilo mwanzo wa maneno juu ya andiko hili!!

**Tanabahi:** Sheikh Shuaib Arnauut<sup>17</sup> hakubainisha katika utoaji wa maelezo yake na uelezaji wake juu ya kitabu *al-Awaswim Minal-Qawaswim*, Juz. 5, uk. 187 cha Ibn Waziir, kwamba Abu Daud amepokea hadithi bila ya lafudhi “Na nyinyi hamtamuna Mola Wenu Mlezi mpaka mfe” bali amenyamaza!! Na hili halifai kwa sababu katika kutaja utanabahisho huu kuna tamko la wazi kwamba lafudhi hiyo ambayo imemfanya Ibn Qayyim aitaje hadithi hii ni tegemezi!! Sijui kwa nini anafanya mfano wa mambo haya?! Je, ni kwa lengo la kueneza kitabu katika miji ya mabwana hawa au kwa malengo gani?!

### **Hadithi ya 35. Kisha Ibn Qayyim akasema:**

“Na ama hadithi ya mtu miongoni mwa Masahaba wa Mtume ﷺ, Swighani amesema: Ametuhadithia Ruuh bin Ubaada: ametusimulia Ubad bin Mansur amesema: Nilimsikia Uday ibn Artwaat akihutubia juu ya jukwaa sehemu inayoitwa Madain, akaanza kutoa mawaidha mpaka akalia na akatuuliza sisi...na hakika nilimsikia fulani ambaye Ubad amesahau jina lake, hakukuwa kati yangu na Mtume ﷺ mtu mwingine, akasema: Hakika Mtume ﷺ amesema: “Hakika Mwenyezi Mungu ana Malaika hutia hofu wapinzani wao kutokana na hofu yake.... Na itakapofika Siku ya Kiyama Mola Wao Mlezi atajidhihirisha kwao basi watamuangalia Yeye, watasema: Utakasifu ni Wako hatujakuabudu kama inavyopaswa kukuabudu wewe.”

Ameipokea Abu Sheikh katika kitabu *Udhmat*, Juz. 3, uk. 993 na 515 kama ilivyo, yaani bila ya kisa cha kwanza. Akasema mtoaji maelezo huko: hakika hiyo imepokewa kutoka kwa Abdullah bin Amru bin Aswi kwa sanad sahihi, naye ni miongoni mwa wale am-bao walikuwa wakiangalia ndani ya vitabu vyatatu. Kama alivypo-okea Khatwib Baghadt katika kitabu chake *Tariikh* Juz. 12, uk. 306.

<sup>17</sup> Yeye akiwa ni mtoaji wa hadithi.

Na kwa maana hii ni kwamba kisa hiki ni cha Kiyahudi. Na kauli yake “nilimsikia fulani ambaye Ubad amesahau jina lake” kama msemaji wa kauli hiyo ni Ubad mwenyewe basi huu ni uongo wa wazi!! Alaai amesema katika kitabu *Jaamiul-Tafswiil fi Ahkaamil-Maraasiil* uk. 206: “Amemtaja Ibn Madini katika wale ambao havakustahili kuwa miongoni mwa Masahaba.” Na sanad ya kisa hiki ni dhaifu kwani Ubad bin Mansur ni dhaifu kama unavyokuta katika wasifu wake katika *Tahdhiibul-Tahdhiib*, Juz. 5, uk. 90. Na Sheikh wake Uday bin Artwaat ni mtu wa Sham Damascus anapokea kutoka kwa Abi Amamat na kutoka kwa mwingine, na Ibn Hajar katika kitabu *Taqriib* amemhesabu miongoni mwa wale wenye kukubaliwa!! Na maana ya hivyo ni kwamba kwake yeye haitolei hoja hadithi yake ila kwa kufuatia. Na amemtaja Ibn Haban katika kitabu *Thuqaat*, Juz. 5, uk. 271 na kasema: “Anapokea hadithi zisizo na mlolongo kamili wa wapokezi.”

Na Daru Qutni amebainisha kwamba yeye anatolea hoja hadithi zake kutoka kwa Amru bin Abasat. Kama ilivyo katika wasifu wake katika kitabu *Tahdhiibul-Kamaal*, Juz. 19, uk. 521. Na hadithi hii imeshatangulia katika Risala hii katika andiko nambari 30, zaidi ya hapo ni miongoni mwa hadithi za Kiyahudi zilizolezwa kutoka kwa Abdullah bin Amru bin Aswi, nayo ni yenye kurudishwa na kukataliwa kwetu sisi.

Na kwa hivyo imebainika kwetu kutokana na uwasilishaji huu wa hadithi ya kumuona Mwenyezi Mungu kwamba si Hadithi mutawatiri kama wanavyodhani baadhi ya watu. Na kauli ishindayo ni kwamba hii ni hadithi iliyobuniwa au potofu au dhaifu, haikubaliwi katika masuala ya kifikihi na milango ya tohara bali wala katika fadhila za matendo na kuvutia na kutisha na kuogopesha. Itakuwaje sasa katika itikadi na katika dhati ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) aliyetukuka kuileta picha ya mwili, uso, mawazo, umbo na sehemu.

Na mwenye kuifikiria na kuitadaburi Qur'ani tukufu ambayo hajijiwi na batili mbele yake na nyuma yake atakuta ombi la kutaka kumuona Mwenyezi Mungu halikutajwa ndani ya Qur'ani ila kwa kulaumu, na kwa mantiki hiyo Mola Manani (s.w.t) anasema: "Wanakuuliza watu wa kitabu wanakutaka uwateremshie kitabu kutoka mbinguni. Hakika walimuomba Musa makubwa kuliko hayo wakasema: Tuoneshe Mwenyezi Mungu wazi wazi, ikawashika ngurumo (ya radi) kwa sababu ya dhuluma yao....." 4:153.

Na kauli yake (s.w.t): "Na wakasema wale wasiotaraji kukutana nasi, mbona sisi hatuteremshiwi Malaika, au kumuona Mola Wetu? Bila shaka wamejituza katika nafsi zao na wameasi uasi mkubwa." 25:21.

### **Uchambuzi wa Hadithi Isemayo: "Ewe Ambaye Macho Hayamuoni."**

Amepokea Tabarani katika kitabu *Mujamul Awsat*, Juz. 9, uk. 172, kutoka kwa Anas bin Malik ﷺ kwamba Bwana Mtume ﷺ alipita kwa mwarabu mmoja naye akiwa akiomba katika Swala yake akisema: "Ewe ambaye macho hayamuoni, wala dhana hazichanganyiki naye, wala hasifiwi na wasifiaji wala habadilishwi na matukio wala haogopi misukosuko ya zama, anajua uzito wa majabali na kiwango cha bahari, na idadi ya matone ya mvua, na idadi ya majani ya miti, na idadi ya yaliyofunikwa na giza la usiku na kuchomokewa na mchana, wala hazivichiki kwake mbingu wala ardhi wala bahari na kile kilichopo ndani ya kina chake, wala jabali na vilivyomo ndani yake, ufanye umri wangu wa mwisho kuwa wa kheri, amali yangu ya mwisho kuwa ya kheri, na siku yangu nzuri iwe ni ile siku nitakayokutana Nawe." Basi Mtume ﷺ akamtumia mtu; akasema: "Utakapomala kuswali mlete kwangu."

Alipomaliza kuswali alimpeleka kwa Mtume, na hakika Mtume alikuwa amepelekewa zawadi ya dhahabu kutokana na baadhi

ya madini, na pindi yule bedui alipofika kwa Mtume, Mtume al-impatia dhahabu akasema: “Ewe mwarabu unatokana na ukoo gani?” Akasema: “Ewe Mtume, ninatokana na ukoo wa Aamir bin Swa’aswa’at.” Akamuuliza: “Je, unajua kwa nini nimekuzawadia dhahabu?” Akasema: “Ni kutokana na undugu uliopo kati yetu na wewe Mtume.” Akasema: “Hakika undugu ni kweli, lakini nimekuzawadia dhahabu kutokana na usifiaji wako mzuri juu ya Mwenyezi Mungu.”

Hafidh Haythami katika kitabu *Majmau Zawaaid*, Juz.10, uk. 158, amesema: “Ameipokea Twabarani katika kitabu *Awsat* na wapokezi wake ni sahihi isipokuwa Abdullah bin Muhammad Abu Abdul-Rahman Adhrami naye ni mkweli.” Na amekubali usahihi wake Al-lamah mwanahadidhi Damiiri katika kitabu *Hayatul-Hayawan Kubra*, Juz. 2, uk. 95 katika mada ya “ndege.” Na hadithi inajulisha juu ya kutoonekana kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t).

### **Yaliyopokewa Katika Qur’ani Tukufu Kuhusu Suala la Kuonekana Kwa Mwenyezi Mungu**

Mwenyezi Mungu akurehemu, jua kwamba haifai kufupisha mtazamo katika suala lolote lile la kisheria kwa kukomea tu katika Sunna na hadithi kabla ya kuwa na mtazamo wa kina wa Qur’ani, kwani Qur’ani ndiyo asili ya kisheria ya awali ambayo inapasa kuwa chimbuko na asili ya fikra pale anapotaka binadamu mhusika kujua hukumu katika suala lolote la kisheria.

Na katika makosa makubwa ambayo baadhi ya watu wanay-atenda leo ni kwamba hakika wao wanapotaka kuangalia suala lolote la kisheria, akili zao na mawazo yao hukimbilia kwanza katika sunna na hadithi! Na huenda wakapuuzia uangaliaji na utafiti katika Qur’ani tukufu! Wala hawajui yaliyomo katika Qur’ani tukufu mionganoni mwa Aya mbalimbali zenyе kufungamana na suala husika.

La kwanza ambalo mtu hulisema: Katika suala hili kuna hadithi is-emayo.....

Ni wajibu kubadili mfumo wa kufikiri kwetu, ambapo ni lazima kuangalia kwanza ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kisha katika Sunna. Na baadhi ya watu wanasesma kauli hii lakini wao hawaitendei kazi, tunawaona wanachukua hadithi mbovu zenyekukataliwa au yenye kuchukiza na wanaacha andiko la Aya ya wazi. Kwa mfano katika suala la uokovu wa wazazi wa kipenzi na mteule bwana wetu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, wao katika suala hili wanategemea hadithi mbovu zenyekurudishwa au zenyekuchukiza zenyekuonesha kwamba hao wawili hawatosalimika na kuokoka, na wanaziacha aya tukufu zenyekujulisha kwa kukata shauri juu ya kuokoka kwao.<sup>18</sup>

Na juu ya hili haifai kusemwa: Wewe sasa hivi unasesma kwa rai ya Muutazilah au Khawaarij au mfano wa maneno hayo, kwani zingatio ni dalili na hoja ya kisheria, sio kwa kauli ya fulani, basi wale ambao wanataka kufikia haki kutoka kwa watu wa elimu wanaangalia katika suala lolote kwa upande wa dalili zake na sio upande wa yule anayesema jambo hilo, hivyo huifanyia kazi kanuni iliyomashuhuri isemayo: “Ijue haki utawajua watu wake” na haki haijulikani kwa kupitia watu, kwa hivyo haki haijulikani kwa kuwakundi hili au kundi lile linasema hivi, na hakika inajulikana kwa kusihiki kwa dalili. Kamwe haitotuzuia sisi kusema pindi tuonapo usahihi wa dalili, sawa wasemao haki hiyo ni Ibaadhi, au Muutazilah au

<sup>18</sup> Nayo ni kauli yake (s.w.t): “Ili uwaonye watu wasiofikiwa na muonyaji kabla yako, na huenda wakakumbuka.” 20:46 na huu ni uwazi katika watu wa Makka ambao alitumwa kwao bwana wetu Mtume ﷺ na kutoka kwake ni baba zake na mababu zake, pamoa na kauli yake (s.w.t): “”Na wala sisi hatuadhibu mpaka tupeleke mtume” 17:15 pamoa na kauli yake (s.w.t): “Na hakuwa Mola Wako mlezi mwenye kuiangamiza miji kwa dhuluma na hali wenyewe wameghafilika” 6:131 Na Hafidh Suyuutwi ana Risala tisa katika kadhia hii ili kuthibitisha kuongoka kwa wazazi wawili watukufu wa bwana Mtume ﷺ.

Zaydiyya au Shia Imamiyya au Jahamiyya au Dhahiriyya au wasio-kuwa hao! Kwani wale watu wenye kusema sisi tunawafuata baba zetu wamekataliwa kisheria, na hilo limetajwa kwa kalamu ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu anasema: “Bali walisema hakika sisi tuliwakuta baba zetu juu ya desturi na tunafuata nyayo zao.”(43: 22).

Na kutoka hapa tunaelekea kwenye Aya za Qur’ani zenyе kufungamana na suala la kuonekana kwa Mwenyezi Mungu au ambazo wamezitolea hoja kwazo wale wenye kuthibitisha kuonekana kwa Mwenyezi Mungu au kutoonekana kwake, na Mwenyezi Mungu ndiye Mwezeshaji:

- 1. Aya ya 1:** Aya ya kwanza katika maudhui hii, Mwenyezi Mungu (s.w.t) anasema:

وُجُوهٌ يَوْمَئِنَ نَاضِرَةٌ إِلَىٰ رَبِّهَا نَاظِرَةٌ وَوُجُوهٌ يَوْمَئِنَ بَاسِرَةٌ تَظُنُّ أَنْ يُفْعَلَ بِهَا  
فَاقِرَةٌ

“Nyuso siku hiyo zitang’aa zikingoja malipo kwa Mola Wao. Na nyuso (nyingine) siku hiyo zitakunjamana. Zitajua kuwa zitafikiwa na msiba uvunjao uti wa mgongo.” (75:22-25).

Aya hii “Nyuso siku hiyo zitang’aa zikingoja malipo kwa Mola wao.” inaelezea nyuso za watu katika ardhi ya ufufuo kabla ya kuingia peponi na motoni! Na kuonekana kwa wale wenye kuthibitisha hilo mionganoni mwa watu wa kutakasa kama vile Ashairah, ni kwa watu wa peponi ndani ya pepo, takrima kutoka kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) na ufadhilisho, kwa dalili waliyoitoa ambayo ni Aya hii: “Wale walifanya wema watapata wema na ziada” basi wema kwao ni pepo na ziada ni kumwangalia Mwenyezi Mungu (s.w.t).

Hivyo basi ikiwa mahala pa kumwangalia ni peponi, na makafiri na wanafiki na watu wa maasi wamezuiwa kumuona Yeye (s.w.t) kama wanavyosema Ashairah wengi,<sup>19</sup> na Aya hii hakika inaelezea hali za watu katika ardhi ya ufufuo kabla ya kuingia peponi na motoni, basi maana ya neno “*Naadhirat*” lililopo kwenye Aya haitakuwa ni kuona wanakokukusudia, bali maana ya Aya itakuwa ni: Nyuso zitang’ara zitakuwa na furaha kwa sababu zinangojea thawabu za Mola Wao na kupewa pepo na kuneemeshwa, kama ulivyo mkabala wa hilo nyingine “Nyuso siku hiyo zitakunjamana, zikijua kuwa zitavunjwa uti wa mgongo,” yaani zikipatwa na huzuni kubwa.

Na maneno haya ni ubainifu wa jinsi itakavyokuwa katika ardhi ya ufufuo na hali ya waumini na makafiri siku hiyo, na kuonekana kutakuwa peponi. Hivyo hapa ni mahala pa mkabala baina ya nyuso ambazo zinangojea thawabu na nyuso ambazo zinangojea adhabu, na suala la kuonekana kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) sio makusudio yake hapa, hususan hakika maneno yanafungamana na kisimamo kabla ya kuingia peponi au motoni.

Kisha Aya za Qur’ani zinahitimisha kwa maneno yake: “Nyuso siku hiyo zitajua kuwa zitafikiwa na kuvunjwa uti wa mgongo” na ni lini nyuso zikawa na dhana? Na nyuso kwa kawaida hazidhani wala kujua! Hakika nyoyo ndizo zinazodhani na kujua na mtu kwa ukamilifu wake! Basi inakuwa wazi kwamba sio makusudio yake nyuso wala macho! Bali dhati ndizo ambazo zinangojea, kudhani na kujua!!

Na uangaliali haunasibishwi na nyuso, hakika hunasibishwa na macho, na uso unajulisha juu ya dhati na sio juu ya jicho. Na watu wamedhani kwamba lafudhi “*Naadhirat*” katika lugha ya Kiarabu

<sup>19</sup> Na hakika amenukuu kwa makubaliano juu ya hilo Hafidh Abu Bakar bin Arabi Ma’lik katika kitabu *Aaridhat Ahwadhi Sharhu Tirmidhi*, Juz. 10 uk. 23 wakati wa kutoa maelezo ya hadithi ya sura, na akanukuu hilo kutoka kwa Imam Muhadithi Kawthari  katika mstari wa pambizo juu ya kitabu *As-maa’u wa Sifaaat cha Bayhaqi*.

halileti maana ya *muntadhirah*, na wamejibiwa na wale wenye kukanusha kuwa kauli yao hiyo ni kosa! Kwa sababu lafudhi hiyo huwa inakuja kwa maana ya *muntadhirat* katika lugha ni kosa! Hakika imekuja hivyo katika Qur'ani tukufu katika kauli Yake (s.w.t):

وَإِنِّي مُرْسِلٌ إِلَيْهِم بِهَدِيَّةٍ فَنَاظِرُهُم بِمَا يَرْجِعُ الْمُرْسَلُونَ

**“Na hakika mimi ni ninawapelekea zawadi, nami nitangoja watakay-orudi nayo wajumbe.”** (27:35), yaani mwenye kungojea yale watakay-orudi nayo wajumbe.

Na pindi baadhi ya watu walipoona hili wakadhani kwamba *naadhirat* linapoungana au kupokea herufi “ilaa” maana yake huwa finyu kwa kumaanisha kuangalia kwenye kumaanisha kuona kuliko maarufu! Na kanuni hii iliyobuniwa haina msingi wowote katika lugha ya Kiarabu. Hakika imebuniwa tu na baadhi ya watu ili wam-changanye yule ambaye hajui lugha ili kuhalalisha madhehebu yao. Na mionganoni mwa yale yanayobatilisha hilo ni kaswida waliyoimba:

وجوه يوم بدر نظارات إلى الرحمن يأتي بالخلاص

**“Nyuso siku ya Badr zikiangalia kumwelekea Rahman, atakuja kwa umaliziaji.”**

Na Raazi amesema katika *Tafsiri* yake Juz. 30, uk. 299, na riwaya ni sahihi:

وجوه نظارات يوم بدر إلى الرحمن تنتظر الخلاص

**“Nyuso zitaangalia siku ya Badri kumwelekea Rahman zikingojea malipo.”**

Na kwa hali yoyote ile hizo zinafaidisha ungojeaji na mazingatio,

na akasema Ibn Wazir katika kitabu *al-Awaswim Minal-Qawaswim*, Juz. 5, uk. 225-225: “Khalil amesema: Waarabu husema *Andhuru ilallah Taala Waila fulani min Baynil-Khalaiq*, yaani ninangojea kheri Zake, kisha kheri ya fulani.”

Kisha akasema: Hakika Sheikh wetu Abu Abdillah Baswary amejibu kwamba uangaliaji ikiwa kwa namna ya kugeuza mtoto wa jicho, sahihi hutumika neno *Ilaa*, vivyo hivyo kwa maana ya kungojea, na wala haizui kutumika (*Ilaa*) kwa sababu majaazi hufuata njia ya uhalisia.

Nyongeza ya dalili za kilugha inaonesha kwamba neno *Nadhar* hata kama litatamkwa pamoja na *Ilaa* bado humaanisha kungojea na si kuona:

Amesema Nabighat Dhubyaani mwandishi wa *Ihdaa Mua'alaqaatil-Ashra*:

**نَظَرْتُ إِلَيْكَ بِحَاجَةٍ لِمَ تَقْضِهَا، نَظَرَ السَّقِيمَ إِلَى وِجْهِ الْعَوْدِ**

“Nimengojea kwako haja ambayo hujaikidi, kama mgonjwa anavyongojea nyuso za wenge kumtembelea.”<sup>20</sup>

Yaani nimengojea kutoka kwako kukidhi haja yangu kama vile mgonjwa anavyongojea aone nyuso za watu wenye kumzuru na kumliwaza! Na akasema Hatwiat aliyekufa mwaka 45 A.H naye ni Muhdharam:

**فَمَا لَكَ عَيْرُ تَنْظَارٍ إِلَيْهَا كَمَا نَظَرَ الْفَقِيرُ إِلَى الْغَنِيِّ**

**“Basi kwa nini hungojei kama fukara anavyomngojea tajiri”**

Na maana yake: Ni kama fukara anavyongojea kukirimiwa na tajiri! Na liangalie hilo katika kitabu *Lisaanul-Arab*, Juz. 5, uk. 219.

<sup>20</sup> Angalia hiyo katika *Sharhu Diiwan Nabigha / kilichochapishwa na Daar Maktabat Hayaat Beirut* uk. 29.

Na akasema Jamiiil Buthaynat aliyekufa mwaka 82 A.H.

إِنِّي إِلَيْكَ لَمَا وَعَدْتُ لَنَا نَظَرٌ      نَظَرُ الْفَقِيرِ إِلَى الْغَنِيِّ الْمَكْثُورِ

**“Hakika mimi nangojea kwako uliloahidi, kama fukara anavyomngoeja tajiri mwenye mali nyangi.”**

Yaani nangojea utekelezaji wa ahadi Yako kama anavyongojea fukara kupewa na tajiri.

Na akasema Jarir aliyekufa mwaka 110 A.H:

من كل أبيض يستضاء بوجهه      نَظَرُ الْحَجَّاجِ إِلَى خَرْجِ هَلَالٍ

**“Kutokana na kila weupe wenyewe kuangaza kwa uso wake, Mahujaji walingojea kuchomoza kwa mwezi mwandamo.”**

Amesema Hafidh mwanalugha Abu Haban katika *Bahru Muhiit* kwenye Tafsir ya neno “*Naadhirat*” akinukuu kutoka kwa Zamakhshari; andiko lake:

Na kwa kuwa Zamakhshari ni mionganoni mwa Muutazila.... basi ambalo linasihi pamoja naye ni yeye kuwa mionganoni mwa maneno ya watu: ‘Mimi nangojea kuona fulani atanifanya nini’, akikusudia kutegemea na kutarajia, na hiyo ndio kauli ya msemajii:

وإِذَا نَظَرْتَ إِلَيْكَ مِنْ مَلَكٍ وَالْبَحْرُ دُونَكَ زَدْتِي نَعْمًا

**Ninapongojea ufalme ulionao, ambao hata bahari haikufikii, hali hiyo inanizidishia tamaa.**

عَيْنِتِي نَاظِرَةً إِلَى اللَّهِ وَإِلَيْكُمْ

**Macho yangu yanamtegemea Mwenyezi Mungu na ninyi.**

Na Ibn Utwiyat amesema: “Wanaona, yaani Muutazila, kwamba maana yake ni kuwa watangojea rehema za Mola Wao Mlezi, au thawabu au ufalme Wake. Hivyo wao wakakadiria uwepo wa neno lililoachwa, na kufanya hivyo ni jambo linalosihii katika lugha ya Kiarabu, kama vile unaposema: Fulani anakungojea wewe kwa kitu kadha; yaani katika utengenezaji wako wa kitu kadha.”

Na amekiri hilo Abu Haban, na hakika nimeeleza maneno yake na yale aliyoyanukuu katika kitabu chake kwa kuwa yeye ni imam mwandishi mwadilifu katika lugha. Hatoi maana kwa kutegemea maneno ya wafasiri, kwa sababu wafasiri wanafasiri Qur’ani kwa kujengea juu ya madhehebu yao na kinyume chake.

Na mionganini mwa yale yanayoonesha kwamba hata kama kitendwa kitapatikana kwa *Ilaa bado halitamaanisha kuonekana*, ni kauli yake Mola Manani: “Je, hujamuona Mola Wako vipi ametandaza kivuli.” Makusudio hapa si kumuona kwa macho bali ni kutafakari na kutaamali. Hivyo makusudio ya “Je, hujamuona Mola Wako” si kumuona kwa macho, kama ambavyo makusudio ya “*Ilaa Rabih Nadhirah*” si kumuona kwa macho, bali makusudio yake ni kama tulivyotaja; ni kutaraji na kungojea, na hasa ukizingatia kwamba Aya iliyotumika kama dalili na ambayo ndiyo yenyenye mzozo, inafuatiwa na Aya nyingine inayonasibisha dhana kwa nyuso ilihali makusudio ni dhati. Na makusudio katika hali zote mbili ni dhati kwa majazi, na wala hakuna dalili ya kukata shauri juu ya kwamba makusudio ya kwanza ni halisi na katika Aya nyingine ni majazi. Hasa ukizingatia uwepo wa Aya zenye kujulisha kwamba kuomba kumuona Mungu ni jambo ninalokemewa na linalochukiwa, na hakika Mwenyezi Mungu amesema: “Macho hayamdiriki Yeye.”

Na kauli yake: “Hawamzungumzishi Mwenyezi Mungu wala hawaangalii wao Siku ya Kiyama” makusudio si wao kumuona Mwenyezi Mungu, bali hakika Mwenyezi Mungu ndiye mwenye

kuwaona wao katika kila hali! Na amesema: “Na mionganini mwao yupo yule anayekuangalia wewe je, wewe unamuongoza kipofu hata kama hawaoni.” Na kauli Yake: “Je, wanaangalia ila wawajie wao malaika au awajie Mola Wako Mlezi” na mfano wa kauli ya Mola Muweza: “Je, wanaangalia ila taawili yake,” na nyingine nyingi!

Na katika kitabu *Lisaanul-Arab*, Juz. 5, uk. 215: “Unasema: ‘*Nadhartu Ilaa Kadhaa Wakadhaa*,’ kwa maana ya kutazama kwa jicho na kwa moyo. Na mwenye kutaraji kitu naye husema: ‘*Innama Nandhuru Ilallah Thumma Ilayka*.’ yaani hakika ninategemea fadhila za Mwenyezi Mungu kisha fadhila zako.” Na pia katika kitabu *Lisaanul-Arab*, Juz. 13, uk. 401: “Unasema: ‘*Imtahantuhu Wamntahantul-Kalimah*’ yaani nangojea na kuona atakuwa na hali gani.”

Yote hayo yanabomoa kanuni yao waliyojiwekea, ya kwamba kama kitendwa kitapatiwana kwa *Ilaa italazimu* kuwa na maana ya kuona kwa macho, nayo ni kauli ya Abu Mansur kama ilivyokuja katika kitabu *Lisaanul-Arab*: “Ukisema: ‘*Nadhartu Ilayhi*’ basi haitakuwa ila kwa jicho.” Maneno haya ni batili na ni wenye kujataliwa, ni kama maneno ya Ibn Arabi katika Aya *Isti'wai*, aliposema kuwa haifai kuifasiri hiyo kwa maana ya utawala!! Nayo ni kati ya madai yaliyobuniwa ya batili katika Kiarabu, na ni kutoka kwa Abu Mansur huyu imechukuliwa kanuni hii ambayo kiukweli ni uzushi batili!

Raghib katika kitabu *Mufradat* amesema: “*Ilaa Twaaami Ghayri Nadhirina Inahu*, yaani ni wenye kukingojea.” Na maana yake si kuwa ni wenye kujitazama chombo, bali maana yake ni wenye kukingojea.

Na kauli ya mshairi:

نَظَرَ الدَّهْرُ إِلَيْهِمْ فَابْتَهَلَ

**Ni utanabahisho kwamba ye ye amewafanya hiyana wao, hatimaye akawaangamiza.**

Na baada ya ubainifu huu tunasema: Kwa uchache Aya hii si yenye kukata shauri juu ya suala hili bali hiyo ni dhana, na itikadi haijengwi ila juu ya yakini.

**Kauli za Wanazuoni Miongoni Mwa Ahlus-Sunnah  
na Wengineo, Ambao Hawathibitishi Suala la  
Kumuona Mwenyezi Mungu Wala Hawasemi Hivyo.**

Amedai Sheikh Abdul-Qahir Baghdaadi katika kitabu *Al-Farqu Baynal-Firaq*, uk. 335, kuwa kuna Ijmai ya Ahlu Sunna kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) ataonekana Akhera. Lakini ukweli ni kinyume na hivyo kwani Ahlu Sunna wametofautiana katika hilo.

Wamesema wafasiri kama vile Qurtub, Juz. 19, uk. 107, na Razi Juz. 30, uk. 226, na hii ndiyo lafudhi ya Fahkru Razi: "Jua kwamba jamhuri ya Ahlu Sunna wanashikamana na Aya hii kuhhibitisha kuwa waumini watamuona Mwenyezi Mungu (s.w.t) Siku ya Kiyama, lakini hakika wamebainisha wafasiri kwamba suala hili si Ijmai ya Ahlu Sunna, na hakika hiyo ni kauli ya wengi wao. Zaydiyya, Imamiyya, Ibaadhi, Muutazilah, maimamu wa Ahlul-Bayt katika karne za mwanzo, Bibi Aisha  na baadhi ya maimamu wa Ahlu Sunna kama vile Abu Salih Salman mwanafunzi wa Abu

Huraira, Mujahid, Akrama,<sup>21</sup> Bashar bin Saray Afuhu,<sup>22</sup> na Yahya bin Saleh Wahdhi<sup>23</sup> na wengineo kama vile Jaswas na Imam Abu Hanifa  na Imam Ghazali S, wote hao wanaona kwamba hakika Mwenyezi Mungu haonekani duniani na wala Akhera.”

Na amesema Ibn Taymiyya Harrani katika *Majmaul-Fataawa*, Juz. 20, uk. 33-34: [Faslu: Na kosa lenye kusamehewa katika ijtiha-di...kama vile..... aliyeitakidi kwamba hakika Mwenyezi Mungu haonekani; kwa kauli yake: ‘Hayatomuona yeye macho’ na kauli yake: ‘Na haikuwa kwa Mwenyezi Mungu aseme na kiumbe ila kwa njia ya ufunuo au nyuma ya pazia’ kama alivyotoa hoja Aisha kwa aya hizi mbili akikanusha Mtume ﷺ kumuona Mwenyezi Mungu, na hakika zinajulisha hivyo kwa njia ya ujumla, na kama alivyonukuliwa kutoka kwa baadhi ya vizazi vilivyokuja baada ya Masahaba kwamba Mwenyezi Mungu haonekani, na wakafasiri kauli yake:

إِلَىٰ رَبِّهَا نَاظِرَةٌ

وُجُوهٌ يَوْمَئِنْ نَاضِرَةٌ

**Nyuso siku hiyo zitang’ara. Zinamtazama Mola wako.**  
**(Surat Al-Qiyama 75: 22-23)**

kwamba ni kungojea thawabu za Mola Wake Mlezi, kama ili-yonukuliwa kutoka kwa Mujahid na Abi Saleh].

<sup>21</sup> Kama alivyonukuu hilo kutoka kwa Mujahid na Abu Saleh Hafidh Ibn Jariir Twabari Salafi katika *Tafsir* yake Juz. 14, uk. 20 / 192-193 kwa sanad zake sahihi, na Hafidh Ibn Hajar katika kitabu *Al-Fat’hu* Juz. 13, uk. 425 kutoka kwa Akrama, na Bukhari na Muslim kutoka kwa Bibi Bi. Aisha  kama inavyojulikana. Kama alivyonukuu hilo kutoka kwa Mujahid na Abu Saleh Hafidh Ibn Jariir Tabari Salafi katika *Tafsir* yake Juz. 14, uk. 20 / 192-193 kwa sanad zake sahihi.

<sup>22</sup> Naye ni mionganoni mwa wapokezi wa Sunna. Wasifu wake umo katika kitabu *Tahdhibul-Tahdhib* Juz. 1, uk. 394 cha Hafidh ibn Hajar.

<sup>23</sup> Naye ni mionganoni mwa Maimamu wa Kisunni wakweli na mionganoni mwa watu wa Bukhari na Muslim na wengineo, wasifu wake umo katika kitabu *Tahdhibul-Kamaal* Juz. 31, uk. 379 cha Hafidh Mazzi.

**Aya ya 2:** Aya ya pili katika maudhui hii ni maneno ya Mola Muweza: “Si hivyo hakika wao kutohana na Mola Wao Mlezi siku hiyo watazuiwa.” Na inategemewa kuwa wao watazuiwa kupata thawabu Zake, ukarimu na utukufu Wake na pepo Yake, au kutoongea naye kama yasemavyo maneno ya Mola Manani (s.w.t):

وَلَا يُكَلِّمُهُمُ اللَّهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَلَا يُزَكِّيهِمْ

**“Wala Mwenyezi Mungu hatawasemesha hao Siku ya Kiyama wala hawatakasi.” (2:174).**

Basi wao kwa mujibu wa Aya hii wamezuiwa kupata rehemha Yake na utakaso Wake.

Na hakika Imam Ghazali katika kitabu *Mustaswfa* Juz. 2, uk. 192, amebatilisha utumiaji wa Aya hii kama hoja ya kuthibitisha kuonekana kwa Mwenyezi Mungu, aliposema huko: “Na Ashairah katika suala la kumuona Mwenyezi Mungu wameitumia Aya hii kama hoja: ‘Si hivyo hakika wao kutohana na Mola Wao Mlezi siku hiyo watazuiwa.’ Akasema: Na hili linajulisha kwamba waumini watakuwa tofauti na wao, na kundi la wanatheolojia akiwemo al-Qadhi na kundi la mafakihi bingwa, ikiwa ni pamoja na Ibn Surayju, wamesema hakika Aya hiyo haina dalili juu ya hilo, nayo ndiyo kauli yenyne nguvu zaidi kwetu, na inajulisha juu yake njia za kuelekea...”. Basi Aya hii sio dalili juu ya kuonekana kwa Mwenyezi Mungu, na hakuna ndani yake utajo wa kumuona Mungu, wala haisihi kabisa kuifanya dalili kutetea suala la kumuona Mwenyezi Mungu (s.w.t).

**Aya ya 3:** Aya ya tatu ambayo inafungamana na suala la kuonekana kwa Mwenyezi Mungu ni ombi la Nabii Musa ﷺ kwa Mwenyezi Mungu la kumtaka amuneshe nafsi yake, na kauli ya Mwenyezi Mungu kwake: “Hutaniona kamwe,” na aya kwa ukamilifu wake ni hii:

وَلَمَّا جَاءَ مُوسَىٰ لِمِيقَاتِنَا وَكَلَمَهُ رَبُّهُ قَالَ رَبِّيْ أَنْظُرْ إِلَيْكَ قَالَ لَنْ تَرَانِي  
وَلَكِنْ انْظُرْ إِلَى الْجَبَلِ فَإِنْ اسْتَقَرَ مَكَانَهُ فَسَوْفَ تَرَانِي قَدْمًا تَجْلَى رَبُّهُ لِلْجَبَلِ  
جَعَلَهُ دَكَّا وَخَرَّ مُوسَىٰ صَعِقًا فَلَمَّا أَفَاقَ قَالَ سُبْحَانَكَ تُبْتُ إِلَيْكَ وَأَنَا أَوَّلُ  
الْمُؤْمِنِينَ

**“Na alipofika Musa kwenye miadi yetu na Mola Wake akamsemesha, alisema: Mola Wangu nioneshe nikutazame. Akasema: Hutaniona kamwe, lakini tazama jabali, kama litakaa pahali pake ndipo utaniona. Basi Mola Wake alipojonesha kwa jabali, alilifanya lenye kuvunjika, na Musa akaanguka hali amezimia. Alipozinduka alisema: Utakatifu ni Kwako na mimi ni wa kwanza wa wanaoamini.” (7:143).**

Tamko “hutaniona kamwe” yaani Nabii Musa عليه السلام wala mtu mwiningine hatomuona Mwenyezi Mungu (s.w.t), hivyo ni aula kufungamana na kushikamana na maneno ya Mwenyezi Mungu (s.w.t): “Hutaniona kamwe” badala ya kushikamana na kauli ya Nabii wetu Musa عليه السلام: “Ewe Mola Wangu Mlezi nioneshe niweze kukuangalia Wewe,” hususan ukizingatia kwamba Nabii wetu Musa عليه السلام alitubia kauli hii pindi aliposema katika Aya hiyo hiyo: “Utakatifu ni Wako” yaani ninakutakasa na ninakuepusha Wewe na hilo “nimetubu Kwako na mimi ni wa mwanzo wa wanaoamini” yaani hakika Wewe huonekani.

Na neno ‘kamwe’ linafidisha (kumaanisha) milele na daima:

إِنَّ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ لَنْ يُخْلُقُوا دُبَابًا وَلَوْ اجْتَمَعُوا لَهُ مُطْهَّرٌ

**“.....Kwa hakika wale ambao mnaowaomba kinyume na Mwenyezi Mungu kamwe hawaumbi inzi hata wakikusanyika kwalo.....”**  
(22:73). Hii imefidisha kushindwa kwao kabisa kufanya hilo!

Na kuna mambo mawili yanayoizunguka Aya hii, ambayo inawezekana kuyatolea majibu, kwani baadhi ya watu wameyafanya kuwa ni hoja:

**Mosi:** Hakika bwana wetu Musa ﷺ aliomba kumuona Mwenyezi Mungu katika Aya hii mbele ya wana wa Israeli ambao aliwachagua ili kukutana na Mwenyezi Mungu aliyetukuka:

وَاخْتَارَ مُوسَى قَوْمَهُ سَبْعِينَ رَجُلًا لِمِيقَاتِنَا فَلَمَّا أَخْذَتِهِمُ الرَّجْفَةُ قَالَ رَبُّ لَوْ  
شِئْتَ أَهْلَكْتَهُمْ مِنْ قَبْلٍ وَإِبَأَيِّ صَانِعٍ لَكُنَا بِمَا فَعَلَ السُّفَهَاءُ مِنَّا

“Na Musa akachagua watu sabini katika kaumu yake kwa miadi yetu. Lilipowashika tetemeko alisema: Mola Wangu! Lau ungetaka ungelilaangamiza wao na mimi zamani. Unatuangamiza kwa sababu ya yale waliyoyafanya wajinga katika sisi?...” (7:155).

Nayo ipo katika fuo hilo la kisa cha kuomba kumuona Mwenyezi Mungu, na kwa hivyo amesema Imam Razi katika *Tafsir* yake Juz. 8, uk. 15 na 20, wakati wa kutafsiri maneno ya Mola Manani: “Na akawachagua Musa wanaume sabini katika watu wake ili akutane nasi...”: “Na linalohusu zaidi ufasaha ni kutimiza maneno katika kisa kimoja katika nafasi mmoja, kisha kuhama kutoka kisa hicho kwenda kisa kingine baada ya kukitimiza. Ama kutaja sehemu ya kisa kisha kuhamia kisa kingine, kisha kuhama kutoka kisa cha pili baada ya ukamilifu wake kwenda kwenye kukamilisha kisa cha kwanza, hakika hali hiyo inawajibisha aina fulani ya mporomoko na utata, hivyo ni bora kuyalinda maneno ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) na sifa hiyo.”

Na hili linafidisha kwamba Nabii Musa ﷺ aliomba kutoka kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) mbele ya watu wake wamuone ili ifahamu kaumu yake kwamba hakika Mwenyezi Mungu haonekani, na kumuona Mwenyezi Mungu (s.w.t) ni muhali, na hakika walisema: “Tuneshe Mwenyezi Mungu wazi wazi,” naye hakuwa amemaanisha hasa kutaka kumuona aliposema “Ewe Mola Wangu Mlezi, nioneshe

nikuangalie Wewe,” kama vile ambavyo Nabii wetu Ibrahim ﷺ hakuwa amemaanisha hasa kwamba nyota na mwezi ni miungu pale aliposema: “Huyu ndiye Mola Wangu Mlezi,” hakukusudia uungu wa sayari hizo mbili. Na hakika kila mmoja kati ya Manabii hao wawili alikusudia kuwaelewesha watu wake kwamba jambo husika ni muhali na haliko hivyo mnavyofikiria.

**Pili.** Je, Mitume ﷺ humuomba Mwenyezi Mungu kitu amba-cho hakifai au muhali? Na uhakika ni kwamba bwana wetu Nabii Nuhu ﷺ alimuomba Mwenyezi Mungu jambo na Mwenyezi Mungu akamwambia: “Ewe Nuhu hakika huyo sio katika watu wako...” (11:46). Na bwana wetu Ibrahim ﷺ alimuomba Mwenyezi Mungu amuoneshe namna gani anaafufua maiti, na kwa kuwa suala hilo likuwa linawezekana ambapo ni tofauti na suala la kumuona Yeye, Mwenyezi Mungu alimuonesha hilo, vivyo hivyo ombi la bwana wetu Nabii Isa ﷺ kuteremshiwa meza ya chakula kutoka mbinguni ni suala lilolokuwa lawezekana na hivyo hakika lilitokea.

مَا كَانَ لِلنَّبِيِّ وَالَّذِينَ آمَنُوا أَنْ يَسْتَغْفِرُوا لِلْمُشْرِكِينَ وَلَوْ كَانُوا أُولَئِي قُرْبَىٰ مِنْ  
بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمْ أَنَّهُمْ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ

**“Haimfai Mtume na wale walioamini kuwatachia msamaha washirikina na ijapokuwa ni jamaa. Baada ya kuwabainikia kuwa ni watu wa motoni.” (9:113).**

Na suala hili ni mionganoni mwa mambo bayana ya kiti kadi am-bayo Mitume wote wanayajua, kwamba washirikina Mwenyezi Mungu hawasamehi na wala hawaingizi peponi. Na pamoja na hivyo Mtume alikuwa halijui hilo na hivyo Mwenyezi Mungu akamfundisha yeye na akamkataza kutokana na kile alichokifanya kinyume na hivyo, akasema (s.w.t): “Na akakufundisha yale uliyokuwa huy-ajui...” (4:113). Na hakika bwana wetu Nabii Ibrahim ﷺ alim-

uomba Mwenyezi Mungu (s.w.t) amsamehe baba yake, Mwenyezi Mungu amesema:

قَدْ كَانَتْ لَكُمْ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ فِي إِبْرَاهِيمَ وَالَّذِينَ مَعَهُ إِذْ قَالُوا لِقَوْمِهِمْ إِنَّا بُرَآءٌ مِّنْكُمْ  
وَمِمَّا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ كَفَرْنَا بِكُمْ وَبَدَا بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمُ الْعَدَاوَةُ وَالْبُغْضَاءُ أَبْدَا  
حَتَّىٰ تُؤْمِنُوا بِاللَّهِ وَحْدَهُ إِلَّا قَوْلُ إِبْرَاهِيمَ لِأَبِيهِ لَا سَتَعْفَرَنَّ لَكَ وَمَا أَمْلَأُ لَكَ مِنَ  
اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ ۖ رَبَّنَا عَلَيْكَ تَوَكَّلْنَا وَإِلَيْكَ أَتَبْنَا وَإِلَيْكَ الْمَصِيرُ

**“Hakika nyinyi mna kigezo kizuri kwa Ibrahim na wale waliokuwa pamoja naye, walipowaambia watu wao: Hakika sisi tumejiten-ga nanyi na hayo mnayoyaabudu badala ya Mwenyezi Mungu. Tunawakataa; na umekwisha kudhihiri uadui na chuki baina yetu na nyinyi mpaka mtakapomwamini Mwenyezi Mungu peke Yake. Isipokuwa kauli ya Ibrahim kumwambia baba yake: Hakika ni-takuombea maghfira; wala similiki chochote kwa ajili yako mbele ya Mwenyezi Mungu. Mola Wetu! Juu Yako tumetegemea, na Kwako tumerudi, na Kwako ndio marejeo.” (60:4).**

Na mionganini mwa maneno mazuri aliyoyanukuu Imam Razi kuhusiana na suala hili ni maneno yake katika *Tafsir* yake Juz. 7, uk. 14 na 238 katika kutafsiri kauli yake (s.w.t): ‘Ewe Mola Wangu Mlezi nioneshe nikuangalie wewe, akasema hutania kamwe’: “Al-Qadhi amesema: Waliyoyasema wanazuoni katika hilo ni kauli nne:

**Ya kwanza:** Ni aliyoyasema Hasan na wengineo<sup>24</sup> kwamba hakika Musa ﷺ hakujuu kuwa suala la kuonekana Mwenyezi Mungu ni jambo lisiloruhusiwa juu ya Mwenyezi Mungu (s.w.t). Akasema: Pamoja na ujinga wa maana hii bado mtu anaweza kuwa mwenye maarifa na Mola Wake na uadilifu wake na tawhiid yake, haiko

<sup>24</sup> Na hili linafidisha kwamba hakika kauli hii ni mashuhuri kwa masalafi, na ambalo amelijaja Raazi baada yake hakika hili ni tija inayopatikana yenye kunukuliwa kutoka kwa Muutazila katika aya hii hayatudhuru sisi chochote.

mbali kuwa kujua kuwa ni muhali Mungu kuonekana au si muhali, kunategemea ufunuo.

**Ya pili:** Hakika Musa ﷺ aliomba kumuona Mwenyezi Mungu kwa ulimi wa watu wake. Hakika walikuwa wajinga kwa hilo wa-kirudufu suala hilo juu yake wakisema: “Hatutokuamini wewe kamwe hadi tumuone Mwenyezi Mungu wazi wazi,” basi akaomba Musa suala la kumuona Mwenyezi Mungu, na si kwa ajili yake yeye mwenyewe. Na pindi lilipopatikana zuio juu ya hilo, ikadhihirika kwamba hakuna njia ya kuwezekana hilo, na hii ni njia ya Abu Ali na Abu Hashim.

**Ya tatu:** Hakika Musa ﷺ alimuomba Mola Wake Mlezi maarifa ya ajabu kwa dharura, na wenye kutoa maelezo haya ni wenye kutofautiana, mionganini mwao yupo mwenye kusema: Alimuomba Mola Wake Mlezi maarifa ya dharura. Na mionganini mwao yupo mwenye kusema; bali alimuomba Yeye kudhihirisha miujiza ya maajabu wakati wa kuteremka mambo ya hatari na wasiwasi kuto-kana na maarifa yake hata ikiwa kutokana na kitendo chake, kama tunavyosema kuhusiana na maarifa ya watu wa akhera, na hilo ndilo alilolichagua Abu Qasim Ka’abi.

**Ya nne:** Makusudio kutokana na swali hili ni kumtaka Mwenyezi Mungu (s.w.t) ataje dalili za kusikia ambazo zinajulisha juu ya zuio la kuonekana Kwake, ili dalili ya kiakili itiliwe nguvu na dalili ya kusikia. Na kuungana dalili ni jambo lenye kutakiwa kwa wenye akili, nalo ni lile ambalo alilolitaja Abu Bakri Aswim.” Maneno ya Fakhru Razi yamekwisha.

Na kwa hiyo imebainika kwamba Aya ni dalili ya kutoonekana kwa Mwenyezi Mungu, na si dalili juu ya kuonekana kwa Mola Mwanani, kwani kiini cha hoja ni kauli Yake (s.w.t) “Hutaniona kamwe.”

Na itakuwaje hiyo iwe ni dalili juu ya kuonekana kwa Mola Muweza? Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwezeshaji.

**Aya ya 4:** Aya ya nne ambayo baadhi ya watu wameifanya dalili juu ya kuonekana kwa Mwenyezi Mungu ni kauli Yake (s.w.t):

لِلَّذِينَ أَحْسَنُوا الْحُسْنَى وَزِيَادَةً

**“Wale waliofanya wema watapata wema na ziada” (10:26).**

Aya hii haina uhusiano kabisa na suala la kuonekana kwa Mwenyezi Mungu, si uhusiano wa karibu wala wa mbali. Na hakika wamefasiri neno “ziada” kuwa ni kumuangalia Mwenyezi Mungu (s.w.t) kwa kutegemea hadithi isiyo sahihi. Na hakika tu-meshawasilisha hadithi husika hapo kabla katika uwasilishaji wa hadithi katika kitabu hiki, nayo ni hadithi nambari 4, hadithi ya Abu Layla kutoka kwa bwana wetu Suhaybu ﷺ, nayo si sahihi. Na maana ya ziada hapa ni ziada ya thawabu na ujira kwa zaidi ya yale waliyoyatenda, kama mnavyosema kumwambia mwajiriwa: “Nimekupa ujira wa kazi yako na ziada.” Na ndio kauli yake (s.w.t): “Atawapa wao ujira wao na atawazidishia kutohana na fadhila Zake” (35:30), na kauli yake (s.w.t): “Ili Mwenyezi Mungu awalipe mazuri ya yale waliyoyatenda, na awazidishie katika fadhila Zake...” (24:38).

**Aya ya 5:** Kauli ya Mwenyezi Mungu (s.w.t):

لَا تُدْرِكُهُ الْأَبْصَارُ وَهُوَ يُدْرِكُ الْأَبْصَارَ وَهُوَ اللَّطِيفُ الْخَبِيرُ

**“Hayamfikii macho; bali Yeye huyafikia macho. Naye ni Mpole Mwenye habari.” (6:103).**

Aya hii iko wazi katika kukanusha kumuona Mwenyezi Mungu duniani na akhera. Na baadhi ya watu wameifanya hiyo ni mionganini

mwa dalili zenyе kuthibitisha suala la kumuona Mwenyezi Mungu, na hili ni mionganoni mwa mambo ya ajabu ya kushangaza!

Na Aya hii inajumuisha duniani na akhera, na inamjumuisha Bwana Mtume ﷺ katika usiku wa Israi na Miraji pia. Na Bibi Aisha ؓ alikanusha kauli ya Ibn Abbas ﷺ ambayo ameinukuu kutoka kwa Kaab bin Akhbar kuhusiana na Bwana Mtume ﷺ kumuona Mola Wake Mlezi usiku wa Miraji. Katika kujibu na kupinga suala hilo alitumia Aya hii, na kama Aya hii isingekuwa inajumuisha watu wote na hali zote, basi asingeifanya dalili ya kupinga hilo. Hakuna shaka kwamba yeye alikuwa ni mtu mwenye elimu zaidi juu ya lugha ya Kiarabu, na kwa hivyo imethibiti kwamba Aya hii inajulisha juu ya ukashaji kwa kujumuisha watu wote.<sup>25</sup> Na fuo la Aya katika Surat An'aam limejulisha juu ya zuio na kumtakasa na kumuepusha Mwenyezi Mungu na hilo.

Na kauli yake (s.w.t): “Macho hayamfikii,” mtendaji hapa ni macho na makusudio ni dhati ya Mwenyezi Mungu (s.w.t), wala macho hayamuoni Yeye, huo ni upande wa kwanza, na kwa upande wa pili “bali Yeye huyafikia macho.” Basi upande huu umetofautiana na ule wa kwanza, kwani amesema: “bali Yeye huyafikia macho” na mtendaji hapa ni Mwenyezi Mungu (s.w.t), kumbuka hakusema: Na macho yake yanawafikia wao, lakini amesema: “bali Yeye huyafikia macho.” Macho ambayo hayawesi kumuona Yeye! Kwa hivyo pande zote mbili za maneno sio zenyе kuungana!

Na kwa ibara ya wazi zaidi ni kwamba: Hiyo ni kwa sababu kauli yake (s.w.t): “Macho hayamfikii” inazungumzia macho na kufikia kwake; na inajulikana kwamba hakika kufikia kwa macho ni uangaliaji na utazamaji wake na si elimu. Na fungu la pili nalo ni kauli yake (s.w.t): “Bali Yeye huyafikia macho,” inazungumzia yale ambayo Mwenyezi Mungu huyadiriki Yeye Mwenyewe kwa nafsi

<sup>25</sup> *Tafsir Imam Razi*, Juz. 7, uk. 13 / 133.

Yake; wala halizungumzii yale ambayo hudirikiwa na uonaji wake au haizungumzii uonaji na yale anayoyaona (s.w.t), na hili fungu la pili hutegemewa ndani yake elimu na hutegemewa pia uonaji, na yote mawili yanaruhusiwa.

Na kwa kuwa neno *al-Baswar* humaanisha mambo mengi ikiwa ni pamoja na macho yenye kuona au uwezo wa kuona au vinyoonwa; na kwa kuwa hakika Yeye anayafikia macho tokea pande zake zote hizi tatu, basi hali hiyo hturejesha hadi kwenye maana ya elimu, nayo ndiyo jumuishi zaidi; na haya hutokana na mishkeli ya kimaneno, na hakujuua hilo mwandishi wa kitabu cha *Ibaanat!* Na kwa hivyo makusudio ya kifungu cha kwanza “Macho hayamfikii” ni uangaliaji na utazamaji, na katika kifungu cha pili “Naye huyafikia maono” ni elimu! Na kwa hivyo inavunja maneno yake na mishkeli yake!

Kisha tunasema: Wamesema baadhi ya watu katika tafsiri ya Aya hii kwamba hakika macho hayamdiriki na hayamfikii kwa kumdhiliti, kwani Mwenyezi Mungu (s.w.t) hadhibitiwi na yeoyote kati ya viumbi! Na kauli hii mbovu inafidisha kwamba wao hawatamuona Yeye mzima bali sehemu yake tu! Yaani wanaona sehemu yake na wala hawaoni sehemu iliyobakia, na wakati huo anakuwa ni vijisehemu na kitu kazima, na anakuwa mwili! Na hii ni kauli batili!

### **Kukiri kwa Hafidh Ibn Hajar:**

Hafidh Ibn Hajar katika kitabu *Al-Fat’hu*, Juz. 8, uk. 607 amesema:

[Kinachopatikana ni kwamba makusudio ya Aya ni kukanusha udhibiti wakati wa kumuona Yeye, na sio kukanusha kumuona Yeye, na Qurtubi katika kitabu *Mufhim* ametoa dalili kwamba udiriki haukanushi kumuona Yeye kwa ushahidi wa kauli yake (s.w.t) akielezea kuhusiana na watu wa Musa A: “Na pindi makundi mawili yalipoon-

ana watu wa Musa wakasema hakika sisi ni wenyewe kufikiwa.” Na huo ni utoaji dalili wa ajabu kwani kinachofungamana na suala la udiriki katika aya 103 ya Sura ya 6 ni uonaji, hivyo ukarushaji kuwa ni kukanusha uonaji; tofauti na udiriki uliopo katika kisa cha Musa, na lau sio uwepo wa habari yenye kuthibitisha kuonekana kwa Mwenyezi Mungu isingelifaa kuachana na dhahiri.] Imeisha kutokana katika kitabu *Al-Fat’hu*.

#### Aya ya 6: Kauli yake (s.w.t):

وَمَا كَانَ لِبَشَرٍ أَنْ يُكَلِّمَهُ اللَّهُ إِلَّا وَحْيًا أَوْ مِنْ وَرَاءِ حِجَابٍ أَوْ يُرْسِلَ رَسُولاً

“Na haikuwa kwa mtu ye yote kwamba Mwenyezi Mungu aseme naye ila kwa ufunuo au kwa nyuma ya pazia au humtuma mjumbe ...”  
(42:51).

Aya hii imejulisha juu ya zolio la kumuona Mwenyezi Mungu (s.w.t) wakati Mwenyezi Mungu anaposema na mja wake, na kwa hivyo Bibi Aisha ﷺ akaitumia kutoa hoja kwa ujumla wake kuwa Bwana wetu Mtume Muhammad ﷺ hakumuona Mola Wake Mlezi usiku wa Miraji, kumrudi yule anayesema Mwenyezi Mungu anaonekana kwa macho. Naye sio mwingine bali ni Kaab Akhbar, na sio bwana wetu Ibn Abbas ﷺ, na huu ni uhakiki wetu kama utakavyokuja baadaye katika kitabu hiki Mwenyezi Mungu akipenda.

Qurtubi katika tafsiri ya Aya hii ya 53 ya Sura ya 16, amesema: Kauli yake (s.w.t): “Haikuwa kwa mtu ye yote kwamba Mwenyezi Mungu aseme naye ila kwa ufunuo” sababu ya hilo ni Mayahudi walimwambia Mtume ﷺ: ‘Kwa nini husemi na Mwenyezi Mungu na kumwona Yeye<sup>26</sup> ikiwa kweli wewe ni Nabii kama alivyokuwa Nabii Musa ﷺ? Hakika yeye alimwona, na hakika sisi hatutokua-

<sup>26</sup> Zingatia vipi hakika fikira hizi zenyewe kupatikana katika suala la kuonekana kwa Mola Manani ni fikira za kiyahudi za kumfanya Mola Muumba ana mwili, na hakika Mwenyezi Mungu ameepukana nalo analibatilisha hilo na analikanusha na kulipinga hilo.

mini wewe mpaka ulifanye hilo.<sup>27</sup> Mtume 8 akasema: “Hakika Musa hakumuona Mwenyezi Mungu kamwe.” hapo ikateremka kauli yake (s.w.t) inayosema: ‘Na haikuwa kwa mtu yeyote kwamba Mwenyezi Mungu aseme naye ila kwa ufunuo...’”

Na Imam Fakhru Razi رض<sup>27</sup> amesema: “Muutazila wamesema: Aya hii inajulisha kwamba Yeye (s.w.t) haonekani, na kwa hivyo Yeye (s.w.t) amezingira vigao vya ufunuo Wake katika mambo haya matatu. Na lau ingelisihi uonekanaji wa Mwenyezi Mungu (s.w.t) kiasi cha Yeye kuongea na mja ilihali mja akimuona Yeye; basi hilo lingekuwa ni jambo la nne, na Mwenyezi Mungu amekanusha sehemu hii ya nne kwa kauli yake: ‘Na haikuwa kwa mtu yeyote kwamba Mwenyezi Mungu aseme naye ila kwa ufunuo...’ ila katika sura hizi tatu.”

Na atakayezidisha sharti katika Aya hii kwa kudai kuwa makusudio yake ni duniani, tutamwambia yeye: Huku ni kusahihisha sharia! Na kusahihisha sharia ni jambo lisilojuzu, hususan ukizingatia kwamba dalili zilizotumika si sahihi na hazithibitishi hilo. Na muweka sharia haghafiliki hadi atanabaishwe, na wala hasahau hadi akumbushwe! Na hadithi zinazozungumzia suala la kumuona Mwenyezi Mungu si sahihi kama tulivyotanguliza maneno juu yake.

**Aya ya 7:** Na wametoa dalili baadhi ya watu juu ya suala la kumuona Mwenyezi Mungu kwa kauli Yake (s.w.t):

تَحِيَّهُمْ يَوْمَ يَلْقَوْنَهُ سَلَامٌ

**“Maamkuzi yao siku ya kukutana Naye yatakuwa ni Salaam.”**  
**(33:44).** Na kauli yake (s.w.t): **“Basi anayetumaini kukutana na Mola Wake Mlezi na afanye vitendo vizuri.”** (18:110), na aya nyinginezo katika ya zile ambazo zimetaja makutano hayo.

<sup>27</sup> Katika tafsiri yake Juz. 14, uk. 27 / 188.

Ukutanaji haufidishi kumuona, hii ni sawa na kauli Yake (s.w.t) kuhusiana na kifo: “Na kwa hakika mlikuwa mkiyatamani mauti kabla ya kuyakuta, basi mmekwisha yaona nanyi mnatazama.” (3:143) na wao hawakuyaona wala hawakuyaangalia hayo bali waliyaonja! Na yote hayo ni majazi na wala haikusudiwi kwayo uonaji wa macho!

Amesema Ibn Waziir akielezea jawabu katika hilo katika kitabu chake *Al-Awaswim Minal-Qawaswim*, Juz. 5, uk. 230: “Na asili katika jibu kuhusiana na hilo ni kwamba makutano si kwa maana ya uonaji, na kwa hivyo hutumia mmoja kati ya hao wawili namna ambayo haitumii mwingine, na juu ya hili hakika kipofu anasema: Nimekutana na fulani, na nimekaa mbele yake na nimemosome yeye, na wala hasemi nimemuona yeye, vivyo hivyo mmoja wao anamuuliza mwenzake, je, umekutana na mfalme? Anasema: Hapana lakini nimemuona juu ya Ikulu.” – Na lau ingelikuwa kukutana kunajulisha kwamba waumini wanamuona Mwenyezi Mungu (s.w.t) basi ingejibishwa kauli yake:

فَأَعْقَبَهُمْ نِفَاقًا فِي قُلُوبِهِمْ إِلَى يَوْمٍ يُلْقَوْنَهُ بِمَا أَخْلَفُوا اللَّهَ مَا وَعَدُوهُ وَبِمَا كَانُوا يَكْذِبُونَ

**“Kwa hiyo akawalipa unafiki nyoyoni mwao mpaka siku ya kukutana naye (Mwenyezi Mungu) kwa sababu ya kumkhali Mwenyezi Mungu ahadi waliiyomwahidi...”** (9:77), ijulishe kwamba wanafiki watamuona, na wao hawasemi hivyo kwa sababu:

إِنَّ الْمُنَافِقِينَ فِي الدَّرْكِ الْأَسْفَلِ مِنَ النَّارِ وَلَنْ تَجِدَ لَهُمْ نَصِيرًا

**“Hakika wanafiki watakuwa katika tabaka la chini kabisa motoni...”**  
**(4:145).** - Itakuwaje sasa wamuone Mwenyezi Mungu (s.w.t)!

Basi maana ya kukutana Naye (s.w.t) kwa upande wa waumini ni ile ithibati yake kwao, na kukutana naye (s.w.t) kwa upande wa

wanafiki na makafiri ni ile adhabu yake kwao, yaani kukutana na adhabu Yake au kukutana na malaika Wake (s.w.t). Kwa hakika yapasa kufanya tadaburi katika mfano wa kauli yake (s.w.t) inayosema:

فَالْيَوْمَ نَنْسَاهُمْ كَمَا نَسُوا لِقَاءَ يَوْمِهِمْ هُدًى

**“Basi leo tutawasahau kama walivyosahau mukutano wa siku yao hii...”** (7:51). Na kauli Yake (s.w.t) isemayo:

وَالَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَلِقاءَ الْآخِرَةِ حَبِطْتُ أَعْمَالُهُمْ

**“Na wale waliozikadhibisha Aya zetu na mukutano wa mwisho, vitendo vyao vimeharabika...”** (7:147) na yote haya hayamaanishi kuonekana kwa Mwenyezi Mungu kabisa.

**Aya ya 8:** Na wametoa hoja baadhi ya watu kuhusu suala la kuonekana kwa Mwenyezi Mungu kwa kauli yake (s.w.t):

وَلَقَدْ رَأَهُ نَزْلَةً أَخْرَىٰ عِنْدِ سِدْرَةِ الْمُنْتَهَىٰ

**“Na bila shaka ye ye amemuona kwa mara nyingine. Penye mkunazi wa mwisho.”** (53:13-14).

Na jibu: Hakika ambaye Mtume ﷺ alimuona kwa mara nyingine sio mwingine bali ni malaika Jibrail عليه السلام kwa dalili kadhaa wa kadha, kati ya hizo ni fuo la Aya mbalimbali, na mionganini mwa hizo ni: Mahala kwani alimuona katika mkunazi wa mwisho na Mwenyezi Mungu (s.w.t) hana mahali, sio mkunazi wa mwisho wala sehemu nyingine yoyote ile, na uonaji huo umetiliwa mkazo na Aya nyingine ambazo ziko katika mtiririko mmoja. Kati ya hizo ni kauli yake Mola Manani inayosema:

لَقَدْ رَأَى مِنْ آيَاتِ رَبِّهِ الْكُبْرَى

**“Kwa hakika aliona katika dalili za Mola Wake Mlezi zilizo kuu.” (53:18)**, na bwana wetu malaika Jibril ni mionganini mwa alama na dalili za Mwenyezi Mungu aliyetukuka bila shaka yoyote. Ki-sha wao wanaihukumu hadithi katika maana za Aya, na hakika Aya hizi zimefasiriwa kwa hadithi sahihi zilizomo katika vitabu sahihi, ambazo hazina kasoro wala msigano na kupingana.

Na katika *Sahihi Muslim* Juz. 1, uk. 159 na 177 kuna Hadithhi kutoka kwa Masruuq, amepokea kutoka kwa Bibi Aisha رضي الله عنها kwamba amesema: “Yeyote atakayesema moja kati ya matatu kwa hakika amemsingizia Mwenyezi Mungu uwongo mkubwa.” Nikasema: Ni yapi hayo? Akasema: “Yule anayedhani kwamba Mtume Muhammad ﷺ amemuona Mola Wake Mlezi, hakika huo ni uwongo mkubwa dhidi ya Mwenyezi Mungu (s.w.t).”

Anasema: Na nilikuwa nimeegemea basi nikaaa, nikasema: Ewe mama wa waumini! Nipe muda mimi wala usifanye haraka, je, Mwenyezi Mungu (a.j.) hakusema:

وَلَقَدْ رَأَهُ بِالْأَفْقِ الْمُبِينِ

**“Na hakika yeye alimuona katika upeo wa macho ulio safi.” (81:23),**

وَلَقَدْ رَأَهُ نَزْلَةً أُخْرَى

**“Na bila shaka yeye amemuona yeye kwa mara nyingine.” (53: 13)??**

Akasema: “Mimi ni wa awali katika umma huu aliyemuuliza Mtume ﷺ, akasema: Hakika huyo ni Jibrail, hakumuona katika sura yake ambayo ameumbiwa isipokuwa mara hizi mbili, alimuona yeye akiwa anateremka kutoka mbinguni, ukubwa wa umbo lake ni kati ya mbingu na ardhi.””

### Aya ya 9: Na vivyo hivyo kauli yake (s.w.t):

وَلَقَدْ رَأَهُ بِالْأَفْقِ الْمُبِينِ

“Na hakika yeye alimuona katika upeo wa macho ulio safi.” (81:23),

Na yametangulia maneno juu ya hilo, kwamba fuo la Aya mbalimbali katika sura hii linajulisha kuwa makusudio ni Jibrail, kwa sababu Mwenyezi Mungu (s.w.t.) hayuko katika upeo wa macho ulio safi, kwani upeo wa macho ulio safi ni sehemu, na Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametakasika na uwepo katika mahala fulani, ila ni imani ya wale wajinga wenyewe fikra kuwa Mwenyezi Mungu ana mwili. Na fuo la Aya hizo ni kauli yake (s.w.t):

إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ ذِي فُؤُرَةٍ عِنْدَ ذِي الْعَرْشِ مَكِينٍ مُطَاعٍ ثُمَّ أَمِينٍ

“Kwa hakika hiyo ni kauli ya Mtume Mtukufu. Mwenye nguvu, mwenye cheo mbele ya Mwenye Arshi. Anayetiwa kisha mwamini-fu.” (81:19-21).

Na katika faslu inayofuata utakuja ufanuzi zaidi kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu aliyetukuka juu ya hilo.

**Aya ya 10.** Zipo Aya ndani ya Qur’ani tukufu zinazobainisha kuwa ombi la kutaka kumuona Mwenyezi Mungu (s.w.t) ni mionganini mwa mambo yenye kukemewa kisheria, na kati ya hayo ni kisa cha Nabii wetu Musa عليه السلام na ombi lake la kutaka kumuona Mwenyezi Mungu, na kuhusu hilo Mwenyezi Mungu (s.w.t) anasema:

يَسْأَلُكَ أَهْلُ الْكِتَابِ أَنْ تُنَزِّلَ عَلَيْهِمْ كِتَابًا مِنَ السَّمَاءِ فَقَدْ سَأَلُوا مُوسَى أَكْبَرَ مِنْ ذَلِكَ فَقَالُوا أَرْنَا اللَّهَ جَهْرًا فَأَخْذَتْهُمُ الصَّاعِقةُ بِظُلْمِهِمْ

**“Watū wa kitabū wanakutaka uwateremshie kitabū kutoka mbin-guni. Hakika walimuomba Musa makubwa kuliko hayo wakasema: Tuoneshe Mwenyezi Mungu wazi wazi, ikawashika ngurumo (ya radi) kwa sababu ya dhulma yao...” (4:153)**

Na kauli yake Mola Manani (s.w.t):

وَقَالَ الَّذِينَ لَا يَرْجُونَ لِقَاءَنَا لَوْلَا أُنْزِلَ عَلَيْنَا الْمَلَائِكَةُ أَوْ نَرَى رَبَّنَا<sup>٢٥</sup>

**“Na walisema wale wasiotumai kukutana nasi: Mbona sisi hatuter-emshiwi Malaika, kumuona Mola wetu Mlezi?...” (25:21), Na makusudio kuhusiana na hayo yako wazi na dhahiri.**

### **Dalili za Kiakili Ambazo Baadhi ya Watu Wanadai Kuwa Zinathhibitisha Kwamba Mwenyezi Mungu Ataonekana:**

Wameeleza baadhi ya watu hoja na dalili walizoona kuwa ni mionganoni mwa dalili za kiakili zenye kuthhibitisha kuwa yafaa na inawezekana kumuona Mwenyezi Mungu (s.w.t) au kwamba suala hilo limethibiti, na kati ya dalili hizo batili ni kauli yao:

**Ya Kwanza:** Kila kilichopo inasihi kuonekana, na Mwenyezi Mungu yupo, kwa hivyo inasihi Mola Manani aonekane!!!

Kwa hakika kwangu mimi huu ni upotofu mionganoni mwa mapotofu! Kwani kanuni ya kila kilichopo inasihi kuonekana iliyosemwa na baadhi ya wanatheolojia ni kanuni batili, haina msingi wowote sahihi kama wasemavyo watu wa elimu ulimwenguni. Na hakika iliwekwa na aliyeiweka ili kuthhibitisha muradi wake! Nayo ni kanuni iliyobuniwa ambayo haina msingi wowote wa usahihi! Kuna vitu havionekani na ye yote hata darubuni (*Telescope*) na hadubini (*Microscope*) kama vile hewa na mvutano na sumaku, mvutano wa mawimbi ya umeme na kuhisi maumivu na vitu vingi ambavyo inawezekana mwanadamu akavitafakari na akaulizia kwa watu wa elimu na wenye ubobezi.

Na kanuni hii pia ni batili kisheria, kwa kauli ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) aliposema: “Na ninaapa kwa vile mnavyoviona na msivyoviona.” Mwenyezi Mungu amebainisha kwetu kwa lafudhi ya (vile) yaani ambavyo, neno lenye kujulisha juu ya vitu visivyo na akili, kwamba kuna vitu tunavyoviona na viro tusivyoviona, na kwa mujibu huu vitu vimegawanyika sehemu mbili: Vyene kuonekana na visivyoonekana, na kwa hivyo imebatilika kanuni hii ya kipotofu.

Na hata tukijaalia kuwa kila kilichopo kati ya vilivyoumbwa inasihi kuonekana, bado Mwenyezi Mungu (s.w.t) haimhusu kanuni hii wala haifanyi kazi juu Yake, kwani yeze “hafanani na chochote,” na kwamba yupo lakini sio kama vile vilivyopo. Hana mwili, hana umbo, hachukui nafasi katika sehemu ya wazi wala hana urefu wala upana wala kina wala sura wala umbo, wala kiwiliwili, na kwa hivyo linafeli hitimisho walilolitaka hao kwamba Mwenyezi Mungu atonekana, kwani kila kilichopo kinaonekana, kwa sababu kumlinganisha Muumba na viumbe ni ufisadi na uovu na batili.

**Ya Pili:** Kauli yake: Je, wewe na wanazuoni ambao wamesema kuwa haiwezekani kumuona Mwenyezi Mungu ndio wajuzi zaidi au Nabii wetu Musa ﷺ ambaye aliomba kumuona Mwenyezi Mungu? Na Manabii ni wajuzi zaidi ya watu wa yale yanayowezekana na yanayokuwa ni muhali katika haki ya Mwenyezi Mungu (s.w.t)!!

Jibu: Ukemeaji na uogopeshaji dhidi ya mpinzani katika yale ambayo yeze amepatia, madahara yake hayamrudii isipokuwa yule mtoaji vitisho! Wala hili halizuii sisi sote kuwa wenye kujua na wenye maarifa na jambo fulani sasa hivi baada ya Mtume ﷺ kutumwa, halizuii sisi kuwa na maarifa na jambo kuliko Manabii Wake kabla Mwenyezi Mungu hajawapa elimu na kuwajulisha jambo husika! Bali huenda ukawa wewe na wanazuoni wa Kiislamu ni wajuzi zaidi wa jambo mionganini mwa mambo ya Kiislamu ya leo kuliko bwana wetu Mtume Muhammad ﷺ kabla Mwenyezi

Mungu hajamfundisha yeye jambo hilo! Na hii haimaanishi kuwa watu ni wajuzi zaidi kuhusu hilo kuliko Mtume ﷺ na Manabii ambao wao ni wajuzi zaidi ya viumbe na wenyе maarifa zaidi kuliko wao kuhusu Mwenyezi Mungu, basi utoaji vitisho na uogopeshaji hautangulizi wala haucheleweshi!

Natoa dalili yenyе nguvu zaidi juu ya hilo, nasema: Bukhari katika *Sahih* yake amesema: “Mlango wa yale aliyokuwa Mtume ﷺ akiulizwa ambayo ufunuo haukuteremshwa kwake, na yeye akisema: Sijui au hakujibu mpaka uteremshwe ufunuo..... na Ibn Mas’ud amesema: Mtume ﷺ aliulizwa kuhusu roho basi akan-yamaza mpaka ilipoteremka Aya.” Na *Bukhari* (7309) amepokea kutoka kwa Jabir bin Abdillah Answar kwamba alipatwa na maradhi basi Mtume ﷺ akamtembelea akamwambia: Nifanye nini katika mali yangu? Akasema: Basi hakunijibu mimi lolote mpaka ilipoteremka Aya ya mirathi.

Na wewe hivi sasa na wanazuoni wa Kiislamu mnajua hukumu ya mirathi. Na mbora wa viumbe, na yeye ndiye mjuzi zaidi, kabla ya muda huo alikuwa hajui jambo hili, na kwa hivyo akanyamaza na hakujibu chochote mpaka ilipoteremka Aya.

Na Nabii wetu Musa عليه السلام – kwa sura yoyote ile hata ikiwa haijanukuliwa ni kwa lengo lipi aliomba, ila yeye anajua kuwa hilo hali-fai na haliwezekani – alipoomba hakuwa anajua hukumu yake basi Mwenyezi Mungu akamfundisha yeye na akasema: “Kamwe hutania” na kwa hivyo akaomba msamaha Nabii wetu Musa عليه السلام juu ya swalii kama ilivyokuja mwishoni mwa Aya aliposema: **“Na alipoz-induka akasema: Utakasifu ni Wako, natubu Kwako, na mimi ni wa kwanza wa wanaoamini.”** (7:143). Na baada ya Mwenyezi Mungu kumpa maarifa yeye kwa kauli yake: “Kamwe hutania” na kutujulisha sisi kwa kauli yake: “Macho hayamfikii bali yeye huy-

afikia macho” tumejua kuwa hilo haliwezekani, na Nabii Musa ﷺ kabla ya kuomba hakuwa mwenye kujua hilo! Na kwa hivyo Mwenyezi Mungu aliwaneemesha Mitume wake akasema:

وَعَلِمَكَ مَا لَمْ تَكُنْ تَعْلَمُ وَكَانَ فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكَ عَظِيمًا

**“Na amekufundisha yale uliyokuwa huyajui, na hakika fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yako ni kubwa.” (4:113).**

Basi Mwenyezi Mungu (s.w.t) amemwambia mbora wa viumbe na mjuzi zaidi, bwana wetu Mtume Muhammad ﷺ: “Na akukukuta ukihangai (kuongoza watu) naye amekuongoza?” (93:7) na akamwambia: “Na tukakufundisha yale uliyokuwa huyajuwi” basi Mitume wanazaliwa hali hawana maarifa ya Mwenyezi Mungu wala elimu ya dini na hakika Mwenyezi Mungu huwaelimisha wao kitu kimoja baada ya kingine baada ya kutumwa rasmi!! Hapo inateremka Qur’ani kidogo kidogo ili apate kujua na kupata maarifa ya jambo moja baada ya jingine!!

Na mimi ninauliza hapa: Je, Nabii tangu muda wa awali (katika ulimwengu wa mbegu) anakuwa ni Nabii na anakuwa ni mjuzi wa kila kitu au Mwenyezi Mungu anamfundisha mambo kidogo kidogo? Ukitisema tangu ulimwengu wa mbegu, nitasema: Hakuna dalili juu ya hilo!! Na kwa hivyo wakasema: Na mara ngapi Mtume Muhammad Mustafa ﷺ alijibu ndio baada ya kujiwa na wahyi, kinyume na hivyo alikuwa hatoi jibu lolote.

Na ukisema: Kidogo kidogo...ninasema kukwambia wewe: Na haya ni mionganoni mwa mambo hakuwa anayajua kabla, na wewe na ye ye sasa hivi ni wajuzi wa hilo! Au ilikuwa ni mtindo wa kutaka kuingiza kidogo kidogo na aliwataka watu wake wapate hivyo!! Na uwepo wa kauli yake ﷺ baada ya kuomba kumuona Mwenyezi Mungu: “Utakasifu ni Wako nimetubu Kwako na mimi ni wa kwan-

za wa walioamini” inatilia mkazo maneno yetu na kubainisha kuwa vitisho na uogopeshaji dhidi ya mwenye kwenda kinyume kwa kauli yake: ‘Itakuwaje Manabii wawe hawamjui Mwenyezi Mungu...’ ni kauli batili haina maana na wala haina ulazima!

Na ama Walii: Hakuna tatizo yeze kutomjua Mola Wake Mlezi! Na kutokuwa mkamilifu! Kwani hujifunza kidogo kidogo! Na kauli ya kuwa Walii hawi mjinga ni kauli isiyokubalika na haina mashiko na ni yenze kukataliwa! Kama vile ulazimishaji wa kwamba kauli yangu katika muktadha wake inalazimisha mimi kuwa ni mjuzi na mwenye maarifa zaidi ya kumjua Mwenyezi Mungu kuliko Nabii Musa ﷺ ni maneno ambayo haiwezekani kusemwa kulingana na kipimo cha maelezo tuliyokwisha tanguliza hapo kabla!!

**Ya Tatu:** Upotoshaji kwamba Mwenyezi Mungu atawaumbia watu Siku ya Kiyama macho na uonaji mwingine wa kudumu kwa hivyo watamuona Mwenyezi Mungu (s.w.t) na watamtazama Yeye na sio utazamaji wenye kutoweka na kwisha!!

**Nasema:** Hakika huo ni upotofu hauna dalili, na ni ufinyu wa kimawazo na ufikiriaji finyu na duni! Tunasema: Uonaji wa macho duniani na akhera umeumbwa na ni wenye kuzuka, nao hata ukitokafautiana na wa akhera ila hakika huo utabakia wenye mapungufu na ni dhaifu kwani huo umeumbwa na umezuka hauwezi kumdiriki wa tangu na tangu muumbaji wa kila kitu!

Na hili linafungamana na jambo muhimu katika utoaji wao wa dalili kwa kutumia kisa cha Nabii wetu Musa A, hakika wao wanasma hakika Mwenyezi Mungu haonekani duniani kwa macho yenze kuisha! Basi ni kwa nini wanatumia ombi la bwana wetu Nabii Musa ﷺ kutaka kumuona Mwenyezi Mungu kuwa ni dalili ya yeze kuskudia kumuona Mungu duniani kwa jicho la kwisha ambalo halil-

jawa na nguvu mfano wa macho ya watu wa akhera yenyeye nguvu ambayo wao wanadai?!

### **Kadhia ya Mtume Kumuona Mwenyezi Mungu (s.w.t) Usiku wa Israi na Miraji:**

Mweyezi Mungu akurehemu. Jua kwamba hapana budi kufanya utafiti juu ya suala hili kwanza kwa upande wa uwepo wake ndani ya Qur'ani tukufu, tunasema: Na hakika zimeshatangulia kwa ufupi kauli Yake (s.w.t): “**Na hakika alimuona mara nyingine katika mkunazi wa mwisho**” na kauli Yake (s.w.t): “**Na hakika ye ye ali muona katika upeo wa macho ulio safi**” (81:23), na kauli Yake (s.w.t): “Kisha akakaribia, na akateremka. Ndipo akawa umbali wa pinde mbili au karibu zaidi,” na sasa hebu tuangalie kwa mapana na Mwenyezi Mungu (s.w.t) Ndiye Mwezeshaji.

Kauli yake (s.w.t): “Kisha akakaribia, na akateremka. Ndipo akawa umbali wa pinde mbili au karibu zaidi.” Ninasema: Hapana budi kuzirejea Aya hizi pamoja na zile za kabla yake ili tuweze kuzifahamu kutokana na fuo lake na mtiririko wake wa maana, twende mwanzoni mwa Surat an-Najmi, tunasema: Mwenyezi Mungu (s.w.t) anasema:

وَالنَّجْمٌ إِذَا هَوَىٰ مَا ضَلَّ صَاحِبُكُمْ وَمَا عَوَىٰ

“**Naapa kwa nyota inapoanguka. Mwenzenu hakupotea.**” (53:1-2), yaani Bwana wetu Mtume Muhammad ﷺ, na kisha:

مَا ضَلَّ صَاحِبُكُمْ وَمَا عَوَىٰ وَمَا يَنْطِقُ عَنِ الْهَوَىٰ إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ

“**Na wala hakukosea wala hatamki kwa matamanio yake, hayakuwa haya ila ni ufunuo anaofunuliwa**” (53:2-4), yaani unaoshuka kwake, na ufunuo huu ambao umeteremka juu ya bwana

wetu Mtume ﷺ amemfundisha yeye kwa amri ya Mwenyezi Mungu (a.j.) bwana wetu Jibrail ﷺ, ametuhabarisha Mwenyezi Mungu kuhusiana na hali yake na wasifu wake kwa kauli yake (s.w.t) baada ya hili:

**عَلَمَهُ شَدِيدُ الْقُوَىٰ ذُو مِرَّةٍ فَاسْتَوَىٰ**

**“Amemfundisha mwenye nguvu sana<sup>28</sup> mwenye umbo zuri, akatulia.” (53:5-6)**, na wasifu huu ni wa bwana wetu Jibrail ﷺ ambaye Mwenyezi Mungu amesema kumhusu yeye katika Aya ny- ingine:

**ذِي قُوَّةٍ عِنْدِ ذِي الْعَرْشِ مَكِينٌ مُطَاعٌ ثُمَّ أَمِينٌ**

**“Mwenye nguvu, mwenye cheo mbele ya mwenye Arshi, mwenye kutiwa huko mwaminifu.” (81:20-21)**, na maana ya neno “*dhu Mirratin*” yaani kiumbe mwenye nguvu nyingi sana. Amesema al-Hafidh Abu Hayan katika kitabu *al-Bahru al-Muhiti*: ““Naye yuko upeo wa juu kabisa’ (53:7) yaani Mtume alimuona Jibrail jinsi alivyo akiwa ameziba upeo wa macho juu kabisa, akiwa na mabawa 600, na muda huo akamkaribia Mtume Muhammad ﷺ mpaka akakaribia ukaribu wa pinde mbili. Na vivyo hivyo yeye alionekana mara ny- ingine akiwa na mbawa 600 sehemu ya mkunazi wa mwisho... ‘ki- sha akakaribia’ kwa Mtume ﷺ ‘Akateremka’ basi akaning’inia angani, na aliquwa umbali wa masafa mafupi karibu naye mfano **wa ‘umbali wa pinde mbili, au karibu zaidi’ (53:9).**

<sup>28</sup> Lafudhi hii ina maanisha kwamba makusudio hapa sio mwengine bali ni bwana wetu Jibrail ambaye Mwenyezi Mungu (s.w.t) amemtuma yeye kwa Bwana wetu Muhammad ﷺ kuwa ni mwalimu, naye amesifika kwamba ni mwenye nguvu kubwa na kwamba yeye akaenea akatulia kwani yeye katika upeo wa mbali wa juu kabisa na hakika aliakaribia na akateremka au akawa umbali wa pinde mbili kutoka kwa mtume ﷺ au karibu zaidi, na hakika yeye alimfunulua bwana wetu Muhammad ﷺ aliyomfunulua kati ya yale ambayo aliyomwamrisha yeye kutoka kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t).

Basi zikaondolewa nyongeza hizi kama alivyosema Abu Ali katika kauli yake: ‘Na hakika umenifanya mimi kutokana na Khuzaima kidole kimoja, yaani mwenye masafa ya umbali wa kidole kimoja.’ ‘Au karibu zaidi’ kwa ukadiriaji wenu, kama vile kauli yake ‘au wanazidisha’, ‘hadi kwa mja Wake’ yaani hadi kwa mja wa Mwenyezi Mungu... ‘Yale aliyomfunulia” ni kutukuza ufunuo ambaa amemfunulia yeye hapo kabla.”” Imekwisha.

Na amesema Ibn Atwai: “Kisha akakaribia’ wengi wamesema: Yaani Jibrail alikaribia hadi kwa Mtume Muhammad akiwa katika umbile lake halisi, na Ibn Abbas na Anas bin Malik wakasema katika hadithi ya Israi: Yaliyo katika muktadha huo ni kwamba ukaribiajji huegemezwu kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) ... na sahihi ni kwamba yote yaliyopo katika kauli hizi yanamhusu Jibrail, kwa dalili ya kauli ya Mwenyezi Mungu ‘Na hakika alimuona yeye mara nyingine.” (53:13). Hakika hii awe alishawahi kumuona kabla ya hapo, na hakika haijapokewa kuwa Mtume aliwahi kumuona Mola Wake Mlezi kabla ya usiku wa Israi.....

‘Basi akamfunulia’ yaani Mwenyezi Mungu ‘mja wake...’ na Hasan amesema: ‘Basi akamfunulia Jibrail mja wa Mwenyezi Mungu Muhammad ﷺ yale aliyomfunulia kama vile ya awali.’ Na Ibn Zayd akasema: ‘Basi akamfunulia Jibrail mja wa Mwenyezi Mungu Muhammad ﷺ yale aliyomfunulia yeye Mwenyezi Mungu (s.w.t) Jibrail ﷺ ’ ‘Haukusema uongo’ (53:11) moyo wa Muhammad ﷺ yale aliyoyaona kwa macho yake kutokana na sura ya Jibrail: Yaani yale yaliyosema moyo wake pindi alipomuona kwamba sikukujua wewe, yaani: Hakika yeye alimuona kwa macho yake mawili na akamwelewa kwa moyo wake, na hakuweka shaka katika yale aliyoyaona yeye kwa haki.””

Haya ndio yaliyoelezwa na kunukuliwa na Hafidh Abu Hayyan katika kitabu chake *Bahrul-Muhit*. Na kutokana na hayo inabaini-

ka kwamba Aya hii haina dalili inayothibitisha kuwa Bwana wetu Mtume ﷺ alimuona Mwenyezi Mungu (s.w.t).

**Nasema:** Na ama yale yaliyokuja kutoka kwa Ibn Abbas na Anas bin Malik kwamba ukaribiaji huo ni kukaribia kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t), ni batili na yanakataliwa na mahafidhi na watu wa elimu hata kama yameelezwa ndani ya *Sahih*, ninakusudia Bukhari. Katika *Bukhari* 7517 kuna riwaya kutoka kwa bwana wetu Anas bin Malik katika hadithi ya Israi: “Na akamkaribia Jabbar Mola Mlezi na Mtukufu na akateremka hadi akawa umbali wa pinde mbili au karibu zaidi.”

Hafidh Ibn Hajar katika kitabu *Fat'hul-Bari*, Juz. 13, uk. 483: [Khattabi amesema: “Hakuna katika kitabu hiki yaani *Sahih* *Bukhari* hadithi ichukizayo zaidi kidhahiri wala ichukizayo vionjo kama hadithi hii, kwani muktadha wake unaweka mipaka ya masafa baina ya pande mbili zilizotajwa, na kupambanua sehemu ya kila upande mmoja kati ya hizo mbili, hili hakika linajulisha mshabihiano na mfanano kati Yake na kitu ambacho alikikaribia kutoka juu mpaka chini.”]

Kisha Hafidh katika uk. 484 akasema: [Akasema: (Yaani Khatwabi) “Hakika imepokewa hadithi hii kutoka kwa Anas bin Malik kutoka katika njia isiyokuwa ya Sharik. Katika njia hiyo hakutaja ndani yake tamko hili baya, jambo ambalo linatilia nguvu kwamba tamko hilo limetoka upande wa Sharik.”]

Na ameeleza Umawiy katika kitabu *Maghaziya* na kutoka katika njia yake ameeleza Bayhaqi kutoka kwa Muhammad bin Amru kutoka kwa Abi Salama kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنه katika kauli yake (s.w.t) inayosema: “Kisha akakaribia akateremka” akasema: “Alikaribia kwake Mola Wake, na sanadi hii ni nzuri, nayo ni ushahidi wenye nguvu juu ya riwaya ya Sharik.”

Kisha Khatwabi akasema: “Na katika hadithi hii kuna tamko jingine ambalo kalitaja Sharik peke yake, hakuna mwingine ali-yelitaja, nalo ni kauli yake: ‘Basi akaenda naye juu, yaani Jibrail akamwelekea Jabbar (s.w.t) akasema ilihali ye ye akiwa sehemu yake: ‘Ewe Mola Wangu Mlezi tufanyie wepesi sisi.’” Na sehemu haiongezwi kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t), hakika hiyo ni sehemu ya Nabii ﷺ mahala pake pa kwanza ambapo alisimama hapo kabla ya kuteremka kwake.”

Kisha Hafidh akasema: [Na amesema Abdul-Haqq katika *Jam'u Bayna Swahihayni*: Ameongeza humo, yaani Shariik, ziada isiyojulikana, na ameleta ndani yake tamko lisilojulikana, na hakika Israi imepokewa na watu kadhaa mionganoni mwa Mahafidhi wa hadithi na wala hakuleta ye yote mionganoni mwao yale aliyoyleta Sharik kuhusu Israi. Na Sharik sio mionganoni mwa Mahafidhi wa hadithi, na ametangulia kusema hilo Abu Muhammad bin Hazm katika yale aliyoeleza Hafidh Abu Fadhl bin Dahir katika Juzu aliyoikusanya ye ye akaiita *Al-Intiswaar Liayyamil-Amswaar*.

Amenukuu humo kutoka kwa Humaydi, kutoka kwa Ibn Hazmi kwamba amesema: ‘Hatukupata kwa Bukhari na Muslim katika vitabu vyao viwili, chochote kisichofaa kuwasilishwa ila hadithi mibili. Dhana iliwashinda wakati wa uandikaji wa Hadithi hizo licha ya umakini wao na kusihi maarifa yao.’ Akataja hadithi hii na akasema: ‘Ndani yake kuna matamko yasiyofahamika na maafa kutoka kwa Sharik. Kati ya matamko hayo ni kauli yake ‘kabla hajafunuliwa wahyi,’ eti alifaradhishiwa Swala. Wakati hakuna tofauti kati ya watu wa elimu kwamba hakika Swala ilifaradhishwa mwaka mmoja kabla ya kuhama, baada ya kufunuliwa wahyi karibuni miaka 12. Pia ni kauli yake ‘Hakika Jabbar akateremka mpaka akawa karibu naye umbali wa pinde mbili au karibu zaidi.’ Na Bibi Aisha ؓ anasema: ‘Hakika aliye karibia na kuteremka ni Jibrail.’”] Imekwisha.

Kisha Hafidh akasema: [Na hakika imetangulia kutanabahisha yale yaliyopo katika hadithi ya Sharik yenyewe kwenda kinyume na Muslim katika *Sahih* yake, kwani yeye amesema baada ya kutaja sanad yake na baadhi ya matini: “Alitanguliza na akachelewesha, akaongeza na akapunguza.” Na Ibn Hazmi alitanguliwa na Abu Suleiman Khatwani katika kuzungumzia maneno ya Sharik kama nilivyotanguliza, na Nasai na Abu Muhammad bin Jaruud wamemzungumzia kwa kusema: “Ni dhaifu.” Na Yahya bin Said Qatwan alikuwa hasimulii kutoka kwake. Ndiyo, Muhammad bin Saad na Abu Daud wamesema: “Ni mwaminifu.” Hivyo basi ni mtu ambaye wametofautiana kumhusu yeye, basi anapokuwa peke yake katika jambo, huhesabika jambo hilo kuwa ni la kinyume na pia ni baya kwa wale wanaoona istilahi ya kinyume na baya ina maana moja.]

Kisha Hafidh akasema: [Na jumla ya mambo ambayo Sharik amekuwa peke yake katika mambo hayo, kwa kwenda kinyume na walio mashuhuri ni mambo kumi bali ni zaidi ya idadi hiyo ya kwanza...]

Na ama dhana ya baadhi ya wanazuoni kwamba mkanushaji wa suala la Mtume ﷺ kumuona Mwenyezi Mungu (s.w.t) usiku wa Israi kuwa ni Bibi Aisha ؓ peke yake ni dhana batili kwa mitazamo ifuatayo:

Hakika ukanushaji huo ni kauli ya Mtume ﷺ na sio kauli ya Bibi Aisha ؓ, tofauti na yale ambayo yamenukuliwa kutoka kwa Ibn Abbas ؓ, katika kitabu *Sahih Muslim* Juz. 1, uk. 159 na 177 kutoka kwa Bibi Aisha ؓ amesema: “Ni mimi ni wa mwanzo katika umma huu niliyemuuliza Mtume ﷺ, akasema: Hakika ni Jibrail, sijamuona katika sura yake ambayo ameumbiwa isipokuwa katika mara hizi mbili.....”

Na hakudai hilo Bibi Aisha ﷺ peke yake bali amesema kuhusu hilo pia Ibn Masuud ﷺ kama ilivyo katika *Sahih Bukhari* 3232 na *Muslim* Juz. 1, uk. 158 na 175. Vivyo hivyo amesema kauli hiyo Abu Huraira. Katika *Sahihi Muslim* 175 kutoka kwa Abu Huraira: “Na hakika amemuona mara nyingine.” Alimuona Jibril.”

Na hakuna katika kitabu *Sahihi Muslim* kulingana na kauli ya Ibn Abbas K kwamba yeze alimuona Mwenyezi Mungu, bali mane-no yake huko ni “Alimuona kwa moyo wake.” Na vivyo hivyo, “Alimuona kwa moyo wake mara mbili.” Na kiwakilishi hapa kinrudishwa mpaka kwa Jibrail, na ni dhahiri hakika baadhi ya watu wameongeza tamko “Mola Wake Mlezi”.

Na ukanushaji wa Bibi Aisha ﷺ haukuwa kumkanusha Ibn Abbas ﷺ, hakika ulikuwa kumkanusha Kaab Akhbar, na dalili juu ya hilo ni yale aliyoyataja Hafidh katika kitabu chake *Fat'hul-Bari*,<sup>29</sup> Juz. 8, uk. 606 amesema: “Katika hadithi ya Tirmidhi<sup>30</sup> kuna nyongeza ya kisa katika simulizi yake. Ameandika kutoka katika njia ya Mujtahid kutoka kwa Shaabi, amesema: Ibn Abbas ﷺ ali-kutana na Kaab Akhbar sehemu ya Arafa, akamuuliza yeze kitu basi Kaab akatoa takbira hadi milima ikamwitikia, akasema Ibn Abbas ﷺ: Hakika sisi ni ukoo wa Hashim! Kaab Akhbar akamwambia: Hakika Mwenyezi Mungu amegawa kati ya kuonekana kwake na maneno yake. Hivi ndivyo ilivyo katika simulizi ya Tirmidhi. Ama kwa Abdul-Razzak ni kwamba, Ibn Abbas ﷺ akasema: Hakika sisi ni ukoo wa Hashim tunasema: Hakika Muhammad alimuona Mola Wake Mlezi mara mbili, basi Kaab akatoa takbira akasema: Hakika Mwenyezi Mungu amegawa uonekanaji wake na maneno yake baina ya Musa na Muhammad, akasema na Musa mara mbili, na Muhammad akamuona mara mbili. Masruuq anasema: Basi nikaingia

<sup>29</sup> Wakati wa utoaji wa maelezo ya hadithi ya 4855 mwanzoni mwa tafsiri ya Surat Najm.

<sup>30</sup> *Sunan Tirmidhiy* 3278.

kwa Bi. Aisha ﷺ nikasema: Je, Muhammad alimuona Mola Wake Mlezi?..., na Ibn Murduwayh kutokana na njia ya Ismail bin Abi Khalid kutoka kwa Abdullah bin Harith bin Nufail kutoka kwa Kaab ana riwaya mfano wa hiyo. Akasema yaani Shaabi: Basi Masruuq akaenda kwa Bi. Aisha ﷺ akataja hadithi, basi ikadhihiri kwa hilo sababu ya swali la Masruuq kwa Bi. Aisha ﷺ kuhusiana na hilo.” Imekwisha kutoka katika kitabu *Fat'hul-Bari*.

Na hapo Bibi Aisha ﷺ akasema: “Ni uzushi mkubwa mno juu ya Mwenyezi Mungu (s.w.t),” yaani ni uongo mkubwa juu ya Mwenyezi Mungu (s.w.t), na kwa kuwa ukarushaji hapa umekuja kinagaubaga dhidi ya riwaya zilizotangulia basi ulikuwa ni ukarushaji dhidi ya Kaab Akhbar na huku ni kumtoa ila na dosari waziwazi. Na hii ni sawa na kauli ya Muawiya kumhusu yeye Kaab kama ilivyo katika kitabu *Sahih Bukhari* (7361): “Na hakika tulikuwa pamoja naye ili muongo ajaribiwe kupitia yeye.” Na hili ni kati ya yale am-bayo yanatilia mkazo kwetu sisi kwamba Masahaba walimtuhumu kwa uongo, hata wakijaribu baadhi ya wale aliowataja Hafidh ibn Hajar kupindisha mambo.

Ninaongeza katika hilo kauli ya bwana wetu Umar bin Khatwab kumwambia Kaab: “Utaachana na hadithi au nikuunganishe wewe na ardhi ya mangedere.” Nayu ni sahihi na thabiti kutoka kwa bwana wetu Umar, ameipokea hiyo Abu Zur’at katika *Tariikh* yake Juz. 1, uk. 544.

Na yote haya ni mfano wa maneno ya Ibn Abbas ﷺ kuhusu mtoto wa mwanamke, Kaab Akhbar Nufu Albakaali: “Amesema uongo adui wa Mwenyezi Mungu.” Nayu ipo katika *Bukhari* Juz. 1, uk. 218, na 122. Na imenivutia kauli ya Hafidh Ibn Hajar huko: “Nikasema: Inawezekana ikawa Ibn Abbas ﷺ amemtuhumu Nufu kuhusu usahihi wa Uislamu wake.”

Na ufupisho wa yale ninayoamini ni kwamba hakika hii ni kisoro na ila kubwa iliyothibitishwa na Masahaba dhidi ya watu hawa, na hakika baadhi ya wale waliokuja baada yao wamejaribu kutaka kuwasafisha na kuwatetea na kujaribu kupindisha mambo juu yao kwamba wamezushiwa na kusingiziwa kwa sababu siasa ya ukoo wa Umayya ulikuwa umesimama katika kuwainua watu hawa na kuwafungulia mlango wa kusimulia hadithi, wakati hapo kabla katika zama za Bwana wetu Umar na ﷺ wana wetu Ali walikuwa ni weneye kupuuzwa, madhalili na hawaruhusiwi kuzungumza.

Na mambo haya kamwe hayafahamu ila yule ambaye ameondo-kana na taasubi na ushabiki wa upofu na kuwfanyia upole watu wasio na hadhi dhidi ya andiko la Kitabu na Sunnah! Ka'ab bin Akhbar alikuwa akisema: "Mwenyezi Mungu amesema katika Taurat! Na ninasoma katika Taurat! Na..."

Na Mwenyezi Mungu (s.w.t) anasema:

وَيَقُولُونَ هُوَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ وَمَا هُوَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ وَيَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبُ وَهُمْ يَعْلَمُونَ

**"Na wanasema hilo limetoka kwa Mwenyezi Mungu na halikutoka kwa Mwenyezi Mungu na wanasema uongo kwa Mwenyezi Mungu na hali ya kuwa wanajua."**

(Surat aal'Imraan 3:78)

## FAIDA YENYE KUSTAAJABISHA NA KUSHANGAZA

**T**unafaidika kutokana na hayo kwamba hapana budi kuangalia na kuhakiki, na wala haifai kutegemea maneno ya Mahafidh au watu wa hadithi vyovyyote itakavyokuwa hadhi yao!! Hafidh Ibn Hajjar katika kitabu chake *Fat'hul-Bari*, Juz. 8, uk. 607 katika ufanuzi wa hadithi nambari 4855 amesema: [Nawawi<sup>31</sup> amesema akimfuta mwingine: “Bi. Aisha  hakukanusha kitendo cha kuonekana kwa Mwenyezi Mungu kwa hadithi isiyo na sanadi (haina mlolongo wa wapokezi), na lau angelikuwa na Hadithi angeitaja.<sup>32</sup> Na hakika alitegemea dhahiri ya Aya kung’amua fatwa juu ya yale aliyoyataja, na hakika wamemkhaliu katika hilo Masahaba wengine. Na sahaba akisema neno na akaenda kinyume nalo mwingine mionganini mwao, kauli hiyo haiwi ni hoja yenye maafikiano, na makusudio ya kudiriki katika Aya ni kudhibiti, na hilo halipindi uonekanaji wa Mwenyezi Mungu.”

Na ukataji shauri wake wa maneno kwamba Bi Aisha  hakupinga kuonekana kwa Mwenyezi Mungu kwa hadithi isiyo na sanadi (isiyo na wapokezi) umefuatwa na Ibn Khuzaimah, kwani yeze katika faslu ya tawhid kutoka katika *Sahih* yake, amesema: “Ukanushaji haupelekei elimu, na wala Bibi Aisha hakueleza kwamba Mtume ﷺ alimpa habari kuwa hakumuona Mola Wake, na hakika aliiatsiri Aya.” Nalo ni jambo la kushangaza!! Hakika lime-thibiti hilo kutoka kwake katika *Sahih Muslim*<sup>33</sup> ambayo ameitolea maelezo Sheikh!<sup>34</sup> Na kwake yeze ni kutoka katika njia ya Daud

<sup>31</sup> Katika *Sharhu Sahih Muslim*, Juz. 3, uk. 9.

<sup>32</sup> Amesahau Sheikh Nawawi  kwamba hadithi yake ni marfuu iliyopokewa kutoka kwa Mtume ﷺ katika *Sahih Muslim* hiyo hiyo ambayo ameifafanua Sheikh Nawawi.

<sup>33</sup> *Sahih Muslim*, Juz. 1, uk. 159 -177.

<sup>34</sup> Yaani kwa Sheikh Imam Nawawi.

bin Abi Hind kutoka kwa Shaabi kutoka kwa Masruuq, katika njia iliyotajwa Masruuq anasema: “Na nilikuwa nimeegemea basi nikaka ni kasema: Je, Mwenyezi Mungu hajasema: ‘Na hakika alimuona mara nyingine?’ Akasema Bi. Aisha ﷺ: Mimi ni wa mwanzo katika umma huu niliyemuuliza Mtume ﷺ kuhusu hilo, akasema: ‘Hakika huyo ni Jibrail.’” Na ameieleza hiyo Ibn Mardawayhi kutoka katika njia nyingine kutoka kwa Daud kwa sanadi hii, akasema: “Mimi ni wa mwanzo niliyemuuliza Mtume ﷺ kuhusu hili ni kasema: Ewe Mtume! Je, umemuona Mola Wako Mlezi? Akasema: ‘Hapana, hakika nimemuona Jibrail akishuka.’”] Yameisha maneno ya Hafidh Ibn Hajar kutoka katika kitabu chake *Fat'hul-Bari*.

### **Kutaja yaliyopokewa kutoka kwa Ibn Abbas ﷺ kuhusu hilo:**

Tunaloamini na kuitakidi kuhusiana na hayo ni kuwa Ibn Abbas ﷺ alinukuu hilo kutoka kwa Kaab Akhbar na wapokezi wakadhani kwamba ni kauli na maneno ya Ibn Abbas ﷺ bila kujua kuwa yeye ameyanukuu maneno hayo kutoka kwa Kaab Akhbar kwa njia ya ngano za kale. Na jambo hili linapatikana na lipo hata kwa mwiningine mionganini mwa Masahaba!

Katika kitabu *Siyaru Aalam Nubala*, Juz. 2, uk. 606, na *Bidayat Wan-Nihayat*, Juz. 8, uk. 109, kutoka kwa Basar bin Said (naye ni mionganini mwa wakubwa wa kizazi kilichokuja baada ya masahaba, na ni mionganini mwa wapokezi wa sunna), amesema: Muogopeni Mwenyezi Mungu na hifadhini hadithi. Basi naapa kwa Mwenyezi Mungu, hakika mmetuona tukikaa na Abu Huraira akihadithia hadithi kutoka kwa Mtume ﷺ, na akitusimulia Kaab Akhbar. Kisha akisimama, na akaongeza: Mara nawasikia baadhi ya wale walio-kuwa pamoja nasi wakifanya ni hadithi za Mtume ﷺ yale waliyyoyasikia kutoka kwa Kaab Akhbar, na wakizifanya ngano za Kaab Akhbar ni kutoka kwa Mtume ﷺ.”

Na hakika yamekuja kutoka kwa Ibn Abbas ﷺ baadhi ya maandiko katika kutafsiri baadhi ya Aya, maandiko ambayo si yenyewe kubaliwa kwa yule mwenye akili. Kati ya hayo ni yale aliyoyapokea Hakim katika kitabu chake *Mustadrak*, Juz. 2, uk. 282, katika maana ya kauli yake (s.w.t):

وَسَعَ كُرْسِيُّهُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ

**“Na elimu Yake imeenea mbingu na ardhi” (2:255).** Kutoka kwa Ibn Abbas ﷺ amesema: “*Kursiyyu* (elimu) ni sehemu za nyayo mbili na Arshi ambayo haukadiriwi uwezo wake.” Hakim amesema: “Hadithi hii ni sahihi kwa sharti la Mashekh wawili japo hawakuiandika.” Ama Dhahabi yeye ameinyamazia.

Na amepokea Ibn Jarir Tabari katika *Tafsir* yake Juz. 3, uk. 9 kwa sanad yake sahihi kutoka kwa Ibn Abbas ﷺ ibara isemayo “Na elimu yake imeenea” akasema: “*Kursiyyu* ni elimu Yake.”

Na linalofaa kusemwa ni kwamba rai ya Ibn Abbas ﷺ ni ile iliyokuja katika riwaya ya Ibn Jarir. Na ama yale yaliyokuja katika riwaya ya Hakim na wengineo kwamba hiyo ni sehemu ya nyayo mbili; ima Ibn Abbas ﷺ amesingiziwa na kuzushiwa, na ima ni yale aliyoyataja na kuyapokea Ibn Abbas ﷺ kutoka kwa Kaab Akhbar, akayataja kwa njia ya kushangaa au kudharau au kukebehi fikra hii potofu yenyewe kuanguka na isiyofaa katika upande wa Maula aliyetukuka, wala haisihi kunasibishwa na Ibn Abbas ﷺ na kuwa hiyo ni itikadi yake!

Kisha nimekuta katika kitabu *Sahih Muslim*, Juz. 2, uk. 1027, na 1407 kwamba bwana wetu Ali ﷺ ambaye ni lango la Jiji la elimu<sup>35</sup>

<sup>35</sup> Imethibiti kwamba Bwana wetu Mtume ﷺ amesema: “Mimi ni mji wa elimu na Ali ni lango lake.” Hadithi hii ni sahihi iliyothibiti, amepokea Hakim katika kitabu *Mustadrak* juz. 3, uk. 127 na Twabarani katika kitabu *Mujamul-Kabiir* Juz. 11, uk. 65 na *Tirmidhiy* Juz. 5 uk. 637/3723 na Abu Naiim katika kitabu *Hilyat* Juz. 1 uk. 64 na

alimwambia Ibn Abbas ﷺ: "Hakika wewe ni mtu mbabaishaji..."<sup>36</sup> katika kadhia ambayo Ibn Abbas ﷺ aliitolea fatwa, na hili lin-afidisha kwamba muda mwininge alikuwa akinukuu au akitoa fatwa mbali mbali zisizokubalika.<sup>37</sup> Na amepokea Hakim katika kitabu *Mustadrak*, Juz. 2, uk. 103, kwamba hakika bwana wetu Ali علیہ السلام alisema kumwambia Ibn Abbas ﷺ: "Unafutu mas'ala ya watu bila elimu?!"

Na yaliyonukuliwa kutoka kwa Ibn Abbas ﷺ kutokana na kauli yake kuwa "Mtume Muhammad alimuona Mola Wake Mlezi kwa moyo wake mara mbili" ni yenye kupingwa na kukataliwa hayasihi wala hayafai kuyafanya hoja kama ifuatavyo:

1. Hakika mtiririko wa Aya tulizozieleza kwa marefu na mpana hapo kabla unajulisha kwamba makusudio ya hilo ni bwana wetu Jibrail عليه السلام na sio Mola Mlezi Mtukufu (s.w.t), kwa sababu Mwenyezi Mungu (s.w.t) hayuko katika upeo wa mbali wa macho ulio safi, kwani Mwenyezi Mungu ametakasika na kuepukana na kuwa katika mahala fulani na

---

Khatwiib Baghdadi katika *Taariikh* yake Juz. 11 uk. 48-49 na Ahmad bin Hanbali katika kitabu *Fadha'il Sahaba* Juz. 2 uk. 634/1081 na Daarmii katika kitabu *Musnad Firdaus* Juz. 1, uk. 43-44 na vinginevyo.

Na hadithi ni sahihi iliyothibiti: Amekubali usahihi wake Yahya bin Muiin kama ilivyo katika tarjuma ya Abi Swalt kutoka katika kitabu *Tahdhibbul-Tahdhib*, Juz. 6, uk. 285 na *Tariikh Baghdadi* Juz. 11, uk. 49 na *Tahdhibul-Kamaal* Juz. 18 uk. 77, kama alivyokubali usahihi wake Hafidh ibn Jarir Twabari katika kitabu chake *Tahdhibul-Athaar* katika Musnad bwana wetu Ali علیہ السلام uk. 104 hadithi ya 8 namna amesema: "Habari hii ni sanad yake ni sahihi" na kama alivyokubali usahihi wake Hakim katika kitabu *Mustadrak* Juz. 3, uk. 127; na vivyo hivyo Hafidh Swalih Din bin Kalkalidi Alaai katika kitabu chake *Naqdu Sahih*, hadithi ya 18; na Hafidh Ibn Hajar Asqalaani kama alivyotaja hilo Hafidh Suyuuri katika kitabu *Kaalai Masnuua* Juz. 1, uk. 334, na kama alivyokubali usahihi wake Hafidh Sakhaawi katika kitabu *Makaswid Hasanat* hadithi ya 189.

<sup>36</sup> Hakika ametoo andiko Hafidh Ibn Hajar katika *Fat'uhul-Bari*, Juz. 9 uk. 168 juu ya hilo.

<sup>37</sup> Na mfano wake ni yale yaliyokuja katika kitabu *Sahih Muslim* 1472 katika suala la Talaka hakika baba Swahbaau akamwambia Ibn Abbas ﷺ: [Nipe kutoka habari yako] yaani kutokana na habari yako na mambo yako ya kushangaza.

kuwa karibu na mahala fulani wala kuteremka, kwani hii ni sifa kati ya sifa za wenyewe miili (yaani viumbe).

2. Hakika kauli hii ni ya Sahaba, na ni yenye kupingwa na hadithi isiyio na sanadi, nayo ni kauli ya Bibi Aisha ﷺ: “Mimi ni wa mwanzo katika umma huu niliyemuuliza Mtume 8 kuhusu hilo, akasema: Hakika yeye ni Jibrail.” Nayo ni sahihi imethibiti katika *Sahih Muslim* na vitabu vinginevyo.
3. Hakika yupo aliyemkubali na kumuafiki Bibi Aisha ﷺ juu ya hilo, kama vile Ibn Mas’ud kama ilivyo katika Bukhari na Muslim. Na kundi la watu wa kizazi kilichokuja baada ya Masahaba ambao ni watu wa tafsiri wametaja hilo.
4. Hakika Imam Muslim alipopokea kutoka kwa Ibn Abbas ﷺ hakuongeza ibara ya kumuona Mwenyezi Mungu (s.w.t), na hakika ameipokea 176 kwa tamko: “Amemuona kwa moyo wake.” Na kwa tamko “Amemuona kwa moyo wake mara mbili.” Na hakusema: “Kamuona Mola Wake Mlezi kwa moyo wake.” wala “Kamuona Mola Wake kwa moyo mara mbili.” Na imetangulia kwamba maana ya Aya inayosema: “Moyo haukusema uongo uliyooyaona” (53:11) Mtume aliona kwa macho yake yaani hakika Mtume ﷺ alimuona bwana wetu Jibrail ﷺ kwa sura yake ya asili au halisi kwa macho yake na akamtambua kwa moyo wake na wala hakuwa na shaka katika yale aliyoyna yeye.<sup>38</sup>

Basi inategemewa kuwa Ibn Abbas ﷺ alimaanisha hilo, yaani Jibrail ﷺ, basi wakaongeza baadhi ya wapokezi katika maneno yake na wakaongeza neno ‘Mola Wake Mlezi!’ Na hakika ametaja

<sup>38</sup> *Tafsir Bahru Muhit*, Juz. 10 uk. 11.

Muslim kauli ya Ibn Abbas ﷺ hii baina ya kauli tatu za Masahaba, wote wanasema kwamba alimuona Jibrail ﷺ.

1. Imetangulia kwamba Ibn Abbas ﷺ amenukuu hilo kuto-ka kwa Kaab Akhbar, na Mayahudi walikuwa wakiitakidi hivyo na wakimuomba bwana wetu Musa عليه السلام kama alivyosema Mwenyezi Mungu (s.w.t) hakika wao walimwambia bwana wetu Musa “Tumuone Mwenyezi Mungu wazi wazi.” Na huko zipo hadithi ambazo wamejaribu baadhi yao kutia nyongeza katika hadithi ambayo imepokewa kutoka kwa Ibn Abbas ﷺ, na kwamba hiyo ni katika hadithi isiyo na sanadi na iliyopokewa kutoka kwa Nabii ﷺ na hili ni kosa la wazi.
2. Hakika amepokea Ahmad bin Hanbali katika kitabu chake *Musnad* Juz. 1, uk. 285, kutokana na njia ya Hamad bin Salama, kutoka kwa Qitadah kutoka kwa Akrama, kutoka kwa Ibn Abbas ﷺ amesema: Mtume ﷺ amesema: “Nimemuona Mola Wangu Mlezi aliyetukuka.”

**Nasema:** “Hadithi hii haihusiani na suala hili na timilisho la hadithi ni: Juudan mtanashati juu yake kipo kidani chekundu.” Vivyo hivyo, ndivyo ilivyo kwa sanad hiyo hiyo ya Ahmad bin Hanbali katika kitabu cha Kamil bin Uday Juz. 2, uk. 677.

Na ana tamko lingine huko, nalo ni: “Hakika Muhammad alimuona Mola Wake Mlezi katika sura ya kijana mtanashati bila ya stara kutokana na lulu, nyayo zake au akasema miguu yake ipo katika viatu vya kijani.”

Na haya kama ilivyotangulia, ni yenye kujulikana kutokana na sentensi potofu zenyе kupokewa juu ya jambo hili kutoka kwa Ibn Abbas ﷺ kwa njia ya Hamad bin Salama! Na lipi litakujuli-

sha wewe ni nani Hamad bin Salama! Basi Ahmad bin Hanbali au yule aliyeibuni na kuiweka hadithi husika na kuchakachua katika sanad yake amepunguza upande mmoja wa hadithi na kufuta upande mwingine. Na huko ni kushindwa kwake! Basi amkeni, zindukeni na jueni kosa la kauli ya Dhahabi katika kitabu *al-Uluwu*: “Sanad yake ni yenye nguvu”!! Na hakika tumemjibu huko na tumbainisha kwamba imebuniwa na kusingiziwa bwana wetu Mtume Muhammad ﷺ.

### **Yale Yaliyopokewa Kutoka kwa Bwana Wetu Abu Dharr Katika Mada Hiyo**

[Angalizo muhimu mno na ukamilisho wa maudhui]: Na miongoni mwa yaliyonukuliwa kutoka kwake ni kauli ya kuthibiti sua-la la Bwana wetu Mtume Muhammad ﷺ kumuona Mwenyezi Mungu (s.w.t) kwa maelezo ya Abu Dharr na Anas bin Malik. Na ama Abu Dharr, amepokea Nasai katika kitabu *al-Kubra*, Juz. 6, uk. 472, na 11536, kutokana na njia ya Hakam bin Aban, kutoka kwa Zayd bin Sharik, kutoka kwa Abu Dharr amesema: “Mtume ﷺ alimuona Mola Wake Mlezi (s.w.t) kwa moyo wake na hakumuona kwa macho yake.” Na hili ni dhaifu kwa sababu ya Hakam bin Aban.

Na ama bwana wetu Anas bin Malik basi amepokea Ibn Khuzaimah, katika kitabu *Tawhid*, uk. 199 na Ibn Abi Aswim nambari 432, kutokana na njia ya Abu Bahr Abdul-Rahman bin Uthman Bakrawi kutoka kwa Shuuba, kutoka kwa Qatadah, kutoka kwa Anas bin Malik amesema: “Hakika Mtume Muhammad ﷺ alimuona Mola Wake Mlezi aliyetukuka.” Na hii ni yenye kukataliwa. Imewekwa na kuchomekwa, kwani Bakrawi ni mharibifu, na la kushangaza kutoka kwa Hafidh Ibn Hajar ni alivyosema katika kitabu chake *Fat'hul-Bari*, Juz. 8, uk. 608: “Ni sanad yenye nguvu.”!!

Na mimi ninayo maangalizo mawili kuhusiana na sanad hii:

**La kwanza:** Hakika Bakrawi huyu ni Abdul-Rahman bin Uthman bin Umayya bin Abdul-Rahman ibn Abu Bakra Thaqafi. Na Abu Bakra ni sahaba mweusi ambaye alikuwa mtumwa wa Thaqif na alisilimu katika vita vya Hunayn, na jina lake ni Nufay'i bin Harith, naye ni mionganoni mwa watetezi wa Bani Umayya, naye ni Yule uliyekataliwa ushahidi wake katika zama za bwana wetu Umar bin Khatwab رضي الله عنه. Umar رضي الله عنه alikataa ushahidi wake dhidi ya Mughira bin Shuuba katika tuhuma ya uzinifu. Basi akabatilisha ushahidi wake na akamchapa mijeledi. Angalia wasifu wake katika vitabu vya wasifu wa wapokezi.

Na mjukuu wake Abu Bahr, Dhahabi katika kitabu *Diwanul-Dhuafai* amesema kumhusu: “Waliacha hadithi yake” na Ahmad bin Hanbali akasema: “Watu waliitupilia mbali hadithi yake.” Na Ibn Hajar katika kitabu *Mujruhina*, Juz. 2, uk. 61 amesema: “Ni mionganoni mwa wenyewe kukataliwa hadithi zao. Ni mionganoni mwa wanaogeza na kubadili hadithi kutoka kwa watu thabiti...” Na angalia wasifu wake katika kitabu *Tahdhibul-Kamaal*, Juz. 17, uk. 271.

**Na angalizo la pili:** Hakika Qatadah ameleta mkanganyiko katika hadithi hii!! Wakati fulani anaipokea kutoka kwa Anas bin Malik na wakati mwingine kutoka kwa Abi Dharr, na muda mwingine kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنه!! Wala hatujui hili linatoka kwake au kutoka kwa mwingine!! Basi zingatia!! Sheikh wetu Sayyid Abdul-Aziz ibn Mas'ud katika kitabu chake *Al-Qaul Asad Fii Bayaan Haal Hadith Raaytu Rabbi Fii Suurati Shaab Amrad*, amesema:

“Qatadah ni mzushi mashuhuri kwa kazi hiyo, ametajwa na Al Hafidh katika kitabu *Tabaqat thalitha min tabaqat tadliis*.<sup>39</sup> Na Shuu-

<sup>39</sup> Tazama kitabu *Taarif Ahlu Taqdiis Bimaratisul Mawsuufina bi Tadriis* cha Hafidh Ibn Hajar uk. 102. Chapa ya Darul Kutubil-Ilmiyyah, mwaka 1405 (A.H.), naye ni katika wenyewe daraja kubwa na tabaka ya tatu ambao Ibn Hajar amewataja kuwa: “Ni katika

ba amesema: "Nilikuwa nauangalia mdomo wa Qatadah anaposema: 'Ametuhadithia' naandika, na asiposema hivyo mimi siandiki. Na hapa hajasema 'Ametuhadithia,' si katika njia hata moja mionganoni mwa njia za Hadithi hii, na jambo hilo lafanya tujizuiue kuichukua kutoka kwake mpaka idhihiri kutoka kwenye njia nyingine kwamba ameisikia kutoka kwa Ikrimah, kama ilivyo kaida katika upokezi wa mwenye kuzusha."

Kimebakia kitu kimoja hapana budi kukitolea tanbihi, nacho ni kuwa, itikadi ya kumuona Mwenyezi Mungu (s.w.t) inajikita zaidi kwa wale wanaojifanya masufi au baadhi ya masufi, na malengo yao yote kutohana na utajo wa Mwenyezi Mungu na ibada ni ili wamuone na wamuangalie Yeye! Hivyo ndivyo walivyoweza masheikh wao kuingiza fikra vichwani mwao na zikakinai nafsi zao! Basi wao ni wenyе kuendelea na madai yao ya kipuuzi kwamba Mwenyezi Mungu ataonekana na kwamba mawali watamuona Yeye kwa hakika na sio majazi wala hapotei machoni mwao hata punde, na wao wanafanya taqiyya katika itikadi hii wala hawasemi kinaga ubaga kuhusu hilo ila kwa wale wanaowaamini! Na hudhihiri wakati mwingine matelezo ya ndimi zao na katikati ya majibizano na majadiliano pamoja nao!

Na wengi mionganoni mwa watu hao wanangojea na kudhani kuwa si muda mrefu Yeye ataondoa kizuizi kwao na watamuona moja kwa moja, na huku ndio kufika kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) ambaye wanamuwazia!! Na wengi wa watu hawa hawafahamu dalili wala njia za utoaji dalili, bali wanashika huku na huku na wanadhani kwamba wao wanajua mambo na wanafahamu hayo kwa uwekaji wazi au kwa upokeaji kutoka kwa Mola wao!! Na kuhusu hilo ipo kauli ya baadhi yao isemayo: "Mimi ninapokea kutoka

---

waliozusha sana, maimamu hawakutolea hoja Hadithi zao, kuna waliozikataa kabisa, na kuna waliowakubali."

moyoni mwangu kutoka kwa Mola Wangu, na nyinyi mnachukua elimu kutoka kwa wafu na sisi tunachua hilo kutoka kwa aliye hai ambaye hafi.”<sup>40</sup>

Na lengo la kutoa tanbihi hii juu ya fikra hii ni kutaka kuon-esha kuwa baadhi ya wanazuoni na waandishi wa upande wa tawhidi waliathirika na mawazo hayo, na hivyo pale walipozungumza ndani ya vitabu vya Tawhid na imani na itikadi juu ya suala la je, Mtume wetu alimuona Mwenyezi Mungu usiku wa Israi au la, wakadhani kuwa wanazuoni wengi wanaona kuwa Mtume ﷺ alimuona Mola Wake Mlezi usiku wa Israi!! Na maneno haya sio sahihi kwa mitazamo ifuatayo:

Hakika wafasiri wengi katika kufasiri kauli yake (s.w.t) isemayo: “Na hakika alimuona mara nyingine” wametaja: Hakika wanazuoni wengi wanashika kauli ya kuwa hakika ye ye alimuona Jibrail, na hilo ni kutohana na kauli ya Hafidh Abu Hayyan katika kitabu chake *Al-bahrul-Muhit*, Juz. 10, uk. 10, ambapo amelisema hilo mahala pengi ikiwemo kauli yake: “Na kwa mujibu wa kauli ya wanazuoni wengi ni kwamba ‘Basi akatulia’ yaani Jibrail katika anga ‘Naye katika upeo wa mbali wa juu kabisa’”.

Na mwenye kufuabilia maneno ya wanazuoni katika vitabu vya tafsiri atakuta kwamba kauli nyingi za wanazuoni waliotajwa huko mionganini mwa masahaba na kizazi kilichokuja baada ya masahaba na wafuasi wao wanasema kwamba ye ye ﷺ alimuona bwana wetu Jibrail na hakumuona Mwenyezi Mungu, ambapo wamefasiri kuwa aliyeonwa na ambaye aliyekaribia umbali wa pinde mbili, au karibu zaidi, ni bwana wetu Jibrail. Bali hakika sisi tunakuta mfano katika kitabu *Fat'hul-Bari* kwamba wale walioikataa na kuipinga hadithi ya Sharik bin Abi ni wanazuoni wengi.

<sup>40</sup> Na huko kuna maneno ya thamani kubwa katika maudhui hii katika kitabu *Fat'hul-Bari*, Juz. 1 uk. 221 mwishoni mwa ufanuzi wa hadithi ya 122 katika kitabu *Sahih Muslim*.

Hivyo basi kauli ya kwamba wengi walikuwa wakiona kwamba Mwenyezi Mungu alionekana usiku wa Israi si sahihi, na ni kosa haya lililoenea kama vile liliivoenea dai la kuwa watangulizi wa mwanzo walikuwa wakimwachia mambo yote Mwenyezi Mungu lakini waliokuja baada yao wamekuwa wakiawili mambo! Na uk-weli ni kinyume na hivyo, hakika tafsiri ya Ibn Jarir Tabari aliyekufa mwaka 310 A.H ambaye aliiita *Jamiul-Bayaan Anitaawil Ayatil-Qur'ani*, na vinginevyo mionganoni mwa vitabu vyatya wanazuoni wa zamani vyatya hadithi na tafsiri vimejaa taawili mbalimbali walizozinukuu kutoka kwa watangulizi wa mwanzo, na hakika tumenukuu sehemu ya taawili hizo katika utangulizi wa kitabu *Sahihu Sharhul-Aqidat Twawiyat*, na katika utangulizi wa kitabu *Daf'u Shabhi Tashbih Biakuffi Tanzih*, na Mwenyezi Mungu ndiye mwafikishaji.

### **Katika Hadithi ya Abu Dharr: ‘Ni Nuru, Nitamuonaje?’**

Hadithi ya Abu Dharr ameipokea kutoka kwa Mtume ﷺ amesema: “Ni nuru nitamuonaje?” au “nimeiona nuru” ni dalili juu ya Mtume ﷺ kutomoona Mwenyezi Mungu (s.w.t). Ameipokea Muslim katika *Sahih* yake Juz. 1, uk. 161 na 178 kutoka kwa Abu Dharr ؓ amesema: Nilimuuliza Mtume ﷺ Je, ulimuona Mola Wako Mlezi? Akasema: “Ni nuru nitamuonaje?”

**Nasema:** Hadithi hii pia inatubainishia sisi kuwa sio Bibi Aisha ؓ peke yake aliyemuuliza Mtume ﷺ kuhusiana na kadhia ya kumuona Mwenyezi Mungu na akabainisha ﷺ kwamba haku-muona Mwenyezi Mungu!! Na hakika amapatia Imam Nawawi katika ufanuzi wa hadithi hii aliposema ؓ akinukuu kutoka kwa baadhi ya wanazuoni huko katika kitabu *Sharhu Sahih Muslim*, Juz. 3, uk. 12:

“Na ama kauli yake ﷺ: ‘Ni nuru nitamuonaje?’ maana yake ni hijabu yake ni nuru nitawezaje kumuona? Imam Abu Abdullah Maazari رضي الله عنه amesema: “Anamkusudia Mungu, hivyo maana yake ni kwamba nuru imenizuia mimi kumuona kama ilivyojiri kawaida ya nuru kuyafunika macho na kuyazuia kukifikia kile kilichopo baina ya muonaji na chenye nuru.”

Na kauli yake ﷺ: “Nimeiona nuru” maana yake: Nimeiona nuru na sikuona kitu kingine. Amesema: Na imepokewa “Nimeiona nuru...” Qadhi Ayadhi رضي الله عنه amesema: “Hadithi hii haikupatikana kwetu sisi wala sijaiona katika chochote mionganini mwa misingi, na ni muhali dhati ya Mwenyezi Mungu iwe ni nuru; kwani nuru ni katika miili na Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametukuka na hilo na haya ni madhehebu ya Maimamu wa Kiislamu....”

**Nasema:** Maneno haya nimeyaleta ili akinai kwayo yule asiyekinai ila kwa nukuu za maulamaa na kauli zao, wala haipi nafasi akili na ufahamu wake ambao Mwenyezi Mungu amemzawadia yeye ili afahamu haki! Kinyume na hivyo ni kwamba hadithi ya Abu Dharr hii iliyomo katika *Sahih Muslim* haisihi kwetu, na hakika ameponda usahihi wake Ibn Khuzaima, na hakika nimeeleza kwa marefu na mapana juu ya hilo katika maelezo yangu juu ya kitabu *al-Uluwu*, andiko 214.

Na vivyo hivyo inabainika kwamba Bwana wetu Mtume ﷺ hakumuona Mwenyezi Mungu (s.w.t) usiku wa Miraj; na uhakika ni ule uliosemwa katika Surat an-Najm:

لَقَدْ رَأَىٰ مِنْ آيَاتِ رَبِّهِ الْكُبْرَىٰ

**“Hakika aliona katika ishara kubwa za Mola Wake Mlezi.”**  
**(53:18).** Na aya za Mwenyezi Mungu ni viumbe Vyake na maajabu ya vitu alivyovitengeneza, na kati ya hivyo ni malaika Jibrail عليه السلام ambaye ameumbwa mwenye mabawa mia sita.

## **Kumuona Mwenyezi Mungu (s.w.t) Usingizini ni Muhali**

Mwenyezi Mungu akurehemu, jua kwamba itikadi ya Kiislamu ni haki yenyе maandiko juu yake katika Kitabu na Sunna, na ya masahaba watoharifu. Hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) amesema: “Hana mfano na chochote naye ni msikivu muoni” na pia anasema: “Hafanani na chochote.” Na katika msingi huo hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) hana sura, umbo, umbile, wala hana kiwiliwili wala habadiliki wala hageuki kutoka sura hadi sura nyingine, wala umbile hadi umbile jingine “Utakasifu ni wa Mola Wako Mlezi Mtukufu kwa yale wanayomsifu”.

Na katika msingi huo tunakata shauri kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) haonekani hali ya kuwa mtu akiwa macho au usingizini, na kwamba (s.w.t) amesema: “Macho hayamfikii na Yeye huyafikia macho naye ni Mpole Mwenye habari”. Na ikiwa jambo hili hivyo ndivyo lilitivo basi hapana budi kuangalia katika baadhi ya ushabihishaji na dalili ambazo wanazozipokea baadhi ya watu kuhusu kumuona Mungu usingizini. **Tunasema:**

1. Hadithi ni batili, nayo ni hadithi ya Ibn Abbas ﷺ amesema: Mtume ﷺ amesema: “Alinijia Mola Wangu Mlezi (s.w.t) usiku katika sura nzuri, akasema nilidhani niko usingizini, akasema: Ewe Muhammad! Je, unajua ni kitu gani ambacho malaika hugombania? Nikasema: Hapana. Basi akaweka mkono wake mabegani mwangu hata nikakuta baridi lake baina ya chuchu zangu. Au alisema shingoni mwangu. – Basi nikajua yale ambayo yamo mbinguni na yaliyomo ardhini. Akasema: Ewe Muhammad! Je, unajua ni kitu gani ambacho malaika hugombania? Nikasema: Ndiyo, hugombania matendo yafutayo madhambi, na matendo

hayo yafutayo madhambi ni hali ya kukaa msikitini baada ya Swala, na kutembea kwa nyayo kwenda kushiriki Swala ya Jamaa, na kutia wudhu wakati wa yale yachukizayo...”<sup>41</sup>

Na hakika ameipokea Tirmidhi katika *Sunan* katika hadithi mchanganyiko, kutoka katika hadithi za Ibn Abbas ﷺ, amesema huko: “Ni nzuri na ngeni.” Na pia kutoka katika hadithi za Maadh bin Jabal na baada ya kutaja hadithi hiyo akasema: “Hadithi hii ni nzuri sahihi, na imenukuliwa kutoka kwa Muhammad bin Ismail Bukhari kwamba amesema kuihusu: Ni nzuri na sahihi.”

Na hadithi ni batili yenye kukataliwa, nayo imehusisha aina mbalimbali ya kumfananisha Mola Manani na kufanya ana mwili, tunajilinda na Mwenyezi Mungu kwalo! Ama sanad yake: Hadithi hii imetokea ndani yake migongano, mara nyingine anaipokea Abdul-Rahman bin Aaish Khadhrami kutoka kwa Mtume ﷺ moja kwa moja, na wakati mwingine kutoka kwa Ibn Abbas ﷺ, na muda mwingine kutoka kwa Maadh bin Jabal. Na hakika ameipokea hiyo Ibn Jawzi katika kitabu *Ilal Mutanaahiyat*, Juz. 1, uk. 34, kutoka kwa Maadh bin Jabal na asiyekuwa yeye, na akasema baada ya hadithi hiyo ya bwana wetu Maadh:

“Asili ya hadithi na njia zake ni zenye kugongana, Daru Qutni amesema: ‘Sanad zake zote ni zenye kugongana, hakuna iliyo sahihi. Na hakika ameipokea kutoka kwa Anas bin Malik, na imepokewa kutoka kwa Qata dah kutoka kwa Abi Qilaada kutoka kwa Khalid bin Jalaaj kutoka kwa Ibn Abbas ﷺ, nalo ni kosa. Na lililohifadhiwa ni kwamba Khalid bin Jalaaj ameipokea kutoka kwa Abdul-Rahman bin Aaish, na Abdul-Rahman hakumsikia Mtume ﷺ, na hakika ameipokea kutoka kwa Malik bin Yakhmir kutoka kwa Maadh. Abu Bakri Bayhaqi amesema: Hakika imepokewa kwa njia kadhaa na

<sup>41</sup> Ameipokea Ahmad bin Hanbali katika *Musnad*, Juz. 5 uk. 243, na Tirmidhi katika *Sunan* Juz. 5 uk. 366, na *Twabaraani*, Juz. 20 uk. 109.

zote ni dhaifu.””

Na Hafidh Ibn Hajar katika kitabu *Nukta Dharaaf* kilichochapishwa pamoja na *Tuhfatul-Ashraaf*, Juz. 4, uk. 382, amesema:- Hadithi inasema: “Alinijia Mola Wangu Mlezi katika sura nzuri....”, nikasema: Akasema Muhammad ibn Nasru Muruuzi katika kitabu chake *Taadhiim Qadr Swalaat*: Na hadithi hii wapokezi wake wanagongana katika sanad yake na haijathibiti kwa watu wa maarifa.” Imekwisha.

Na amesema Hafidh Ibn Hajar katika kitabu *Tahdhiibul-Tahdhib*, Juz. 6, uk. 185 katika wasifu wa Abdul-Rahman bin Aaish Khadhrami anayetwa pia Saksi: “Wametofautiana kuhusu uswahaba wake na sanadi za hadithi zake. Imepokewa kutoka kwake hadithi “Nilimuona Mola Wangu Mlezi katika sura nzuri,” na ikasemwa amepokea hilo kutoka kwa mtu kati ya Masahaba. Na ikasemwa amepokea hilo kutoka kwa Malik ibn Yakhamir kutoka kwa Maadh bin Jabal.... Abu Zur’at Damishqi amesema: Nikasema kumwambia Ahmad: Hakika Ibn Jabir anasimulia hadithi kutoka kwa Ibn Jalaaj kutoka kwa Abdul-Rahman bin Aaish hadithi isemayo: Nilimuona Mola Wangu Mlezi katika sura nzuri, na anasimulia kutoka kwa Qatadah, kutoka kwa Abi Qiladah, kutoka kwa Khalid bin Jalaaj, kutoka kwa Ibn Abbas ﷺ? Akasema: Hii sio kitu chochote! Na kauli ni ile aliyoisema Ibn Jabir.”

Yaani hakika kati ya njia zake, iliyso sahihi zaidi ni ile ambayo amepokea Ibn Aaish kutoka kwa Mtume ﷺ kama ilivyokuwa wazi kwa mwenye kuchunguza sanad yake. Na Ibn Aaish hajakutana na Mtume ﷺ, na amehitimisha Tirmidhi maneno juu yake katika kitabu *Sunan* Juz. 5, uk. 369, baada ya kuitaja hadithi ya Maadh aliposema: “Kutoka kwa Abdul-Rahman bin Aaish, kutoka kwa Mtume ﷺ: Na hiyo ni sahihi na Abdul-Rahman... hakusikia kutoka kwa Mtume ﷺ.”

Na ambalo linadhihiri kwangu; hakika maneno ya Tirmidhi ni yenye kugongana katika hadithi hii, na ninadhani uzingatiaji kuwa hadithi hii ni sahihi haujathibiti kutoka kwake, licha ya uwepo wa tamko hilo katika *Sunan* yake.

Na ama kuhusiana na upande wa matini nao ni batili! Kwa sababu ndani yake kuna ushabihisho dhidi ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) na kumfanya ana mwili, na kuwa amemuona kwa sura, ilihali ametukuka Mola Wetu Mlezi kutokana na sura na umbo. Eti na kwamba Yeye ameweka mkono Wake (na katika hadithi nyingine kiganja Chake) baina ya mabega ya Mtume ﷺ. Na kwamba yeye Mtume amekuta ubaridi wake na kwamba mkono huo ni mdogo kiasi kwamba umeenea eneo lililopo baina ya mabega ya Mtume ﷺ, na hakika bwana wetu Mtume ﷺ alijua yale yaliyopo mbinguni na yaliyomo ardhini. Hakika yote hayo ni batili kama nilivyobainisha katika Risala yangu katika kitabu *Aquwalu-Huffadh Manshuurat Fii Bayaan Wadh'u Hadithi Raaytu Rabbi Fii Ahsani Suurat*, kilichochapishwa pamoja na kitabu *Daf'u Shabhi Tashbih Biakuffi Tanzih*.

2. Yale wanayoyaeleza kutoka kwa Ahmad bin Hanbali, kwamba yeye alimuona Mola Mlezi Mtukufu usingizini mara 99, akasema ikiwa nitamuona mara ya mia moja nitamuuliza. Basi akamuona kwa mbali na akamuuliza, akasema: Ewe Mola Wangu Mlezi, ni kwa kitu gani hujikurubisha wanaojikurubisha Kwako? Akasema: Ewe Ahmad kwa maneno Yangu. Akasema: Ewe Mola Wangu Mlezi kwa ufahamu au bila ya ufahamu? Akasema: “Kwa ufahamu na bila ya ufahamu.”

Kisa hiki ni cha uongo hakisihi kabisa! Amekitaja Dhahabi katika kitabu *Siyarul-Aalaam Nubaalai*, Juz. 11, uk. 347 kwa sanad mbili kutoka kwa Ahmad bin Hanbali, na zote hizo mbili zinazunguuka juu ya Ahmad bin Muhammad bin Maqsam, naye ni muongo

kama ilivyo katika kitabu *Lisaanul-Miizan*, Juz. 1, uk. 260.

Na hakika imepatikana katika kisa hiki ziada na nyongeza!! Na kisa amekipokea Khalaal katika kitabu chake *Amaali* katika kikao cha tano kutoka kwa Sheikh wake ambaye Mahufadh wamemtuhumu kwa uongo, huyo Ahmad bin Muhammad ibn Maqsam, kama alivyotaja Dhahabi katika kitabu *Siyaru Aalam Nubalaat*, na hili ni andiko lake:

“Kutoka kwa Abdullah bin Ahmad amesema: ‘Nilimsikia baba yangu akisema: Nimemuona Mola Mlezi Mtukufu usingizini akasema: Ewe Mola Wangu Mlezi ni kipi kilicho bora wanachojikurubisha kwacho wenyewe kujikurubisha? Akasema: ‘Kwa maneno Yangu ewe Ahmad.’ Nikasema: Ewe Mola Wangu Mlezi kwa ufahamu au bila ufahamu? Akasema: ‘Kwa ufahamu na bila ufahamu.’”

Na hakuna katika hadithi hii kama unavyoona kwamba yeche ali muona mara 99!! Kisha hakika hii sio mionganini mwa hoja za kisheria kwa maafikiano. Na sahihi kwetu, bali ambalo tunakata shauri kwalo ni kwamba, tunaona kuwa hayo yote ni upotofu na ni mionganini mwa mapotofu makubwa. Hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) ha onekani usingizini kabisa, kwani Mola Manani hana umbo (shakli), wala sura na sio nuru kwa maana ya mwanga, “hafanani na chochote” na hana anachofanana nacho.” Na lililo maarufu ni kwamba mwenye kusema kuwa alimuona Mola Wake Mlezi usingizini hakika yeche alimuona mtu au sura ya mtu akimzungumzisha na ikapatikana moyoni mwake kwamba huyo ni Mwenyezi Mungu. Na hali hii wanaiita baadhi ya watu kwa jina la hijabu ya sura. Na Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametakasika, hana sura na maumbo kabisa. Na kwa uhakika huyu muonaji anakuwa hajamuona Mwenyezi Mungu. Na yaliyonukuliwa kutoka kwa Ahmad ni uwongo na hayana hoja ndani yake, na kama yamethibiti kutoka kwake. Hukumu hazithibiti kwa ndoto. Baadhi ya watu humuona mtu usingizini na hatimaye inapatikana

nyoyoni mwao, au mawazoni mwao kuwa wamemuona Mwenyezi Mungu (s.w.t). Mungu ameepukana na yote hayo wanayomfikiria nayo na kumsawiri, basi anawazungumzisha wao na wanazungumza naye. Na sisi tuna yakini kwamba huyu mwenye kuonekana sio Mwenyezi Mungu aliyetukuka, ambaye hafanani na chochote. Na linalopatikana hapa ni kwamba, hakika sisi tunasema hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) haonekani usingizini kabisa.

**Maneno ya Nawawi na Bajouri Katika Suala la  
Kuonekana kwa Mwenyezi Mungu na Ubainifu  
Ambao Unaonesha Udhaiju na Kosa**

Imam Nawawi رضي الله عنه katika kitabu *Sharh Sahih Muslim*, Juz. 3, uk. 5 amesema:

“Na ama mwandishi wa kitabu *Tahriru* kwa hakika amechagua kuonekana kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t), amesema: “Na hoja katika suala hili na hata kama zikiwa nyangi lakini sisi hatushikamani nazo ila zile zilizo na nguvu zaidi, kati ya hizo ni hadithi ya Ibn Abbas رضي الله عنه: ‘Je, mnastaajabu urafiki wa Nabii Ibrahim صلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ kwa Mola Manani; na Mola Muumba kusema na Musa صلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ, na suala la Mtume Muhammad صلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ kumuona Mwenyezi Mungu.’ Na kutoka kwa Akrama alimuuliza Ibn Abbas رضي الله عنه je, Muhammad صلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ alimuona Mola Wake Mlezi? Akasema: Ndiyo.

“Na hakika imepokewa kwa sanad isiyokuwa na shaka kutoka kwa Qatadah, kutoka kwa Anas bin Malik رضي الله عنه amesema: Muhammad صلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ alimuona Mola Wake Mlezi. Na alikuwa Hasan akiapa kwamba hakika Muhammad صلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ alimuona Mola Wake Mlezi. Na asili katika mlango huu ni hadithi ya Ibn Abbas ambaye ni wino wa umma na marejeo kwake katika mambo mugumu, na hakika amerejea yeye Ibn Umar رضي الله عنه katika suala hili na aliyempeleka yeye akamuuliza: Je, Mtume Muhammad صلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ alimuona Mola Wake

Mlezi? Basi akampa habari kuwa yeye alimuona.

“Wala hadithi ya Bi. Aisha ﷺ haiwezi kutia dosari hili, kwa sababu Bi. Aisha ﷺ hakutoa habari kwamba yeye alimsikia Mtume ﷺ akisema: ‘Sijamuona Mola wangu Mlezi.’ Bali hakika ametaja yaliyotajwa akiawili maneno ya Mwenyezi Mungu (s.w.t): ‘Na haikuwa kwa Mwenyezi Mungu aseme na kiumbe ila kwa wahyi au nyuma ya pazia au amtume mjumbe.’ Na kauli yake (s.w.t): ‘Macho hayamfikii’ na sahaba akisema kauli na akatofautiana naye mwininge mionganoni mwao kauli yake haitakuwa hoja. Hivyo zikisihi riwaya za Ibn Abbas katika kuthibitisha uonekano wa Mwenyezi Mungu itawajibika kufuata muelekeo wa kuthibitisha hilo, kwani hilo sio mionganoni mwa yale ambayo akili inayadiriki, inayafikia na kuyachukua kwa dhana, bali hayo yanachukuliwa kwa kusikia, wala hakuna ye yote anayeruhusu kumdhania Ibn Abbas ﷺ kuwa amezungumza suala hili kwa dhana na ijithadi.

“Na hakika amesema Muamar bin Rashid, pindi alipotaja kuhitilafiana Bi. Aisha ﷺ na Ibn Abbas ﷺ: ‘Bi. Aisha ﷺ kwetu sisi sio mjuzi zaidi ya Ibn Abbas ﷺ.’ Kisha hakika Ibn Abbas ﷺ amethibitisha kitu walichokikanusha wengine, na kinachothibitishwa hutangulizwa juu ya kile kinachokanushwa.” maneno haya ni ya mwandishi wa kitabu cha *Tahrir*.

“Matokeo ni kwamba hakika wanazuoni wengi wanaamini Mtume ﷺ alimuona Mola Wake Mlezi, yaani kwa macho mawili ya kichwa chake usiku wa Israi na Miraj, kwa hadithi ya Ibn Abbas ﷺ, na nyinginezo mionganoni mwa zile zilizotangulia, na uthibitisho huu hawauchukui ila kwa kusikia kutoka kwa Mtume ﷺ, hili ni mionganoni mwa yale ambayo hayapaswi kutiliwa shaka kwayo.

“Kisha hakika Bibi Aisha ﷺ hakukanusha kuonekana kwa Mwenyezi Mungu kwa hadithi kutoka kwa Mtume ﷺ, na lau

angekuwa na hadithi kuhusu hilo angeitaja, na hakika alitegemea kung'amua hukmu kutohana na Aya mbalimbali, nasi tutabainisha jibu lake.

“Ama Bibi Aisha ﷺ kutumia kauli ya Mwenyezi Mungu “Macho hayamfikii” kuwa ndio dalili, jibu lake liko dhahiri kwani kudiriki ni kuzingira, na Mwenyezi Mungu (s.w.t) hazingirwi, na likipatikanana andiko linalokanusha kuzingira hailazimu kutohana na andiko hilo kukanusha uonaji bila ya kuzingira. Na nitajibu Aya kwa majibu mengine hakuna haja ya kuyaeleza baada ya kutaja hayo....”

### **Kauli ya Bajuuri Katika Kitabu *Sharhul- Jawharat na Mjadala Wake***

Allama Bajuuri katika kitabu chake *Sharhul-Jawharat*, uk. 117, amesema:

Kauli yake “Na kwa mwenye kuchagua dunia umethibiti” yaani umepatikana uonekanaji wake (s.w.t) duniani na akhera, duniani usiku wa Israi, na mchaguaji ni Mtume wetu Muhammad ﷺ. <sup>42</sup> Na katika neno ‘Mukhtari’ kuna maana kwamba yeye <sup>صلی اللہ علیہ وسّع آنہ مکان</sup> alich-aguliwa kwa ajili ya heshima hii. Na lenye nguvu kwa wanazuoni wengi ni kwamba hakika yeye <sup>صلی اللہ علیہ وسّع آنہ مکان</sup> alimuona Mola Wake Mlezi (s.w.t) kwa macho yake mawili ya kichwa chake yakiwa sehemu yake, ambapo ni tofauti ya yule aliyesema: Yaligeuzwa na kuwa moyoni kwake, kwa ushahidi wa hadithi ya Ibn Abbas رض na wen-gineo.

Hakika Bi. Aisha رض alikanusha kutokea hilo kwa Mtume <sup>صلی اللہ علیہ وسّع آنہ مکان</sup> lakini ametangulizwa juu yake Ibn Abbas رض, kwa sababu yeye ni mwenye kuthibitisha. Na kanuni inasema hakika kithibitishacho hutangulia juu ya kile kikanushachcho, hadi Muamar bin Rashid akase-

<sup>42</sup> Na hili linabainisha ubatili wake, kwani chanzo chake ni Kaab Akhbar, na yeye ni mwenye kutofautiana na maandiko!!

ma: ‘Bi. Aisha ﷺ kwetu si mjuzi zaidi ya ibn Abbas ﷺ, na صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ alikuwa akimuona Mola Manani (s.w.t) mara kwa mara.’”

Na kutokana na maneno ya Ibn Wafaa: ‘Hakika hali ya Nabii Musa عليه السلام ya kumrudisha Mtume ﷺ kuhusiana na swala bila shaka urudiaji huo ulikuwa ni kushuhudia nuru mara nyingi.’ Na akaghani shairi akisema:

Na siri katika kauli ya Musa pindi alipomrudisha yeye ili idhihiri nuru kwake aishuhudie – unadhihiri ung’ajji juu ya uso wa Mtume, uzuri ulioje Ewe Mwenyezi Mungu, alirudia hivyo Mtume.

Basi hekima juu ya hilo ni: Kupata nuru kutoka kwenye uso wake ﷺ, na kila mara nuru iliongezeka. Na hekima ya dhahiri ni: Kufanyiwa tahfifu.

Na kuna ikhtilafu kuhusu kuonekana Kwake kwa mawalii. As-hairah wana kauli mbili, iliyo na uzito kati ya hizo mbili ni ile ya kukataza. Na haki ni kwamba haijathibiti duniani ila kwake yeye ﷺ, na mwenye kudai hilo asiyekuwa yeye, duniani akiwa macho, basi amepotea kulingana na masheikh ambao wamekwenda baadhi yao hadi katika kumkufurisha.

Allamah Qawnawi amesema: “Ikiwa itasihi kutoka kwa mmoja kati ya wenyе kuzingatiwa kuwa hilo lilitokea, basi itatakiwa kufanyiwa taawili. Na hiyo ni kwa kuwa hali zinazokithiri hufanya ghaibu kuwa ni hadhiri, hasa mwenye kukithirisha kushughulika na siri ya kitu, huwa kitu hicho kana kwamba kimehudhuria mbele yake, kama vile kinajulikana kwa kila mmoja.” Yamekwisha maneno ya Qawnawi.

Yote haya ni katika kumuona Yeye (s.w.t) hali akiwa macho.

Na ama kumuona Yeye (s.w.t) usingizini inanukuliwa kutoka kwa Qadhi Ayyadh kwamba, hakika katika hilo hakuna mzozo ka-

tika utokeaji wake na usahihi wake, kwani Shetani hajifananishi na Mwenyezi Mungu (s.w.t) kama vile Mitume ﷺ. Na akataja mwiningine tofauti na hivyo. Na wakasema baadhi yao: Hakika Shetani ana-jifananisha na Yeye na sio Mtume,<sup>43</sup> na tofauti ni kwamba Mtume ni kiumbe hivyo kujifananisha na yeye kunapelekea kuchanganya watu, ambapo ni tofauti na Mola Manani, Yeye jambo lake linajulikana.<sup>44</sup>

Na wakasema baadhi yao: Wala hajifananishi na malaika, wala na jua, wala mwezi, wala nyota zinazoangaza, wala mbingu ambayo yenye mawingu. Na imeelezwa kwamba Imam Ahmad alimuona Maula Manani (s.w.t) usingizini mara 99 na akasema: Ikiwa nitamuona mara ya mia moja nitamuuliza, basi akamuona na akamuuliza, akasema: Ewe Mola Wangu Mlezi, ni kwa kitu gani hujikurubisha nacho wanaojikurubisha Kwako? Akasema: Kwa kusoma maneno Yangu. Akasema: Ewe Mola Wangu Mlezi, kwa ufahamu au bila ya ufahamu? Akasema: “Kwa ufahamu na bila ya ufahamu.”

Na mwonekanaji akiwa katika sura ambayo si muhali Kwake Yeye Mungu basi jua huyo ni Mungu Mwenyewe. Na akiwa katika sura ya mwanaume kwa mfano, basi huyo si Yeye (s.w.t) bali ni kiumbe mionganoni mwa viumbe Wake (s.w.t). Na wakati huo itasemwa: Hakika yeye alimuona Mola Wake Mlezi kwa ujumla kwa hekima inayodhihiri kwa wafasiri kwa kusema: Inajulisha juu ya hili na lile.

**Na imesemekana kuwa: Ni Yeye mwenyewe, na kumzingatia**

<sup>43</sup> Na tunajiweka mbali kusema hayo juu ya Mwenyezi Mungu (s.w.t)!!

<sup>44</sup> Ni maneno yasiyofaa, na wala hayana maana! Vipi liwe (jambo lake linajulikana) je, muumbaji (a.j) anajulikana umbo lake na sura yake na mwonekano Wake?! Na maneno hapa yamezingirwa katika umbo (shakli), sura na maumbile, kwa sababu kadhia hapa nayo ni uonekanaji ambaa haufungamani ila kwa mambo haya, vyovoyote atakavyoribu kuwabebesha hilo wabebaji na wafanya taawili. Na maneno haya ni hatari mno, kwa sababu ndani yake kuna shetani anajifananisha na Mwenyezi Mungu na anajiweka sura Yake! Sio hili ila upotoshaji wa wazi wanamfanya Yeye picha picha ya elimu na maarifa. Ametukuka Mwenyezi Mungu utukukaji mkubwa na wa mbali mno!

kuwa ni Yeye kwa sura hii ni kwa ubongo wa rai na maoni, lakini ukweli sio Mola Manani (s.w.t).

Na hakika mmoja wa masufi alisema: Hakika yeye amemuona Mola Wake Mlezi usingizini kwa wasifu wake, akaulizwa: Vipi ulimuona, akasema: Aligeuza macho yangu katika moyo wangu basi nikawa mwili mzima ni macho, nikamuona ambaye hafanani na chochote.

Na kati ya yale tuliyoyaeleza juu ya paragrafu za Imam Nawawi na Allamah Bajuri  inabainika kwako uovu wa dalili za wase-maji kuhusu suala la kuonekana kwa Mwenyezi Mungu na kwamba msingi wake umejengeka juu ya ufuataji na sio uhakiki, na yatosha kuunganisha mzingatiaji hadi kufahamu yale yanayopatikana kuto-kana na makosa na ugeuzaji wa maneno!

Hakika tumejaribu kulifanyia utafiti suala hili kwa kadri ya nguvu na uwezaji na kutoa dalili mbalimbali na hoja nyingi za wanaoamini hilo, pamoja na kubainisha daraja ya hoja hizo na nguvu za dalili zao. Na ninamuomba Mwenyezi Mungu (s.w.t) zoezi hili liwe na faida kwa watu wa elimu, na Mwenyezi Mungu (s.w.t) ndiye Mwenye kusema haki. Naye anaongoza njia. Na shukurani zote ni za Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu.

---

## **ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION**

---

1. i) Qur'an Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili  
ii) Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhangwa wa Imam Hussein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imam Ali (a.s.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudhar
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu

27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua kwa Mujibu wa Ahlulbayt (a.s)
33. Udhuu kwa Mtazamo wa Qur'ani na Sunna
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Qur'ani na Kuhifadhiwa Kwake
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya Sala Mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipyta
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an Yatoa Changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina - 'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu

58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatoo
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Dhana ya Ndoa ya Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raj'ah)
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema

89. Adabu za Sokoni Na Njiani
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali (AT- TAWASSUL)
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Maimamu wa Ahlul Bait – Ujumbe na Jihadi
100. Idi Al-Ghadir
101. Kusoma sura zenyе Sijda ya wajibu
102. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunna za Nabii Muhammad (saww)
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Mwanamke Na Sharia
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqlain
115. Ndoa ya Mutaa
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne

120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vy'a kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vy'a kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul l'Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu
135. Adhana ni Ndoto au ni Wahyi?
136. Tabaruku
137. Saada Kamili – Kitabu cha Kiada cha Maadili
138. Vikao vy'a furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vy'a wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mjadala wa Kiitikadi
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu

151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swalaa ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Shia na Qur'ani – Majibu na Maelezo
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlis za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. as-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)

182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali Ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Historia maana na lengo la Usalafi
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Upotoshaji Dhahiri katika (Turathi) Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina (as) na Makhalifa
197. Tawheed Na Shirki
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni waKisunni na Kishia (Al- Muraja'aat)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Imam Husain ni Mfumo wa Marekebisho na Mageuzi
206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura
211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza

213. Imam Ali na Mambo ya Umma
214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa
215. Uimamu na Tamko la Kutawazwa
216. Mfumo wa Wilaya
217. Vipi Tutaishinda Hofu?
218. Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo
219. Maeneo ya Umma na Mali Zake
220. Nahju 'L-Balagha— Majmua ya Khutba, Amri, Barua, Risala, Mawaidha na Semi za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (a.s.)
221. Mukhtar – Shujaa aliyelipiza kisasi dhidi ya wauaji wa Imam Husein (as) hapo Karbala
222. Mazingatio Katika Swala
223. Imam Hasan na Mfumo wa Kujenga Jamii
224. Vyakula Na Vinywaji
225. Kuelewa Rehema ya Mwenyezi Mungu
226. Imam Mahdi na Bishara ya Matumaini
227. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
228. Shia Na Sahaba - Majibu na Maelezo
229. Majanga Na Jukumu la Jamii
230. Shia Na Hadith - Majibu na Maelezo
231. Upotofu Ndani ya Kitabu cha Mitaala kwa Shule za Sekondari
232. Ugaidi Wa Kifikra Katika Medani Ya Kidini
233. Yafaayo kijamii
234. Uswalihina Dhahiri Na Batini Yake
235. Mkakati wa Kupambana na Ufakiri
236. Mwanamke Katika Harakati Za Mageuzi
237. Jihadi
238. Hija Katika Maneno Na Ujumbe Wa Imam Khomeini (R.A)
239. Tiba Ya Maradhi Ya Kimaadili
240. Yusuf Mkweli
241. Taqiyya Kwa Mujibu Wa Sheria Ya KIISLAMU

242. Imam Mahdi (A.S) Imam Wa Zama Hizi Na Kiongozi Wa Dunia
243. Talaka Tatu
244. Safari Ya Kuelekea Kwa Mwenyezi Mungu
245. Hotuba Za Kiislamu Juu Ya Haki Za Binadamu
246. Mashairi Ya Kijamii
247. Ngano Ya Kwamba Qur'ani Imebadilishwa
248. Wito Kwa Waumini: "Enyi Mlioamini"
249. Imam Husain (a.s) ni Utu na Kadhibi
250. Imam Husain ni Kielelezo cha Kujitoa Muhanga na Fidia
251. Imam Mahdi ni Tumaini la Mataifa
252. Kuchagua Mchumba
253. Mazungumzo ya Umoja – Ukossoaji na Usahihishaji
254. Utamaduni wa Mwamko wa Kijamii
255. Hekima za kina za Swala
256. Kanuni za Sharia za Kiislamu
257. Utamaduni kufuatana na Qur'ani na Utekelezaji wa Kivitendo  
(Sehemu ya Kwanza)
258. Kauli sahihi zaidi katika kufafanua Hadithi